# MABADILIKO YA KISEMANTIKI YA MANENO KATIKA LUGHA YA KIKAMBA: MTAZAMO WA KIDAYAKRONIA

ANGELA NTHENYA MUSYOKA

Kazi hii Imewasilishwa kwa ajili ya Kutosheleza Baadhi ya
Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Chuo
Kikuu cha Machakos, Kenya

SEPTEMBA 2025

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na wala haijawasilishwa au kutahiniwa katika chuo kingine chochote.

____________________ 26-09-2025

Angela Nthenya Musyoka Tarehe

C50-12733-2017

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ajili ya utahini wa shahada ya uzamili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Machakos.

____________________ 08/09/2025

Dkt. Makoti Vifu Tarehe

Idara ya Isimu na Lugha

Chuo Kikuu cha Machakos

____________________ 30/09/2025

Dkt. Mutua John Tarehe

Idara ya Isimu na Lugha

Chuo Kikuu cha Machakos

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia familia yangu. Mume wangu mpendwa Augustus kwa ushirikiano katika kazi hii, watoto wangu Caroline, Peter Ronney na Mark. Elimu ni bahari haina mwisho.

# SHUKURANI

Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, nguvu, fikira na uwezo wa kuiandika kazi hii. Bila msaada wa Mungu uandishi wa tasnifu hii usingewezekana kamwe. Shukrani zangu za pekee ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Vifu Makoti na Dkt. John Mutua kwa kujitwika jukumu hili zito. Mwenyezi Mungu awaneemeshe neema anuwai.

Sitasahau uongozi wa Chuo Kikuu cha Machakos kwa msaada mkubwa kwangu licha ya udhaifu wangu kama mwanafunzi pamoja na changamoto chungu nzima zilizonikabili wakati wa kozi hii. Mmeniongoza vyema. Sina cha kuwalipa ila ninawaombea maisha marefu.

Mume wangu mpendwa, umeandamana nami kila hatua. Madhila yangu yalikuwa yako na ulikuwa msaada wakati wa uhitaji. Wema wako kwangu siuchukulii kuwa jambo la kawaida katu! Mola akubariki na akujalie karama tele.

Wazazi wangu Bw. Andrew Musau na Bi. Petronilla Mueni, asanteni sana! Wema wenu haulipiki hapa duniani ila mbinguni tu! Mlijinyima mali mkawa wanyonge wa hali kusudi nipate mustakabali mwema. Mola awajalie afya, hekima na furaha, mzidi kuwafaa wengine.

# YALIYOMO


UNGAMO...ii
TABARUKU ...iii
SHUKURANI ...iv
IKISIRI ...viii
ABSTRACT...ix
FAHARASA ...x
UFAFANUZI WA DHANA KUU ...xi
VIFUPISHO...xii
ORODHA YA MAJEDWALI ...xiii
ORODHA YA VIAMBATISHO...xiv
SURA YA KWANZA ...1
UTANGULIZI ...1
1.0 Utangulizi...1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ...1
1.1.1 Historia ya Biblia ...2
1.2 Suala la Utafiti ...5
1.3 Malengo ya Utafiti ...6
1.4 Maswali ya Utafiti...6
1.5 Sababu za Kuteua Mada...6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ...7
1.7 Upeo wa Utafiti...8
1.8 Kiunzi cha Nadharia ...9
SURA YA PILI...15
YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA...15
2.0 Utangulizi...15
2.1 Maana na Mabadiliko ya Maana...15
2.2 Michakato ya Mabadiliko ya Maana...18
2.3 Sababu za Mabadiliko ya Maana ...23
2.4 Pengo la Utafiti ...30
2.5 Hitimisho...30
SURA YA TATU ...32
MBINU ZA UTAFITI NA UCHANGANUZI WA DATA ...32
3.0 Utangulizi...32

3.1 Eneo la Utafiti ........ 32
3.2 Sampuli ya Utafiti ........ 32
3.3 Vifaa vya Utafiti ........ 34
3.4 Mbinu za Kukusanya Data ........ 35
3.5 Mbinu za Kuchanganua na Kuwasilisha Data ........ 36
3.6 Maadili katika Utafiti ........ 38
3.7 Hitimisho ........ 38
SURA YA NNE ........ 39
UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA ........ 39
MABADILIKO YA KISEMANTIKI YA MANENO YA KIKAMBA ........ 39
4.0 Utangulizi ........ 39
4.1 Mabadiliko ya Kisemantiki ya Nomino na Vitenzi ........ 39
4.1.1 Kundi la Nomino katika Biblia ........ 40
4.1.1.1 Maana ya nomino kwa mujibu wa Muktadha ........ 42
4.1.1.2 Maana ya Nomino kwa mujibu wa wazee ........ 64
4.1.1.3 Maana ya Nomino kwa mujibu wa watoto ........ 74
4.1.2 Kundi la Vitenzi katika Biblia ........ 88
4.1.2.1 Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa Muktadha ........ 91
4.1.2.2 Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa wazee ........ 102
4.1.2.3 Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa watoto ........ 110
4.2 Michakato ya Kisemantiki inayosababisha Kubadilika kwa Maana ........ 118
4.2.1 Usogezi wa Maana ........ 118
4.2.1.1 Sitiari ........ 119
4.2.1.2 Sinedoche ........ 120
4.2.2 Upanuzi wa Maana ........ 120
4.2.3 Ubanaji wa Maana ........ 122
4.2.4 Usambaratikaji wa Maana ........ 125
4.2.5 Uimarikaji wa Maana ........ 126
4.2.6 Tasfida ........ 127
4.2.7 Utowekaji wa Maana ........ 128
4.2.8 Kuhamisha maana ........ 129
4.3 Sababu za Mabadiliko ya Maana za Maneno ........ 133
4.3.1 Maendeleo ya Jamii ........ 133
4.3.2 Kupotea kwa motisha ya matumizi ........ 134
4.3.3 Upolisemia wa maneno ........ 135

4.3.4 Ukuruba wa maana .......... 136
4.3.5 Maneno Mwiko katika Jamii .......... 137
4.3.6 Uzalishaji wa maana potovu .......... 138
4.3.7 Unasibu wa alama za Kiisimu .......... 139
4.4 Hitimisho .......... 140
SURA YA TANO .......... 141
MUHTASARI NA MAPENDEKEZO .......... 141
5.0 Utangulizi .......... 141
5.1 Matokeo ya Utafiti .......... 141
5.2 Hitimisho .......... 144
5.3 Mapendekezo .......... 145
MAREJELEO .......... 147
KIAMBATISHO I .......... 152
MASWALI YA KUONGOZA MAHOJIANO .......... 152
KIAMBATISHO II .......... 154
MANENO YALIYOBADILIKA MAANA .......... 154
KIAMBATISHO III .......... 156
MANENO YALIYOTEULIWA KUTOKA B1 NA B2 .......... 156
KIAMBATISHO IV .......... 157
KIAMBATISHO V .......... 158

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno ya Kikamba kwa mtazamo wa kidayakronia. Ulitalii jinsi maneno ya Kikamba yalivyobadilika maana kuanzia mwishoni mwa karne ya ishirini (20) (miaka ya sabini) hadi karne ya 21. Aidha, ulichunguza sababu za mabadiliko hayo. Uchunguzi ulifanywa kaunti ndogo ya Mwala katika Kaunti ya Machakos ukiwalenga wazungumzaji wa lahaja ya *Kĩmasaku*. Hii ndiyo lahaja ambayo mtafiti pamoja na wakazi wengi wa kaunti ndogo ya Mwala huzungumza. Utafiti uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Dhana ambayo inashikilia kwamba maana ya neno ni dhana au taswira inayoibuliwa na neno hilo akilini mwa mwanalugha wakati neno hilo linapotamkwa; na Nadharia ya Nyanja za Kisemantiki inayoeleza kwamba maneno hayafai kuchukuliwa kama vipashio huru vinavyojitegemea, bali yanafaa kuhusishwa na mengine yanayohusiana kimaana. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza nomino na vitenzi ambavyo vimebadilika maana, kubainisha mabadiliko ya kisemantiki katika maneno hayo, kutathmini michakato ya kisemantiki inayohusishwa na mabadiliko hayo na kuchunguza sababu za mabadiliko hayo ya maana katika maneno ya Kikamba. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na ya maktabani. Maneno yalikusanywa kutoka Biblia za Kikamba; *Mbivilia* (UBS, 1974) na *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (IT, 2011). Vitabu vinne (4) vya Biblia viliteuliwa kwa kutumia usampuli wa makusudi: *Mwanzo* na *Zaburi* katika Agano la Kale na *Luka* na *Mathayo* katika Agano Jipya. Maneno mia mbili (200) yaliteuliwa kimakusudi kutoka kwenye Biblia hizi mbili; nomino mia moja na kumi na sita (116) na vitenzi themanini na vinne (84). Fomyula ilitumiwa kupunguza maneno haya hadi hamsini (50). Mtafiti aliteua nomino thelathini (30) kimakusudi, kumi na tano (15) kutoka *Mbivilia* (1974) na kumi na tano (15) kutoka *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (2011). Vilevile, vitenzi ishirini (20) viliteuliwa kimakusudi, kumi (10) vikitolewa kwenye *Mbivilia* (1974) na kumi (10) kwenye *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (2011). Wahojiwa walikuwa wanaume watano (5) na wanawake watano (5) wenye umri wa miaka sabini na mitano (75) na zaidi na wavulana watano (5) na wasichana watano (5) ambao umri wao ni kati ya miaka kumi (10) hadi kumi na minne (14). Wote waliteuliwa kwa njia ya makusudi. Wazee hawa walijua maana ya maneno hayo kwa kuwa wameishi katika kipindi kinachotafitiwa na ndio mashahidi wa mabadiliko ya kisemantiki ya maneno ya Kikamba kuanzia mwishoni mwa karne ya 20 hadi karne ya 21. Data ilichanganuliwa kwa kulinganisha majibu ya wahojiwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wasomaji wa matini za Kikamba kuelewa maana za maneno kama yalivyotumika katika Biblia za awali hasa Biblia iliyochapishwa mwaka wa 1974 na maana mpya ya maneno hayo kwa mujibu wa Biblia iliyochapishwa mwaka 2011. Yataongezea tafiti zilizopo za kiisimu hasa kuhusu mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha. Ni matumaini ya mtafiti kwamba kizazi cha sasa kitaelewa maana za maneno yanayopatikana katika matoleo ya awali ya Biblia ya Kikamba.

# ABSTRACT

This study investigated the semantic change of words in Kikamba language diachronically. It studied how Kikamba words have changed in meaning from late 20th century (1970s) to the 21st century. It also explored why this has happened. The study was done in Mwala sub-county in Machakos County, targetting the speakers of *Kĩmasaku* dialect. This is the dialect spoken by both the researcher and majority of the residents of Mwala sub-county. The study was guided by two theories: Conceptual Theory which states that the meaning of a word is the concept that is formed in the mind of the linguist when the word is spoken; and the Semantic Field Theory which states that words should not be treated in isolation but in relation to their semantically related words or their semantic fields. The objectives of the study were to identify nouns and verbs that have changed meaning in Kamba language, to identify the csemantic changes that have affected the nouns and verbs, to investigate the semantic processes involved and to investigate the causes of semantic change of those words. Data was collected through interviews and the library. Words were collected from two Kikamba Bibles, *Mbivilia* (UBS,1974) and *Mbivilia Kĩkamba kya Ĩvinda Yĩĩ,* (IT, 2011). Four books of the Bibles were selected through purposive sampling: *Genesis* and *Psalms* in the Old Testament and *Luke* and *Matthew* in the New Testament. From the two Bibles, two hundred (200) words were selected purposively, one hundred and sixteen (116) nouns and eighty- four (84) verbs. A formular was used to reduce the words to fifty (50). The researcher purposively chose thirty (30) nouns, fifteen (15) from *Mbivilia* (1974) and fifteen (15) from *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (2011). Similarly, twenty (20) verbs were chosen purposively, ten (10) from *Mbivilia* (1974) and ten (10) from *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (2011). The interviewees included five (5) men and five (5) women aged seventy- five (75) years and above and five (5) boys and five (5) girls between the ages of ten (10) and forteen (14) years who were selected through purposive sampling. The old men and women were to give the meaning of these words because they have lived during the period in question and are witnesses of the semantic change of words in Kamba language during the late 20th and the 21st centuries. Data was analysed by comparing the responses of the respondents and was presented using descriptive method according to the objectives of the study. The study will help readers of Kamba texts to understand the meanings of words as used in the earlier Bibles especially the Bible published in 1974 and the new meanings of those words as used in the Bible published in 2011. It will also add to linguistic research especially on change of meaning of words in a language.

# FAHARASA

| | |
|---|---|
| Dayakronia: | Diachrony |
| Isimu historia: | Historical linguistics |
| Kiunzi cha nadharia: | Theoretical framework |
| Maadili katika utafiti: | Ethical Issues |
| Elimu inayojikita katika Umilisi: | Competence Based Curriculum |
| Mwiko: | Taboo |
| Nadharia ya Dhana: | Conceptual Theory |
| Nadharia ya Nyanja za Kisemantiki: | Semantic Field Theory |
| Ubanaji: | Restriction |
| Usambaratikaji; | Deterioration |
| Uimarikaji: | Amelioration |
| Upanuzi: | Expansion |

# UFAFANUZI WA DHANA KUU

| | |
|---|---|
| Biblia ya Zamani: | Biblia iliyochapishwa mwaka 1974, chapa ya UBS. |
| Biblia ya Kisasa: | Biblia iliyochapishwa mwaka 2011, chapa ya IT. |
| Dayakronia: | Mapito ya wakati au nyakati tofauti kihistoria. Katika utafiti huu ni kuanzia mwishoni mwa karne ya ishirini (20) hadi karne hii ya ishirini na moja (21). |
| Dhana: | Wazo lisilo bayana wala la hakika lakini ambalo mtu au jamii huwa nalo na kulipendekeza kwa wengine ili lizidi kuchunguzwa. |
| Fahiwa: | Mfumo wa mahusiano ya kiisimu baina ya faridi moja ya kileksia na faridi nyingine. |
| Isimu Historia: | Tawi la isimu ambalo huchunguza mabadiliko ya lugha kiwakati. |
| Jamii-lugha: | Kundi la watu ambao ni wazungumzaji wa lugha moja au wazawa wa lugha moja. |
| Kiashiria: | Umbo fulani la kusemwa au kuandikwa ambalo huwakilisha dhana fulani. |
| Kiashiriwa: | Kitu halisi katika ulimwengu halisi kwa mfano nyumba au gari. |
| Kikamba cha kale: | Kikamba kilichoandikwa katika matini za kale zilizoandikwa au kuchapishwa kabla ya karne ya ishirini na moja (21). |
| Kikamba cha sasa: | Kikamba ambacho kimeandikwa katika matini nyingi katika karne hii ya ishirini (20) na ambacho huzungumzwa na watoto wa umri wa miaka kumi (10) hadi kumi na minne (14). |

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| B1: | Biblia ya Kikamba chapa ya UBS lililochapishwa mwaka wa 1974 |
| B2: | Biblia ya Kikamba chapa ya IT lililochapishwa mwaka wa 2011 |
| CBC: | Competence Based Curriculum |
| IT: | Interconfessional Translation (of the Bible) |
| Ktk.: | Katika |
| Lk.: | Luka |
| Mat: | Mathayo |
| Mch: | Mchoro |
| Mw: | Mwanzo |
| M.Y: | Mifano yangu |
| N: | Nomino |
| n.w: | Na wengine |
| T: | Kitenzi |
| Taz: | Tazama |
| UBS: | United Bible Society |
| Uk: | Ukurasa |
| Zab: | Zaburi |

# ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 3.1: Michakato ya Kisemantiki inayoathiri Nomino na Vitenzi (M.Y)..........37

Jedwali 4.1: Maana za Nomino kwa mujibu wa Muktadha........................................63

Jedwali 4.2: Maana ya nomino kwa mujibu wa wazee..............................................73

Jedwali 4.3: Maana ya Nomino kwa mujibu wa watoto.............................................85

Jedwali 4.4: Maana ya vitenzi kwa mujibu wa muktadha ........................................101

Jedwali 4.5: Maana ya vitenzi kwa mujibu wa Wazee ............................................108

Jedwali 4.6: Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa watoto ............................................116

Jedwali 4.7: Muhtasari wa michakato ya Kisemantiki katika Nomino na Vitenzi....131

# ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Maswali ya Kuongoza Utafiti……………………………………….152

Kiambatisho II: Maneno yaliyobadilika Maana……………………………….........154

Kiambatisho III: Maneno yaliyoteuliwa kutoka B1 na B2.…………………………156

Kiambatisho IV: Idhini ya Chuo cha Machakos……………….……………………...157

Kiambatisho V: Idhini ya NACOSTI……………………………………………….158

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ina maelezo ya kimsingi kuhusu utafiti. Tumefafanua usuli wa suala la utafiti. Tumebainisha suala la utafiti kwa kueleza dhana ya mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha ya Kikamba kwa kurejelea Biblia ya Kikamba chapa ya UBS (1974) na Biblia ya Kikamba chapa ya IT (2011). Tumeeleza malengo ya utafiti na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Sababu za kuchagua mada zimeelezwa. Tumefafanua umuhimu wa utafiti na kubainisha mipaka ya utafiti. Aidha, nadharia zilizoongoza utafiti zimefafanuliwa.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Lugha ni mfumo wa sauti nasibu na ishara za kisarufi ambazo kwazo watu wa jamii fulani ya lugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao (Habwe & Karanja, 2007). Sauti hizi huwa na maana. Kila jamii ina lugha yake ya kipekee inayoendeleza mawasiliano ya kila siku. Lugha hubeba utamaduni, nao utamaduni hubadilika kwa mujibu wa mapito ya wakati. Mahitaji ya jamii hupanuka au kuongezeka na kusababisha uundaji wa leksimu mpya, ukopaji wa msamiati na upanuzi wa maana ili kukidhi mahitaji mapya ya kimawasiliano. Kwa mfano, vifaa vipya vinapobuniwa katika jamii huundiwa msamiati mpya au kuwasilishwa kwa kutumia hazina ya msamiati katika jamii, nao msamiati huo hupata maana ya ziada. Kipengele kimoja cha utamaduni kinapopotea basi maana husika hudondoshwa.

Campbell (2004) anasema kwamba maneno mengi katika lugha ni ya kipolisemia. Kadri muda unavyopita maana zaidi huingizwa katika lugha na kusababisha maana za maneno hayo kuongezeka au kubadilika.

Neno linaweza kudumisha maana ya msingi huku pia likiendelea kupata maana nyingine za ziada (Ullman, 1972). Maana hizi za ziada huweza kupata mashiko na kutumiwa zaidi kuliko ile maana ya msingi. Mabadiliko ya maana yanapotokea huathiri mawasiliano. Iwapo maneno yanayotumiwa na mzungumzaji hayaeleweki kwa mpokeaji wa ujumbe, basi wawili hao hawataelewana. Hivyo basi mabadiliko ya lugha ni sharti yachunguzwe mara kwa mara ili mawasiliano baina ya jamii-lugha yawe ya kufana.

Katika karne hii ya ishirini na moja, lugha huendelea kubadilika kutokana na mwingiliano wa kijamii, kitamaduni, kiteknolojia na kidini. Mabadiliko haya hujitokeza katika maana za maneno hasa katika nomino na vitenzi. Maneno haya hutumika kila siku katika mawasiliano. Katika lugha ya Kikamba, maandiko ya kale kama vile matini za kidini yamehifadhi msamiati ambao umebadilika maana au hautumiwi katika mawasiliano. Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba kwa kutumia Biblia Takatifu ya Kikamba ya mwaka wa 1974 chapa ya UBS inayojulikana kama *Mbivilia.* Aidha, Biblia ya Kikamba iliyochapishwa mwaka 2011 inayofahamika kama *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* ilitumiwa kusaidia kubainisha maneno ambayo yamebadilika maana.

### 1.1.1 Historia ya Biblia

Biblia ni muhimu sana katika Ukristo wa Kiafrika na ndicho kitabu kinachosomwa zaidi kuliko vitabu vinginevyo katika ukanda wa Afrika Mashariki (Mugambi, 1995). Biblia hupatikana kwa urahisi katika maeneo ya miji sawa sawa na mashambani. Aidha,

tunaweza kusema kwamba hiki ndicho kitabu kilicho na uwezo wa kuteka makini ya watu wengi, hasa Wakristo. Historia ya Biblia ya kwanza Afrika Mashariki inaenda sambamba na chimbuko la dini ya Kikristo katika ukanda huu wa Afrika Mashariki (Musyoka na Ireri, 2019), katika karne ya kumi na tisa (19). Wamishonari wa kikristo walipowasili katika pwani ya Afrika Mashariki katikati ya karne ya kumi na tisa (19), walianza jaribio la kutafsiri Maandiko Matakatifu (Biblia) kwa lugha za Kiafrika. Lengo lao lilikuwa ni kuwawezesha Waafrika waongofu kuisoma Biblia katika lugha waliyoielewa vizuri. Katika kipindi hiki cha kutafsiri Biblia, utalii wa kina wa lugha za Kiafrika na utamaduni wa Waafrika haukuwa umefanywa. Jambo hili lilizua changamoto kubwa katika kazi ya kutafsiri Biblia. Lengo la mfasiri lilikuwa kuwasilisha Neno la Mungu kama lilivyoandikwa bila kubadilisha ujumbe kwa namna yoyote. Jambo hili lilisababisha tafsiri halisi.

Tafsiri kwa kawaida ni kazi isiyokamilika na tafsiri yoyote huhitaji kufanyiwa marekebisho na hatimaye kazi hiyo itafsiriwe tena kulingana na jinsi lugha inavyobadilika ili kukidhi mahitaji ya utamaduni unaobadilika katika jamii (Nida, 1982). Tafsiri ya kwanza ya Biblia katika lugha ya Kikamba ilifanywa na Mmishonari Ludwing Krapf. Hii ndiyo iliyokuwa tafsiri ya pili kufanywa katika lugha ya Kiafrika nchini Kenya, ya kwanza ikiwa ya Kiswahili. Krapf alitafsiri *Injili ya Mtakatifu Marko* mwaka wa 1850. Wamishonari wengine Hoffman, Pfitzinge na Ernest Brutzer wa Misheni ya Leipzing nao wakatafsiri *Injili ya Mtakatifu Luka* mwaka wa 1898, kitabu cha *Matendo ya Mitume* mwaka wa 1904 na *Injili ya Mtakatifu Mathayo* mwaka wa 1909. Katika tafsiri zilizotajwa hapa, Kikamba kilichotumiwa kilikuwa kigumu kwa wazungumzaji asilia kuelewa kwa kuwa kilikuwa hakiendani na kanuni za sarufi ya Kikamba. Kwa hivyo kikundi cha wafasiri kilichoongozwa na mmishonari George W. Rhoad kilitafsiri tena *Injili ya Mtakatifu Marko* mwaka wa 1915, *Injili ya Mtakatifu*

*Yohane* mwaka wa 1916 na kitabu cha *Danieli* mwaka wa 1935. Wakamba waliosaidia kufanya tafsiri hii walikuwa Aaron Kasyoki na Jeremiah Kyeva kutoka Kangundo, Machakos (Mojola, 2020).

Hatimaye, kikundi cha Wamishonari katika Bara Afrika (African Inland Mission) kwa usaidizi wa wenyeji kiliendeleza tafsiri ya vitabu vilivyosalia na mnamo mwaka wa 1956, Biblia nzima ya Kikamba ilikuwa imetafsiriwa lugha ya Kikamba. Biblia hiyo ilipewa jina *Maandĩko Matheu ma Ngai Metawa Mbivilia Nĩmo Utianĩo wa Tene na Mweũ* (Maandiko Matakatifu ya Mungu yanayoitwa Biblia ambayo ni Agano la Kale na Jipya). Biblia hii ilichapishwa na *British Foreign Bible Society* (Waruta, 1975).

Tafsiri ya Biblia katika lugha ya Kikamba ilifanywa kwa ushirikiano mkubwa wa wamishonari wa Kikristo, lakini wazungumzaji asilia wa lugha ya Kikamba walitelekezwa. Hawakuhusishwa kikamilifu, na ndiyo maana hali ya kilahaja iliyopo Ukambani haikuzingatiwa. Kwa mfano baadhi ya lahaja zilipuuzwa wakati wa kutafsiri Biblia. Lahaja iliyopewa kipaumbele ni ile inayozungumzwa katika eneo la *Masakũ* (Machakos) ambayo inaitwa *Kĩmasakũ* (Mojola, 2020). Biblia ya kwanza ya Kikamba ilikuwa na makosa mengi ya uvuguvugu wa maana na makosa ya sarufi kutokana na mwelekeo wa wafasiri wa kufanya tafsiri halisi na pia ukosefu wa umilisi katika lugha ya Kikamba. Kuanzia mwaka wa 1960 hadi 1966, kazi ya kurekebisha makosa ya Biblia hii ilianza. Makosa yalirekebishwa na hati kukuzwa. Biblia iliyorekebishwa ilichapishwa mwaka wa 1974 na Biblia hii ikakubaliwa na makanisa Ukambani. Toleo hili lilizingatia lahaja ya Kimasaku kama lahaja iliyo sanifu (Dube & Wafula 2017). Toleo hili la 1974 ndilo linalotumika sana miongoni mwa Wakamba.

Mnamo mwaka wa 2011, tafsiri nyingine ya Biblia ilifanywa kwa kutumia Kikamba sanifu na kuchapishwa na Chama cha Biblia nchini Kenya (Bible Society of Kenya).

Kazi ya tafsiri ilifanywa kwa ushirikiano wa Wakamba wa maeneo mbalimbali kwa hivyo haikuwa na upendeleo. Baadaye mwaka wa 2015, msomi mwanathiolojia wa Kiafrika Mbiti alitafsiri Biblia Agano Jipya kutoka Biblia ya Kigiriki. Sababu ya kufanya tafsiri hii ni kuwa alidai kuwa alipata changamoto akitumia Biblia iliyochapishwa 2011. Biblia hii haijapata uungwaji mkono kwa kuwa Mbiti aliiandika peke yake na huenda ikaathiriwa na ubinafsishaji wa ujumbe na maana. Biblia iliyochapishwa mwaka wa 1974 imepata umaarufu miongoni mwa Wakamba na ndiyo inayopatikana kwa wingi katika madhehebu ya Kikristo Ukambani. Utafiti wetu ulijikita katika Biblia ya Kikamba chapa ya UBS (1974) na chapa ya IT (2011). Mtafiti hakuangalia jinsi maana ilivyopotoka katika Biblia zilizotajwa, bali jinsi maana ilivyobadilika kwa mujibu wa Biblia hizo mbili.

## 1.2 Suala la Utafiti

Biblia ya Kikamba iliyochapishwa mwaka 1974 bado inaendelea kutumika makanisani na katika hafla kama vile harusini, licha ya kuwa baadhi ya msamiati wake haueleweki maana miongoni mwa kizazi cha karne hii ya 21. Baadhi ya nomino na vitenzi havitumikikwa maana ile ile katika Kikamba cha sasa. Hali hii inaleta mkanganyiko katika uelewa wa ujumbe uliokusudiwa kwa watumiaji wa leo. Ingawa tafiti nyingi za kiisimu zimechunguza mabadiliko ya kisemantiki katika lugha mbalimbali, lugha ya Kikamba haijafanyiwa utafiti wa kutosha katika nyanja hii. Hakuna utafiti wa kina uliofanywa kueleza mabadiliko ya kisemantiki ya nomino na vitenzi vya Kikamba, hasa vilivyo katika Biblia ya kale. Pana pengo la kitaaluma katika kubainisha na kufafanua mabadiliko ya kisemantiki ya baadhi ya nomino na vitenzi katika lugha ya Kikamba. Jambo hili litarahisisha uelewa wa matini za kale na kudumisha matumizi wa lugha ya Kikamba kwa vizazi vijavyo.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba kwa mtazamo wa Kidayakronia. Malengo ya utafiti huu yalikuwa:

i. Kuchunguza nomino na vitenzi vilivyobadilika maana katika Biblia ya 1974 na ile ya 2011.

ii. Kubainisha mabadiliko ya kisemantiki katika nomino na vitenzi.

iii. Kutathmini michakato ya kisemantiki inayohusishwa na mabadiliko hayo.

iv. Kuchunguza sababu za mabadiliko ya maana ya nomino na vitenzi hivyo katika lugha ya Kikamba.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Ni nomino na vitenzi gani ambavyo vimebadilika maana katika Biblia ya Kikamba ya 1974 na ile ya 2011?

ii. Ni mabadiliko gani ya kisemantiki yanayobainika katika nomino na vitenzi?

iii. Ni michakato gani ya kisemantiki inayohusishwa na mabadiliko hayo?

iv. Ni sababu gani zilisababisha mabadiliko hayo?

## 1.5 Sababu za Kuteua Mada

Mtafiti aligundua kuwa baadhi ya maneno katika vitabu vya dini vilivyoandikwa kabla ya au katika karne iliyopita ya ishirini (20) yana maana ambazo hazieleweki na kizazi cha leo. Baadhi ya msamiati uliotumiwa katika Biblia za kale kama vile *Mbivilia* (1974) hautumiwi katika mazungumzo ya kawaida ingawa Biblia zenyewe zinasomwa makanisani, nyumbani na katika hafla za arusi au mazishi. Waumini wengi

wanaosikiliza mahubiri kutoka Biblia hizo hawaelewi maana iliyokusudiwa ya baadhi ya maneno, hivyo pana haja ya kuchunguza iwapo maneno hayo yamepata maana zaidi au yamepata maana ya ziada na kuoanisha maana hizo na usasa. Aidha, jamii hubadilika kadiri wakati unavyopita. Jamii inapobadilika viungo vyake hubadilika pia. Lugha ni kiungo hai cha jamii na haina budi kubadilika. Baada ya kipindi kirefu mabadiliko hayo yanaweza kuzua maana zilizo tofauti kabisa na maana asilia. Hivyo basi mtafiti aliona haja ya kuchunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba. Afafanue ni maneno yapi yamebadilika maana na yapi yamekufa ingawa kuna maneno mapya kwa maana ileile.

Aidha, watoto Wakamba waliozaliwa katika karne hii ya ishirini na moja huzungumza Kikamba cha leo kilichojaa misamiati ya Kiingereza na Sheng'. Watoto hawa hawaelewi Kikamba cha miaka ya nyuma ambacho kipo katika Biblia. Hii inawafanya watoto kutoelewa ujumbe katika Biblia hiyo. Kwa hivyo, kulikuwa na haja ya kuchunguza maana na kuonyesha mabadiliko ili watoto wanaposoma Biblia ya Kikamba cha kale waelewe ujumbe unaotolewa.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba kuanzia miaka ya sabini (1970) hadi sasa katika karne ya ishirini na moja (21). Ulichunguza mabadiliko hayo kuanzia miaka iliyotajwa kwa sababu tangu wakati huo hadi sasa imepita takriban miaka hamsini (50) na kama tujuavyo, lugha hubadilika kadri muda unavyoenda katika viwango mbalimbali. Lekisimu mpya huundwa, lekisimu hukopwa kutoka lugha nyingine, matamshi yakabadilika, maumbo ya lekisimu kubadilika au maana kuhamishwa. Vilevile ulichunguza sababu zinazochangia mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha ya Kikamba.

Matokeo ya utafiti huu yalikusudiwa kuwasaidia wasomaji wa matini za Kikamba hususan Biblia kuelewa maana mpya za lekisimu ambazo zimeibuka kuwasilisha maana ile ile ya zamani ya dhana fulani. Pia ni matumaini ya mtafiti kuwa kutokana na utafiti huu jamii ya leo itaelewa maana katika Biblia zilizotangulia hususan miaka ya sabini (1970). Utata uliopo wa kimawasiliano baina ya wazawa wa lugha ya Kikamba wanaoishi katika vipindi tofauti kihistoria, utapunguzwa na kudumisha dhima kuu ya lugha ambayo ni mawasiliano.

Vilevile utafiti huu una manufaa kwa waandishi wa vitabu katika kuunda kamusi za Kikamba. Jambo hili litakuza msamiati wa lugha ya Kikamba. Maneno ambayo maana inafifia au imekufa yalibainishwa ili kuhifadhi maneno na maana hizo. Aidha, matokeo ya upekuzi wa kitaaluma wa mada hii yatasaidia katika kuwahimiza watafiti wa isimu na lugha kuhusu hali ya lugha ya Kikamba na lugha nyinginezo za Kiafrika ili washirikiane na waundaji sera kuunda sera mwafaka za kudumisha lugha asili na kudhibiti kutoweka kwa maana. Pia mtaala mpya unaojikita katika umilisi ujulikanao kama C*ompetence- based Curriculum* (CBC) ambao ulianzishwa mwaka wa 2017 chini ya mfumo wa 2-6-3-3 unatilia mkazo ufundishaji wa lugha asilia za jamii. Utafiti huu utasaidia walimu na wanafunzi wa shule za msingi kujifunza Kikamba kama lugha ya kwanza. Aidha, waandishi wa vitabu watatumia matokeo ya utafiti huu kutunga vitabu kwa lugha ya Kikamba kukidhi mahitaji haya.

## 1.7 Upeo wa Utafiti

Kuna aina mbalimbali za mabadiliko ya lugha. Kwa mfano, mabadiliko ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Utafiti huu ulijikita katika mabadiliko ya kisemantiki pekee. Maneno pekee ndiyo yaliyochunguzwa kwa sababu neno ndicho kipashio kinachounda sentensi katika mazungumzo. Lugha ya Kikamba sawa na lugha

nyinginezo ina aina mbalimbali za maneno kama vile nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihusishi, viwakilishi na vihisishi. Tulilenga kutathmini tu mabadiliko ya kisemantiki ya nomino na vitenzi vya Kikamba kwa kuwa hivi ndivyo vipengele vya kimsingi katika lugha. Ni vigumu kuwa na sentensi kamilifu inayowasilisha ujumbe kwa msikilizaji au msomaji pasipokuwa na nomino au kitenzi au vyote viwili. Na hivyo maneno haya ndiyo huwezesha mawasiliano. Matini iliyotumika katika uchunguzi huu ni Biblia ya Kikamba (Mbivilia) iliyochapishwa mwaka wa 1974, chapa ya UBS na Biblia ya Kikamba cha sasa (Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ, IT, 2011) pekee ingawa zipo Biblia nyingi. Aidha, zipo matini nyingi za Kikamba ambazo ziliandikwa au kutafsiriwa kwa lugha ya Kikamba katika karne iliyopita kwa mfano *Mũtũnga na Ngewa yake* (Mbiti, 1967) lakini Biblia ilichaguliwa kimakusudi kwa kuwa inapatikana kwa urahisi katika jamii ya mtafiti.

## 1.8 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Dhana na Nadharia ya Nyanja za Kisemantiki. Nadharia ya Dhana iliasisiwa na John Locke (Ashworth, 2020). Mawazo ya Locke yalitokana na maoni ya wanaisimu wa kale kama vile Sapir na de Saussure, Ogden na Richards (Alawadi, 2020). Mwasisi wa nadharia ya Nyanja za Kisemantiki ni Trier (1934). Baadaye iliendelezwa na wataalamu wengine kama vile Firth (1951) na G. Miller (Crystal, 2010). Aidha, mikabala ya wanaisimu Ullman (1972), Palmer (1996), Leech (1981), Lyons (1981), Lyons (1999), Yule (2006) na Dirk Geeraerts (2010) kuhusu mabadiliko ya maana imejikita katika nadharia hii.

Nadharia ya Dhana ya Locke (Ashworth, 2020) inahusisha maana na dhana au taswira ya akilini. Mhimili mkuu wa nadharia hii ni kwamba maana ya leksimu ni dhana au taswira inayoibuliwa na leksimu hiyo akilini mwa mwanalugha wakati leksimu hiyo

inapotamkwa. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti kuwasaili wazee na watoto ili kupata maana mbalimbali za maneno yaliyoteuliwa kama data ya utafiti huu. Mihimili mingineyo ya nadharia ya dhana ni ifuatayo:

Maana ya maneno, misemo na sentensi hujengeka akilini mwa msikilizaji au mzungumzaji. Mawasiliano hufanyika iwapo msikilizaji amejenga dhana iliyokusudiwa na mzungumzaji. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuyatambua maneno ambayo hayakueleweka maana miongoni mwa watafitiwa wakati wa mahojiano.

Uhusiano kati ya leksimu na dhana ni wa moja kwa moja. Nadharia ya dhana huhusisha moja kwa moja maana na wazo, taswira au hisi badala ya kuhusisha maana na kitu moja kwa moja. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuchunguza maana za maneno kwa mujibu wa muktadha wa Biblia, mawazo ya wazee na mawazo ya watoto.

Mzungumzaji wa lugha huwa na taswira akilini mwake ikirejelea kitu halisia katika ulimwengu wa lugha. Kwa mfano neno *kĩvĩla* (kiti) linapotajwa, linaibua taswira fulani akilini mwa mzawa wa lugha ya Kikamba, taswira ya kifaa cha kukalia kwa jumla. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kutambua maneno yaliyobadilika maana kwa kuwa yeye ni mzawa wa jamii ya Wakamba na dhana za maneno katika lugha husika zimejengeka akilini mwake.

Dhana inayojengeka akilini mwa watu ni ile dhana inayotokana na imani, mitazamo na misimamo ya watu kuhusu jambo au kitu fulani. Kwa mfano neno *satani* (shetani) linaweza kuzua dhana ya kiumbe kibaya chenye pembe na sura mbaya au pengine mtu mbaya. Mhimili huu ulitumiwa kuchanganua nomino dhahania katika data ya utafiti kwa mfano *Asa* na *Mwĩai*.

Picha za akilini ni dhahania ya kutosha kuweza kuwakilisha maana za nomino au vitenzi vya kawaida. Kitu chochote kinapotajwa huibua taswira ya kitu hicho akilini

mwa mwanalugha. Mhimili huu ulitumika kuchunguza mabadiliko ya maana ya nomino na vitenzi vya kawaida katika lugha ya Kikamba.

Maana inayojengwa hutegemea zaidi ukomo wa fikra za msikilizaji au mzungumzaji. Kwa hivyo utofauti katika uwezo wa kujenga dhana akilini kuhusu leksimu fulani unaweza kupunguza au kubadili maana ya kitu kinachojengewa dhana. Kwa mfano mtu aliyezaliwa na kukulia kwenye mazingira duni ambapo watu hulala kwenye mabanda tu, akisikia neno *nyumba* limetumiwa, taswira inayojengeka akilini mwake inaweza kuwa ni banda. Maana ya neno *nyumba* itakuwa imepunguka. Mhimili huu ulikuwa faafu kwa utafiti huu kwa kuwa ulimwezesha mtafiti kuziandika maana zote zilizotolewa na watoto kama maana za ziada za maneno hayo.

Vilevile mhimili huu uliweka wazi upungufu wa nadharia hii kwa kuwa iwapo kila mwanalugha ana uhuru wa kujenga dhana kuhusu neno fulani kadiri ya ukomo wa fikra zake, maana za maneno zitakuwa na utata mkubwa. Hivyo basi nadharia hii pekee haikuwa toshelevu kuchunguza mabadiliko ya maana. Pia nadharia ya dhana haiwezi kuelezea maneno mawili kuwa ni visawe kwa kuwa imedai kila neno huwa na dhana moja tu. Kwa mfano kitenzi *ya* (la) kinaweza kuleta dhana kadhaa:

a) Kutia kitu kinywani na kukimeza

b) Kushinda au kupata au kutunukiwa zawadi

c) Kikiambatanishwa na nomino *ĩvu* (tumbo) tutapata kitenzi *ya ivu* ambacho kina maana ya *himili* au *pata mimba.*

Kutokana na udhaifu huo nadharia ya Nyanja za Kisemantiki (Trier, 1934) ilitumiwa ili kuangazia maneno yenye mahusiano kama vile ya usawe, usinonimia, upolisemia na

kufidia upungufu uliopo. Nadharia ya Nyanja (Trier, 1934) iliendelezwa na Firth mwaka1951(Mikael Brunila na Jack LaViolette, 2022).

Kwa mujibu wa Lyons (1999) na Chapman na Routledge (2005), Firth anasema kwamba sifa za neno hutokana na washirika wa neno hilo. Firth (1951) anajulikana kwa usemi wake *you shall know a word by the company it keeps* (Chapman & Routledge, 2005). Yaani, neno hujulikana kutokana na washirika wa neno hilo au maneno yanayolizingira neno husika. Mhimili huu ulisaidia kutambua maneno ambayo yalipata maana kutokana na maneno mengine yaliyopatikana katika mazingira sawa ya kijamii. Nomino *ũkũngi* iliyokuwa na maana ya 'upepo wenye kasi ya wastani' ilipata maana mpya 'makapi' kwa kuwa upepo huo daima hupeperusha makapi. Kutokana na ushirikiano wa nomino hizi mbili, watoto walizihusisha maana pia.

Lugha haijaundwa kwa leksia zinazojisimamia kimaana bali kwa mafungu ya leksia yanayohusiana kimaana kwa mujibu wa nyanja. Kupitia mfumo huu, baadhi ya maneno huunda nyanja za maana chini ya dhana moja ya jumla. Kwa mfano:

a) Mnyama- Ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na ngamia

b) Dini- Kikristo, Kiislamu, Kiyahudi na Kihindu

c) Vitabu vya dini ya Kikristo- Biblia Takatifu, *Sifuni Bwana* na *Misale*.

Katika mfano wa kwanza hapo juu nomino *mnyama* ina maana ya jumla ilhali *ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na ngamia* ni maana mahususi.

Mhimili huu ulitusaidia kupata maana mpya ambazo ziliibuka kutokana na dhana ileile iliyokuwapo katika karne ya ishirini (20) au dhana ambazo ziliibuka kutokana na neno moja katika kipindi cha utafiti, kuanzia mwishoni mwa karne ya 20 hadi karne hii ya 21.

Mhimili mwingine unasema kuwa kila nyanja ina msamiati wake kwa mfano nyanja ya dini, sanaa na elimu. Kwa mfano:

a) *Malondu* (Kondoo)- Katika nyanja ya ufugaji, *malondu* ni wanyama watulivu wanaofugwa ambao hupenda kumfuata mchungaji kila aendapo. Katika dini, neno hili lina maana ya waumini walio chini ya mchungaji mmoja.
b) *Mũĩthi* (Mchungaji)- Katika nyanja ya ufugaji ni mtu anayepeleka mifugo malishoni na kidini ni msimamizi wa kanisa na waumini wake.
c) *Kũĩea* (kuvua)- Maana yake ni kutoa samaki baharini katika nyanja ya uvuvi lakini katika nyanja ya dini ni kuwarudisha watu kwenye njia ya imani/ kanisani.
d) *Kũvanda mbeũ* (kupanda mbegu)- Matika nyanja ya kilimo ni kutia mbegu ardhini ili ziote ilhali katika dini ni kutoa zaka au sadaka na kutoa sala kwa Mungu ili kupata matakwa fulani kwa Mungu.

Mhimili huu ulikuwa faafu katika utafiti wetu kwa kuwa maneno yote yaliyochunguzwa yalihusu dini. Aidha, maneno yaliweza kuwekwa katika makundi kulingana na mahusiano mengineyo.

Upanuzi wa fahiwa ya neno moja husababisha kubanwa kwa maana za maneno yanayolizingira neno hilo. Iwapo neno moja litapitia mabadiliko ya kisemantiki, basi muundo mzima wa nyanja leksika utabadilika. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza maneno yaliyobanwa na yaliyopanuka kimaana katika Biblia zilizotumiwa katika nyanja ya dini.

Maana za maneno hueleweka kwa urahisi yanapoelezwa kwa kuzingatia mahusiano ya kifahiwa kama vile sinonimia, polisemia na antonimia. Mhimili huu ulisaidia katika kueleza maana za maneno na mahusiano ya kifahiwa yaliyodhihirika baina ya maneno yaliyoteuliwa kutoka Biblia ya zamani Mbivilia na maneno mbadala yaliyoteuliwa

kutoka Biblia ya kisasa. Hata hivyo utafiti huu haukujikita katika ufafanuzi wa mahusiano ya kifahiwa, mahusiano hayo yalitajwa tu wakati wa kufafanua maana ya maneno.

Mfumo mzima wa vikoa leksika hubadilika na hatimaye kuathiri mahusiano ya maneno na lugha kwa jumla. Mhimili huu ulituongoza kuchunguza na kueleza mabadiliko ya nomino na vitenzi, na jinsi mabadiliko hayo yameathiri lugha ya Kikamba. Kwa jumla nadharia hii ilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa ilirahisisha uchanganuzi wa maneno kama dhana ya akilini. Aidha, nadharia hii ilikuwa faafu katika shughuli za utunzi wa lekisimu kwa kuwa visawe vya msamiati wa zamani vilionyeshwa na pia maana za maneno yaliyokuwa na upolisemia zikabainishwa.

Hata hivyo, nadharia hii ina upungufu wake. Baadhi ya vikoa ni changamani, vinawakilisha dhana zaidi ya moja na huleta utata wakati wa uainishaji. Kwa mfano neno *ndege* 'chombo cha usafiri' na *ndege* 'nyuni'. Iwapo muktadha wa mazungumzo haujawekwa wazi, patakuwa na utata wa kuelewa kinachomaanishwa. Nadharia ya dhana ilisaidia kufidia upungufu huu kwa kuwa maana ya maneno iliangaliwa kama dhana inayojengeka akilini mwa wanajamii husika.

# SURA YA PILI

## YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Imeonyesha mchango wa wataalamu na watafiti mbalimbali kuhusu mada ya utafiti huku ikibainisha tofauti iliyoko kati ya kazi hizo na utafiti wetu. Aidha, imebainisha mchango wa ugunduzi wao kwa utafiti huu. Upekuzi wa yaliyoandikwa umepangwa katika makundi manne kulingana na malengo ya utafiti. Malengo ya kwanza miwili yameunganishwa kwa kuwa yanahusu kuyaorodhesha maneno yaliyobadilika maana na kuambatanisha na maana kama zinavyojitokeza kutokana na mahojiano:

i. Maana na mabadiliko ya maana katika baadhi ya nomino na vitenzi
ii. Michakato ya mabadiliko ya maana
iii. Sababu za mabadiliko ya maana

### 2.1 Maana na Mabadiliko ya Maana

Neno *maana* lina fahiwa mbalimbali na watu hulitumia kumaanisha vitu mbalimbali (Habwe & Karanja, 2007). Dhana hii ni ya kidhahania kwa kuwa haina muundo thabiti kama vile viambajengo vingine vya lugha vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Maana katika kiwango cha neno huru huitwa maana kileksia. Maana hii hurejelea maana ya msamiati wa lugha kama inavyowakilishwa katika kamusi. Hii ndiyo maana ya msingi. Maana nyingine ni ya kisarufi ambayo hujitokeza katika muktadha wa matumizi katika sentensi. Maana ya kisarufi huzalishwa na maana ya kimsingi. Kunazo maana nyinginezo za ziada kama vile maana husishi, maana elekezi na maana

umaanisho. Utafiti wetu ulijikita katika maana ya kileksia ingawa maana nyinginezo zilikuwa za maana pale ambapo maana za ziada zilijitokeza.

Maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi yake (Lyons, 1981). Maana inayoibuliwa na neno au kauli, hutokana na uwezo wake wa kutumika katika mawasiliano. Hivi ni kusema kwamba kauli moja inaweza kutumiwa katika nyanja tofauti za mawasiliano. Pia inamaanisha kwamba neno linaweza kutamkwa na likakosa kuibua maana yoyote kwa wasikilizaji au likaibua maana isiyokusudiwa na msemaji. Maelezo ya Lyons yalituwezesha kuchunguza maneno ambayo hayakuibua maana yoyote baada ya kutamkwa kwa wahojiwa hasa watoto. Kutoibua maana yoyote kulimaanisha kwamba maneno hayo hayakutumika tena katika mawasiliano miongoni mwa kundi lengwa.

Wittgenstein (2009) anaunga mkono maoni ya Lyons kwa kusema kuwa kila neno au sentensi humaanisha kazi inayotenda katika mazungumzo. Anaitazama lugha kama kifaa kinachotekeleza majukumu mbalimbali na kinachobadilika kulingana na mahitaji ya watumizi wake. Wakati mwingine kifaa huweza kutumiwa kwa kazi tofauti kwa mfano shoka la kuchanjia kuni likatumiwa kukatia nyama. Maana ya msamiati huweza kubadilika kulingana na matumizi tofauti. Maelezo haya yalitusaidia kuchunguza maneno ambayo yamepata matumizi tofauti na awali.

Taylor (1999) akizungumzia maana za nomino *information* katika lugha ya Kiingereza katika jarida lake *Cognitive Semantics* anaeleza kwamba hali ya nomino si tuama. Nomino hiyo inaweza kupata hali tofauti ikitumiwa katika nyanja tofauti kwa mujibu wa mantiki katika lugha husika. Utafiti wa Taylor ulihusu nomino za Kiingereza lakini ulikuwa faafu sana katika uchunguzi wa mabadiliko ya maana katika lugha ya Kikamba.

Abuga (2013) alichunguza "Mabadiliko ya lugha ya Ekegusii" na akagundua kuwa kipengele cha kileksia cha lugha hiyo kilibadilika huku kile cha kimofolojia kikibakia vile vile. Aligundua kuwa mwachano wa wakati baina ya watumia lugha ulizua lahaja mpya ya lugha ya Ekegusii. Utafiti ulibaini baadhi ya mambo yanayoshinikiza mabadiliko ya lugha mathalani elimu, ujozi lugha, wingi lugha, ubadilishaji msimbo miongoni mwa mengine. Ugunduzi huu ulisaidia katika lengo la tatu la utafiti wetu ambalo ni kubaini sababu za mabadiliko. Aidha, kipengele cha mabadiliko ya maneno kidayakronia kinajitokeza, ambacho ndicho kiini cha utafiti wetu. Utafiti wa Abuga ni tofauti kwa kuwa amechunguza maneno mkopo pekee na nadharia zilizotumiwa ni ile ya Usawe na ya Taathira za jamii. Vile vile alichunguza Ekegusii na mimi nilichunguza Kikamba.

Martines n.w (2015) katika jarida la *Semantic Change* alichunguza mabadiliko ya maana katika vitenzi vya Kiingereza. Anasema kwamba kila neno lina maana ambazo ni za kawaida zilizo katika lugha rasmi iliyoandikwa, lakini pia tunaweza kupata maana nyingine katika miktadha isiyo rasmi katika mazungumzo. Aidha, neno hilo likitumiwa katika maeneo au nyanja tofauti linaweza kupata maana nyingine tofauti. Utafiti huu ulichunguza vitenzi pekee katika lugha ya Kiingereza. Ulisaidia sana katika kuchunguza maana nyingine za nomino na vitenzi teule zinazojitokeza katika lugha ya Kikamba katika nyanja ya dini.

Prakasam na Abbi (2018) wakimnukuu Firth (1957) wanasema kuwa maana ya neno ni matumizi yake katika muktadha. Hatufai kuuliza neno lina maana gani bali maana tunaipata kutokana na matumizi yake katika muktadha maalum. Kuna muktadha wa kijamii, kiisimu na usemi. Kwa mfano neno *kiti* katika muktadha wa jamii ya Waswahili ni kifaa cha kukalia bali katika muktadha wa jamii ya Wakamba neno hilo lina maana

ya sehemu ya uzazi ya mwanamke. Maneno yaliyoteuliwa yalichunguzwa katika miktadha mbalimbali kama vile katika usemi, katika muktadha wa B1 na B2 ili kubaini mabadiliko ya maana yalivyotokea.

Nordquist (2019) anasema kwamba mabadiliko ya kisemantiki hayamaanishi kubadilika kwa maana ya neno kama tunavyofikiria, bali ni kuongezwa kwa maana katika mfumo wa kisemantiki au kutoweka kwa maana katika mfumo huu huku umbo likibakia vivyo hivyo. Katika Semantiki na isimu historia, mabadiliko ya kisemantiki ni mabadiliko yoyote ya maana ya neno kwa mujibu wa mapisi ya wakati (Norquist, 2019). Pia huitwa kuhamishwa kwa maana, mabadiliko ya kileksia au maendeleo ya kisemantiki. Lugha ya binadamu hubadilika kila mara kutokana na mabadiliko ya dunia na hitaji la njia rahisi za kujieleza na kuwasiliana. Mabadiliko ya kisemantiki yanaweza pia kutokea wakati wazungumzaji asilia wa lugha huchukua misemo kutoka lugha nyingine na kuitumia katika mazingira yao kwa mawasiliano. Hata hivyo mabadiliko hayatokei kwa wakati mmoja. Kipengee kipya kinapoingizwa katika lugha kinaweza kuchukua muda kuwa sehemu ya msamiati wa lugha hiyo.

## 2.2 Michakato ya Mabadiliko ya Maana

Anttila (1989) akizungumza kuhusu uimarikaji wa maana anasema kwamba maana ya neno ambayo ni hasi inaweza kubadilika na kuwa chanya baada ya kipindi kirefu pale ambapo msamiati unakoma kuwa lugha mwiko na kufanywa lugha ya mazungumzo ya kawaida katika jamii. Kwa mfano, katika Kiingereza cha zamani (Old English), kivumishi *nice* kilimaanisha *foolish* au mjinga. Katika Kiingereza cha sasa, kivumishi hiki kinarejelea dhana *-zuri*. Maelezo haya yalitusaidia kuchunguza iwapo baadhi ya msamiati katika lugha ya Kikamba umepata mabadiliko ya aina hii.

Nabhany (1982) anasema kwamba baadhi ya maneno katika lugha yanaweza kuhamisha maana (Kresse, 2002). Uhamishaji wa maana ni mchakato ambapo maana ya neno huhawilishwa kwa neno jingine ambalo tayari linatumiwa katika lugha, kisha neno lililohamisha maana hutoweka. Dhana ya zamani hubaki katika jamii huku ikiwakilishwa na umbo jingine tofauti. Umbo hili linaweza kuwa limekopwa kutoka lugha nyingine, likawa limeundwa na wanajamii au likachukuliwa kutoka msamiati ambao tayari unatumika. Kwa mfano, zifuatazo ni leksia katika lugha ya Kiswahili zilizotoweka na dhana zikahawilishwa kwa maneo mengine:

| Kikale | Kisasa |
|---|---|
| Gongwa | Ikulu |
| Ng'andu | Dhahabu (Nabhany,1982) |

Kuna michakato minne ya mabadiliko ya maana: upanuzi, ubanaji, usambaratikaji na uimarikaji wa maana (Palmer, 1996). Maana ya neno hupanuka linapotumiwa katika nyanja tofauti likapata maana ya jumla. Upanuzi wa maana ni mchakato ambapo maana za neno huongezeka (Crowley & Bowern, 2010). Aidha, neno linapopanuka maana husemekana limepata maana ya jumla; kwa hivyo linawasilisha dhana mbalimbali au linatumika katika miktadha mipana zaidi. Kwa mfano nomino ya Kiingereza *dog* ilikuwa na maana bayana, 'mbwa wa aina maalum mwenye nguvu nyingi'. Hatimaye maana ya nomino hiyo ilipanuka, ikaanza kurejelea mbwa wa aina yoyote. Maana asilia ya nomino *tingatinga* ni kifaa maalumu kinachotumika kuchimba ardhi na kuchota udongo aghalabu wakati wa kutengeneza barabara (Rajab, 2017). Katika muktadha wa siasa ni 'kiongozi mwenye nguvu kiutendaji'.

Ubanaji wa maana ni hali ambapo maneno hupoteza maana zake za jumla na kurejelea maana zilizo bayana zaidi kuliko zamani (Campbell,2004). Neno ambalo awali

liliwakilisha dhana pana hudondosha baadhi ya dhana kuwakilisha dhana finyu au moja. Kwa mfano kitenzi cha Kiingereza *starve* kilichotokana na Kiingereza cha zamani (Old English) *steorfan* kilimaanisha *to die* au kufa kutokana na sababu yoyote kama vile uzee, ugonjwa au njaa. Hatimaye maana ilibanwa ikawa *die of hunger* (kufa kwa njaa pekee). Maelezo haya yalitoa mwangaza kuhusu michakato mbalimbali ya mabadiliko ya maana katika lugha iliyotafitiwa ya Kikamba.

Panapo mabadiliko ya lugha mabadiliko ya kileksia ni jambo la kutarajiwa sawia na yale ya kifonetiki (Yule n.w, 2000). Hivyo basi wataalamu hawa wanasema kuwa kuna mabadiliko ya kianalojia, ubunifu wa maneno mapya, upanuzi, udondoshaji wa maana na utowekaji wa maana. Haya ni baadhi ya mabadiliko yatakayochunguzwa katika utafiti wetu.

Crystal (2003) anaeleza kuwa usambaratikaji wa maana unatokea pale ambapo msamiati hubadilika na kuanza kuhusishwa na masuala duni hivyo kupunguza ukubalikaji wake katika mazungumzo. Maana ya neno ambayo ilikuwa chanya hubadilika na kuwa hasi. Kwa mfano nomino *toilet* ilimaanisha ‘kitambaa cha kufunika meza’. Baadaye ikaanza kutumiwa badala ya nomino ya Kiingereza *lavatory* yenye maana ‘mahali pa kujisaidia au choo’. Mabadiliko haya yalisababishwa na uwepo wa miiko kama vile kutotaja sehemu za kufanya haja, kwa hivyo neno *toilet* likatumiwa kitasfida. Hatimaye nomino *toilet* ilisambaratika maana. Maelezo haya yanaenda sambamba na malengo ya utafiti wetu ambayo ni kuchunguza jinsi maneno katika lugha ya Kikamba yalivyobadilika maana.

Abuga (2013) anasema kwamba utowekaji wa maana hutokea pale ambapo matumizi ya neno fulani husitishwa kabisa. Dhana iliyokuwa ikiwakilishwa hutoweka au kubadilika na kulifanya neno kuwa halifai tena au maumbo mapya yakaingia katika

jamii yakaziwakilisha dhana za awali. Maumbo haya yanaweza kuwa yamekopwa kutoka lugha nyingine au yakawa yameundwa na wanajamii. Kwa mfano katika lugha ya Ekegusii, neno *esoreti* limekopwa kutoka lugha ya Kinandi kuwakilisha maana ‘kibuyu’. Nomino asilia ya Ekegusii iliyotumiwa ni *ekerandi*. Nomino hii haitumiwi tena, mahali pake pamechukuliwa na nomino mkopo *esoreti*.

Rajab (2017) alichunguza “Mabadiliko ya maana ya msamiati wa Kiswahili katika muktadha wa kisiasa”. Uchunguzi wake uliweka wazi kuwa wanasiasa hutumia msamiati tofauti katika hotuba kwa minajili ya kufikisha ujumbe na kuwasiliana na wafuasi wao. Msamiati watumiao hutolewa katika miktadha mingine na hivyo basi husababisha kupanuka, kufinyika, usogezi, uimarikaji na udhalilikaji wa maana. Kwa mfano maana ya asili ya nomino ‘tingatinga’ ni kifaa maalumu kinachotumika kuchimba ardhi na kuchota udongo aghalabu wakati wa kutengeneza barabara. Maana ya ziada iliyopatikana katika muktadha wa siasa ni ‘kiongozi mwenye nguvu kiutendaji’. Nomino ‘tingatinga’ ilipanuka maana. Aidha, kitenzi ‘chemka’ hurejelea dhana mbili; kufanya kitu cha majimaji kutokota, na kukasirika. Maana iliyoibuka katika muktadha wa kisiasa ni kufeli. Uchunguzi huu ulishughulikia lugha ya Kiswahili bali si Kikamba. Maneno yaliyochunguzwa yalihusu muktadha wa kisiasa, na yaliteuliwa kutoka hotuba za kisiasa, tofauti na uchunguzi wetu ambao ulichunguza maneno kutoka Biblia ya Kikamba inayoitwa *Mbivilia* (1974) na Biblia nyingine ya Kikamba cha siku hizi ijulikanayo kama *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ*. Hata hivyo ulikuwa na manufaa kwetu kwa kuwa ulichunguza mabadiliko ya maana ya msamiati kama tulivyochunguza na ukabainisha baadhi ya michakato ya mabadiliko ya maneno.

Lugha imekuwa ikipitia mageuzi tangu ilipoanza kutumika. Sehemu iliyo muhimu zaidi ya mageuzi ya lugha ni mabadiliko ya kisemantiki au mabadiliko ya maana za maneno. Kuna michakato kadhaa ambayo imechangia mabadiliko ya kisemantiki ingawa baadhi ya michakato ina athari kubwa zaidi kuliko mingine (McWhorter, 2020). Michakato hiyo ya kisemantiki ni kama vile usogezi, ubanaji, upanuzi, utowekaji, usambaratikaji na uimarikaji wa maana. Maelezo ya McWhorter yalisaidia sana utafiti wetu kwa maana yalibainisha baadhi ya michakato ya kisemantiki ambayo inaweza kuchochea mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha.

Gichuru (2020) alitathmini "Mabadiliko ya maana za leksia za Kiswahili kwa mtazamo linganishi wa kikale na kisasa". Ugunduzi wake ni kuwa mbinu zalishi zaidi katika mabadiliko ya maana ni upanuzi wa maana. Alieleza kwamba tasfida ni mchakato wa mabadiliko ya maana unaorejelea matumizi ya lugha ya heshima badala ya kutumia moja kwa moja lugha ya matusi au yenye kukera ili kuficha ukali wa maneno na kufunika aibu. Lugha hutumiwa kutegemea miiko na tamaduni za jamii husika. Kwa mfano awali nomino *ngono* ilirejelea usingizi (kugona- kulala). Kisha ilianza kutumiwa badala ya kutaja moja kwa moja neno 'kujamiiana'. Ikawa watu wanasema 'kugona'. Sasa hivi nomino hii ikitajwa haiibui maana kulala usingizi bali hurejelea tendo la ndoa. Aidha, matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa maendeleo ya jamii katika nyanja mbalimbali ndicho chanzo kikuu cha mabadiliko ya maana ya leksia.

Utafiti wa Gichuru utatufaa kwa kuwa uliweka wazi aina za mabadiliko ya lugha na sababu za mabadiliko hayo. Hata hivyo, utafiti huu haukuchunguza lugha ya Kikamba bali ulishughulikia lugha ya Kiswahili.

## 2.3 Sababu za Mabadiliko ya Maana

Ullman (1972) anasema kwamba maana za maneno zinaweza kubadilika kutokana na uzalishaji wa maana potovu. Daima lugha hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Watoto hujifunza lugha katika jamii. Wanapokua wanaweza kuelewa maana za maneno vinginevyo. Wakikosa kurekebishwa patatokea mabadiliko ya kisemantiki katika kizazi kipya. Wao pia wanaweza kuwapokeza wana wao maana zenye makosa. Kwa mfano vijana wengi wa karne hii wanapozungumza Kiswahili aghalabu hutumia kivumishi –enye visivyo. Mfano katika sentensi, *'Nitakuonyesha vyenye utaandika'. Sentensi hii ina makosa ya kisarufi na haina mantiki. Msemaji anafaa kusema, "Nitakuonyesha jinsi utakavyoandika". Makosa kama haya yasiporekebishwa yanaweza kupokezwa kwa kizazi kipya na kubadilisha lugha. Utafiti wetu ulichunguza mabadiliko ya maana kuanzia mwishoni mwa karne ya ishirini (20) hadi karne ya ishirini na moja (21). Hiki ni kipindi kirefu ambapo vizazi vilipokezwa lugha ya Kikamba, kwa hivyo palikuwa uwezekano wa makosa katika kurithisha maana za baadhi ya maneno. Jambo hilo liliangaliwa.

Hali ya kiasili ya maneno huwa wazi na hakuna mipaka kuhusu maana za maneno (Ullman, 1972). Hali hii ya uwazi wa maana husababisha maana za maneno kutokuwa dhabiti, kwa hivyo hubadilika badilika. Kwa mfano hakuna mpaka wazi baina ya nomino 'mchele' na haiponimu zake 'wali' na 'mpunga'. Mara nyingi watu husema tutakula mchele akimaanisha tutakula 'wali'. Mwengine atasema anaenda kununua mpunga akimaanisha 'mchele'. Wengine huchagua kutumia haiponimu moja tu kuashiria dhana hizo zote. Jambo hili husababisha mabadiliko ya maana. Maelezo ya Ullman yalitufaa kwa kuwa tulichunguza iwapo data ya utafiti wetu ilikuwa na sifa ya uwazi.

Kupotea kwa motisha wa matumizi ya maana mojawapo ya neno, husababisha mabadiliko ya maana (Anusu, 2015). Maneno yanapoegemezwa kwenye fahiwa zake huwa ni mbinu moja ya kudhibiti maana kwa kiwango fulani, lakini maana moja ya neno ikitumiwa zaidi kuliko maana nyinginezo za neno hilo, maana zisizotumiwa zitakufa (Campbell, 2004). Kwa mfano, katika kipindi fulani, neno *gay* lilikuwa na maana mbili; *joyful* na *homosexual*. Maana hizi mbili zilitumika pamoja hadi pale taratibu wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza walianza kuegemea kwenye maana *homosexual* kiasi kwamba maana nyingineyo ilikufa. Nomino 'shoga' katika lugha ya Kiswahili pia ilikuwa na maana mbili; 'rafiki wa kike wa mwanamke' na 'mwanamume anayefanya mapenzi na mwanamume mwingine'. Maana hii ya pili imetumiwa sana katika jamii kiasi kwamba maana ya kwanza inaelekea kupotea. Utafiti wa Anusu ulitusaidia kutambua maneno yaliyopoteza mojawapo ya maana zake kutokana na wazungumzaji kuegemea maana moja.

Leksia za lugha zina sifa ya upolisemia. Polisemia ni neno lenye maana mbili au zaidi zinazokaribiana sana (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2013). Kwa mfano 'kupe' kwa maana ya mdudu na 'kupe' kwa maana ya mtu anayeishi kwa kutegemea wengine. Maneno yana uwezo wa kupata maana mpya bila kupoteza maana yake asilia (Fromkin na wenzake, 2014). Kutokana na sifa hii ya lugha, maneno hubadilika maana kulingana na jinsi yanavyotumiwa. Kwa mfano kitenzi cha Kikamba *ya* kinaweza kuwa na maana nyingi. Mtu anaposema, 'Ninaya milioni!' ni vigumu kubaini maana ya kauli hii. Anaweza kumaanisha ametumia shilingi milioni zikaisha, ameshinda shilingi milioni au ametafuna milioni. Maana asilia ya kitenzi *ya* imehawilishwa hadi kwenye vitendo vingine visivyohusiana na kutia kitu kinywani na kumeza. Maelezo ya Fromkin yalitusaidia kwa kuwa tuligundua kuwa sifa hii ya upolisemia ilichangia sana katika mabadiliko ya maana ya maneno katika utafiti wetu.

Ullman (1972) anasema kwamba mabadiliko ya maana yanaweza kutokea iwapo neno litatumiwa katika muktadha tata. Muktadha ni sehemu ya ulimwengu halisi ambamo matukio yamejikita (Charles, 2000). Aidha, muktadha ni maneno yaliyo nyuma au mbele ya neno fulani katika sentensi. Iwapo maneno yaliyo nyuma au mbele ya neno fulani hayatoi maelezo kikamilifu kuhusu neno hilo, basi huenda lisieleweke kama ilivyokusudiwa. Iwapo kile anachomaanisha msemaji wa kauli fulani sivyo kinavyofasiriwa na msikilizaji, mabadiliko ya maana yatatokea. Kwa mfano neno ‘tia’ linaweza kutumiwa kuleta maana kadhaa:

i) Nimeenda kwa mwalimu <u>nikamtia</u> akaniruhusu kwenda nyumbani.

ii) Vijana wa Makueni <u>tuliwatia</u>…hawakuamini.

iii) Alijifanya mwerevu sana, askari <u>walimtia</u> akasema ukweli.

Miktadha ambamo kitenzi ‘tia’ kimetumiwa ina utata. Kutokana na miktadha hii tata ni rahisi kubadilisha maana iliyokusudiwa na msemaji. Katika sentensi (i) maana ya ‘tia’ inaweza kuwa ‘nikamdanganya’, ‘nikampiga’ au ‘nikamhonga’. Kila sentensi itafasiriwa kuleta maana mbalimbali kwa mujibu wa msomaji. Jambo hili husababisha mabadiliko ya maana. Maelezo ya Ullman yalituwezesha kuchunguza maana za data ya utafiti wetu katika muktadha wa B1, B2 na katika mazungumzo ya wazee na watoto, ili kuona jinsi maana ilivyobadilika katika miktadha hiyo.

Tsunoda (2006) anasema kwamba kupotea kwa majina ya ukoo kunahusishwa na utengano na misukosuko miongoni mwa jamii lugha pamoja na mtagusano wa lugha mbalimbali. Jambo hili husababisha wazungumzaji wa lugha kurahisisha baadhi ya istilahi ili kueleweka upesi na wasikilizaji walio karibu. Kwa mfano katika jamii ya Wakamba msamiati huu wa ukoo unazidi kupotea miongoni mwa kizazi cha karne hii ya ishirini na moja (21). Majina kama vile *mwenduu*, *wasa*, *ũkũlũ* na *nau* ambayo ni ya

ukoo hayatumiwi na kizazi cha karne hii. Badala yake hutumia vitohozi *andi, angoo, kasini, ndati* na kadhalika (Muthoka, 2017). Utafiti wa Tsunoda ulihusu majina ya ukoo nao utafiti wetu ulihusu majina pia, ambayo ni nomino na vitenzi. Sababu zilizozungumziwa hapa pia tulizichunguza iwapo ziliathiri data ya utafiti wetu.

Palmer (1996) anasema kwamba mabadiliko ya maana husababishwa na mambo manne. Mambo hayo ni uhitaji wa maana mpya, kuwapo kwa maneno mwiko katika jamii, uibukaji wa dhana za kisayansi na wakati mwingine mabadiliko hutokea kwa bahati. Maana ya neno hubadilika wakati neno hilo linahitaji maana mpya. Uhitaji huu husababishwa na kuwepo kwa dhana mpya ambazo zinahitaji majina. Kwa mfano, kifaa cha kielektroniki kinachounganishwa na kompyuta ili kuwezesha kufungua programu au kuandika kwenye kiwambo huitwa *kipanya*. Neno 'panya' (udogo wake ni kipanya) limekuwapo tangu zamani likirejelea mnyama mdogo anayependa kula nafaka. Kutokana na uibukaji wa dhana mpya, nomino 'panya' ilipata maana ya ziada. Maoni ya Palmer yalikuwa faafu katika utafiti wetu kwa kuwa tulipata baadhi ya sababu za mabadiliko ya maana za maneno.

Aidha, Palmer (1996) anasema kwamba maana ya neno hubadilika iwapo neno hilo litatumiwa kama neno mwiko. Iwapo neno jingine litachukua nafasi ya neno mwiko, basi litaongezewa maana. Kwa mfano, neno la Kiingereza *restroom* halimaanishi mahali pa kupumzika, bali linatumiwa kitasfida kurejelea dhana *place to defacate or wash and arrange your hair* (Oxford Learners' Dictionary, 2002). Katika Kiswahili ni mahali pa kunyia au kukogea na kuchania nywele. Kutokana na mawazo haya tulichunguza maneno ambayo yalibadilika maana kutokana na kufanywa kuwa mwiko au kutwikwa maana ya nomino iliyo mwiko katika jamii ya Wakamba.

Vile vile, maana za maneno hubadilika iwapo maneno hayo yatatumiwa kama msamiati wa kisayansi (Palmer,1996). Msamiati wa kisayansi huchukuliwa kutoka msamiati wa kawaida wa lugha lakini hutumiwa kurejelea vitu tofauti na kirejelewa cha awali. Kwa mfano maana ya nomino *mass* hurejelea 'mkusanyiko wa watu au vitu' (Oxford Learners' Dictionary, 2002). Neno hili katika taaluma ya Fizikia linamaanisha wingi wa nyenzo zilizomo ndani ya kitu. Aidha, maana ya kitenzi *pakua* ni kutoa chakula kwenye chombo cha kupikia na kutoa mizigo kutoka kwenye chombo cha kusafiria. Neno hili sasa limepata maana mpya ya kisayansi. Tukisema 'pakua data' katika Kiingereza ni *download data*. Maoni ya Palmer yalituwezesha kuchunguza iwapo baadhi ya maneno katika data ya utafiti wetu yalitumiwa kama msamiati wa kisayansi.

Kwa mujibu wa Blank (1999) upanuzi wa maana husababishwa na ukuruba wa maana. Dhana mbili tofauti zinapokaribiana kimaana zinaweza kusababisha mabadiliko ya maana. Kwa mfano nomino 'ndege' awali ilitumiwa kurejelea 'kiumbe mwenye mabawa anayepaa angani'. Baadaye chombo cha usafiri chenye mabawa na kinachopaa angani kikapewa jina ndege (Gichuru, 2020). Nomino ndege ikapanuka maana. Neno *kũkindana* katika Kikamba awali lilirejelea kusukumana na kuangushana kwa kupimana nguvu katika mchezo wa miereka. Dhana ya kuangushana katika miereka inakaribiana na dhana ya kuangushana katika tendo la ngono. Kutaja masuala ya ngono ni mwiko katika jamii ya Wakamba kwa hivyo badala ya kutaja tendo la ngono wazungumzaji wakawa wanatumia neno hili lenye ujirani wa dhana kurejelea ngono. Kwa sasa neno *kũkindana* maana yake ni kushiriki ngono na hii ndiyo maana inayojulikana na kizazi cha karne hii ya 21. Hata hivyo kulitaja kunadhihirisha utovu wa maadili na ndiyo maana halitumiwi na kizazi cha karne ya 21 katika mazungumzo ya kawaida. Wazee wa miaka zaidi ya sabini na tano (75) bado hulitumia bila wasiwasi

kumaanisha kuangushana huku wakizua utata wa kimawasiliano baina yao na wazawa wa karne hii ya ishirini na moja (21).

David (2009) alifanya uchanganuzi wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi yalibainisha kuwa tabia ya kitamaduni ya kutotaja majina ya wakwe na mashemeji, mtagusano wa jamii na majirani na mitazamo ya jamii kuhusu maneno fulani ni baadhi ya mambo yaliyosababisha utohozi na ubadilikaji wa maneno. Utafiti huu ulitusaidia sana kwa kuwa ulibainisha baadhi ya sababu za kutokea kwa mabadiliko ya maana katika lugha. Hata hivyo ni maneno mkopo pekee yaliyochunguzwa.

Muthoka (2017) alitathmini "Kikamba Language Shift and Endangerment in an Urban Upmarket". Aligundua kwamba pana tofauti katika ruwaza za kuchagua lugha baina ya watu wazima na watoto. Wazazi wanapotangamana na watu wengine wazima huzungumza lugha ya Kikamba lakini wanapozungumza na wana wao hutumia ima Kiingereza au Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa tofauti na wetu kwa kuwa ulichunguza mtazamo wa wakazi wa mjini kuhusu lugha ya Kikamba wala haukuchunguza nomino au vitenzi vilivyopitia mabadiliko ya kisemantiki kama tulivyofanya. Utafiti huu ulikuwa na manufaa kwetu kwa kuwa ulibaini kuwa Wakamba waliokomaa wana umilisi katika lugha yao kuliko wale wachanga. Ugunduzi huu ulituelekeza kuwateua wazee wa miaka sabini na mitano (75) na zaidi kuelekeza utafiti wetu kuhusu Kikamba cha kale, maana asilia za maneno hayo, maneno yaliyobadilika maana na kuwateua watoto ili tuchunguze kiwango chao cha ufahamu wa lugha ya Kikamba.

Fromkin na wenzake (2014) wanasema kwamba maneno huwa na sifa za kipolisemia au huwa na maana zaidi ya moja kutegemea muktadha. Kila neno lina maana moja ya msingi na maana zingine za ziada. Watumiaji wa lugha wanaweza kuacha maana ya

msingi na kupendelea maana za ziada. Matokeo yake ni kwamba maana ya msingi ya neno hutoweka. Anazidi kusema kuwa watoto wanaweza kupokezwa lugha kutoka kwa walezi kwa njia isiyostahili. Wao huendelea kuitumia lugha ikiwa na maana waliyoipokea. Maana hiyo ndiyo huendelezwa kwa jamii-lugha. Anasisitiza kwamba virejelewa huendelea kubadilika kulingana na mpito wa wakati. Vinapobadilika panazuka uhitaji wa wanajamii kubuni majina ya virejelewa vipya. Maandiko haya yalisaidia sana katika utafiti huu kuelezea sababu za mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha ya Kikamba.

Mwendamseke (2016) alitathmini "Mwelekeo wa maana za kipolisemia katika msamiati wa Kiswahili". Maana zilizoangaziwa ni za kipolisemia pekee bali si za jumla kama ilivyo katika utafiti wetu. Ilibainika kuwa binadamu ana tabia ya kurahisisha lugha na huepuka kuwa na maumbo mengi katika lugha. Hivyo basi kunakuwa na dhana nyingi ambazo huwakilishwa na umbo au neno moja. Utafiti huu ulitufaa katika kuchunguza mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha ya Kikamba kwa kuwa maana za kipolisemia hutokana na michakato ya kisemantiki itakayochunguzwa kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti wetu.

Babusa (2019) alichunguza "Etimolojia na mabadiliko ya maana na utamkaji wa msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili". Aligundua kuwa maneno mengi ya Kiarabu yaliswahilishwa na konsonanti kubadilishwa ili kurahisisha matamshi kwa wazungumzaji wa Kibantu. Kulitokea mabadiliko ya maana katika baadhi ya maneno ya Kiarabu yaliyotiwa katika Kiswahili. Kwa mfano, neno la Kiswahili 'sakafu' lilikopwa kutoka lugha ya Kiarabu (saqfu). Neno la Kiarabu *saqfu* lina maana ya 'dari', yaani sehemu ya juu ya nyumba iliyo chini ya paa. Lakini neno hili lilipokopwa na kuingizwa ndani ya Kiswahili, maana yake ilibadilika na kuwa 'sehemu ya chini ya

nyumba iliyotandazwa na kutiwa saruji'. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa ni dhihirisho kuwa maneno katika lugha yoyote hubadilika maana.

## 2.4 Pengo la Utafiti

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu semantiki. Zipo chache zilizotalii semantiki katika lugha ya Kikamba. Musyimi (2011) alichunguza maana za majina ya watu katika jamii ya Wakamba. Ngina, (2015) alishughulikia uchanganuzi semantiki wa vionyeshi. Muthoka (2017) alitalii "Kikamba language shift and endangerment in an urban upmarket". Hakuna utafiti uliochunguza mabadiliko ya kisemantiki ya nomino na vitenzi katika lugha ya Kikamba kwa mtazamo wa Kidayakronia. Aidha, watoto wengi hawaelewi maana ya msamiati wa kale, jambo linaloashiria pengo la uelewa wa msamiati wa Kikamba katika nyanja za kidini na kijamii. Vile vile, hakuna jitihada za makusudi za kuhifadhi maneno ambayo yanafifia au kutoweka kabisa. Bila juhudi hizo, kizazi kijacho kitapoteza sehemu ya urithi wa lugha. Hivyo basi palikuwa na pengo la kiutafiti ambalo tulikusudia kuliziba. Tulichunguza iwapo nomino na vitenzi vya Kikamba vimebadilika maana ili kujaribu kuhifadhi maana zinazofifia au zilizotoweka. Pia tulichunguza michakato ya kisemantiki inayohusishwa na mabadiliko na sababu za mabadiliko hayo. Matini za utafiti zilikuwa *Mbivilia* (UBS,1974) na *Mbivilia ya Kĩkamba Kya Ivinda Yĩĩ* (IT, 2011).

## 2.5 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia masuala kadhaa kwa nia ya kuupa utafiti msingi wa kisayansi. Masuala yaliyoangaziwa ni maelezo ya wataalamu kuhusu mabadiliko ya lugha, michakato ya mabadiliko ya maana na sababu za mabadiliko hayo. Tasnifu zilizoandikwa kuhusu mabadiliko ya maana katika lugha zilitaliiwa. Aidha, majarida

yaliyofafanua masuala ya mabadiliko ya maana yaliangaziwa. Pengo ambalo halikuzibwa na watafiti waliotangulia lilibainishwa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza jinsi utafiti ulivyofanyika. Inaeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti wetu. Mbinu za utafiti ni jumla ya taratibu zinazotumika wakati wa kufanya utafiti (Kothari, 2004). Mbinu zilizoangaziwa ni eneo la utafiti, sampuli ya utafiti, vifaa vya utafiti, mbinu za kukusanya data, mbinu za kuchanganua na kuwasilisha data pamoja na mifano michache ya uchanganuzi huu na nidhamu katika utafiti.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani na maktabani. Ulifanywa katika kaunti ndogo ya Mwala katika Kaunti ya Machakos. Eneo hili lilichaguliwa kwa kuwa lilikuwa karibu sana na makazi ya mtafiti. Hapo ndipo watafitiwa walipopatikana kwa urahisi na kwa muda mfupi. Aidha, eneo hili ni miongoni mwa maeneo tisa (9) yanayounda kaunti ya Machakos na linaakisi sifa bia za maeneo mengineyo katika kaunti ya Machakos. Kwa hivyo lahaja inayozungumzwa katika eneo hili ni Kimasaku. Data ilipatikana kwa njia ya mahojiano nyanjani na usomaji maktabani. Mtafiti alisoma vitabu, tasnifu, majarida na matini nyinginezo zilizoilenga mada iliyotafitiwa.

## 3.2 Sampuli ya Utafiti

Sampuli ni sehemu ndogo ya jumla ya idadi (Kothari, 2004). Sampuli ya utafiti wetu ilikuwa Biblia ya Kikamba *Mbivilia* (1974) chapa ya UBS na Biblia nyingine ya Kikamba kinachozungumzwa katika karne ya ishirini na moja (21), *Mbivilia ya*

*Kĩkamba kya Ĩvinda Yĩĩ* (IT, 2011). Vitabu vinne (4) vya Biblia viliteuliwa kwa njia ya makusudi: *Mwanzo* na *Zaburi* katika Agano la Kale na *Mathayo* na *Luka* katika Agano Jipya. Mtafiti alikuwa na imani kuwa vitabu hivi ndivyo vingempa data faafu kwa kuwa vilisheheni msamiati wa kale ambao hautumiwi sana katika mazungumzo ya kawaida na huenda haueleweki na kizazi cha karne hii ya ishirini na moja (21). Biblia ya zamani *Mbivilia* (1974) ilisomwa na maneno mia moja (100) kuteuliwa kimakusudi. Haya ni maneno ambayo yalikuwa na utata wa maana kwa mtafiti. Mtafiti alilinganisha Biblia hizi mbili, chapisho la mwaka 1974 na la 2011 kuchunguza iwapo maneno hayo mia moja yalipatikana katika muktadha huo ulioteuliwa. Ilibainika kwamba Biblia ya kisasa ya mwaka 2011 ilitumia maneno tofauti. Maneno hayo tofauti yalikuwa mia moja (100) na yalijumuishwa katika data, idadi jumuia ikawa mia mbili (200). Nomino zilikuwa mia moja kumi na sita (116) na vitenzi themanini na vinne (84).

Mtafiti alitumia mbinu ya asilimia kutambua sampuli ya utafiti kutokana na idadi jumuia ya maneno mia mbili (200). Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli wakilishi inapaswa kuwa na angalau asilimia kumi (10%) ya idadi jumuia. Mugenda & Mugenda (2013) wanasema kwamba sampuli wakilishi ya idadi jumuia inafaa kuwa asilimia kumi (10%) hadi asilimia thelathini (30%). Mtafiti alitumia asilimia ishirini na tano (25%) ili kupata sampuli ya utafiti kama ifuatavyo:

$25/100 \times 200 = 50$

Asilimia ishirini na tano (25%) ya mia mbili (200) ni hamsini (50). Maneno hamsini (50) pekee ndiyo yalihitajika kutafitiwa. Maneno hamsini (50) yaliteuliwa kimakusudi, nomino thelathini (30) na vitenzi ishirini (20). Nomino kumi na tano (15) zilitolewa kwenye Biblia ya zamani *Mbivilia* (1974) na nyingine kumi na tano (15) kwenye Biblia ya kisasa, *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (2011). Kati ya vitenzi ishirini (20),

kumi (10) vilikuwa vya *Mbivilia* (1974) na kumi (10) vya *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* (2011). Maneno hamsini ndiyo yalichunguzwa iwapo kuna maana imebadilika au kupotea.

Kando na kuzichambua matini, wanajamii ishirini (20) waliteuliwa kwa njia ya makusudi na kuhojiwa kuhusu mabadiliko ya kisemantiki ya maneno yaliyoteuliwa. Miongoni mwa watu hawa ishirini (20), watano (5) walikuwa wanaume na watano (5) walikuwa wanawake wote wenye umri wa miaka sabini na mitano (75) na zaidi. Aidha, wengineo ni wavulana watano (5) na wasichana watano (5) wenye umri wa miaka kumi hadi kumi na minne (10-14).

Usampulishaji wa makusudi humwezesha mtafiti kuteua eneo, kitafitiwa au watafitiwa ambao wana habari kuhusu suala la utafiti na kuwasilisha kundi lengwa (Walliman, 2011). Njia ya makusudi ilifaa zaidi kwa kuwa mtafiti alilenga kundi moja la wazawa wa karne ya ishirini (20) na kundi jingine la wazawa wa karne ya ishirini na moja (21) pekee. Wazee wenye umri wa miaka sabini na mitano (75) na zaidi wameishi katika vipindi viwili vya utafiti wetu ambavyo ni karne ya ishirini (20) na ya ishirini na moja (21). Kwa hivyo wana uelewa wa maana ya maneno yaliyotumiwa awali ambayo yamo katika matini lengwa na mabadiliko yoyote ya maana ambayo yametokea. Watoto nao walitumiwa katika utafiti huu kuchunguza iwapo walifahamu maana ya maneno ambayo yaliteuliwa kama data ya utafiti na kudhihirisha hali halisi ya lugha ya Kikamba kama ilivyo katika karne hii ya ishirini na moja (21).

## 3.3 Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulitumia kalamu na daftari ili kunakili msamiati uliobadilika maana kutoka matini ya utafiti iliyosomwa. Rununu ilitumiwa kunasa sauti na kunakili majibu na maoni ya wahojiwa na mchakato mzima wa mahojiano ili kuhakikisha uhifadhi bora

zaidi wa data na urejeleaji panapo haja. Tarakilishi ilitumika kuchapa kazi hii ya utafiti kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mtandao ulitumika kupakua baadhi ya machapisho, tasnifu, majarida na taarifa zilizohusu semantiki.

## 3.4 Mbinu za Kukusanya Data

Data ya utafiti wetu ilikusanywa maktabani na nyanjani kwa kutumia mbinu ya usomaji wa makala na mahojiano. Mtafiti alipitia maandiko yaliyozungumzia mabadiliko ya kisemantiki ya lugha. Aidha, alizisoma matini za utafiti ambazo ni Biblia mbili; Biblia ya zamani, *Mbivilia*, iliyochapishwa mwaka 1974 na Biblia ya kisasa *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ,* iliyochapishwa mwaka 2011. Vitabu vinne (4) vya Biblia viliteuliwa kimakusudi; *Mwanzo* na *Zaburi* katika Agano la Kale na *Mathayo* na *Luka* katika Agano Jipya. Mtafiti alitambua maneno mia mbili (200) ambayo yalihitaji kuchunguzwa. Utambuzi wa maneno haya ulikuwa rahisi kwa maana mtafiti mwenyewe ni Mkamba na anao umilisi wa lugha ya Kikamba.

Mbinu ya asilimia iliyopendekezwa na wataalamu kama vile Kothari (2004) na Mugenda & Mugenda (2013) ilitumiwa kutambua idadi ya data tafitiwa. Mbinu hii hupendekeza sampuli ya utafiti iwe kati ya asilimia kumi (10%) na asilimia thelathini (30%) ya idadi jumuia. Mtafiti alitumia asilimia ishirini na tano (25%) ili kupata sampuli ya utafiti. Asilimia hii ni miongoni mwa asilimia zilizopendekezwa na wataalamu. Kwa kutumia asilimia ishirini na tano (25%) mtafiti aliweza kutambua idadi ya maneno ambayo yangetafitiwa. Maneno hamsini (50) pekee.

Maneno hamsini (50) yaliteuliwa kimakusudi, nomino thelathini (30) na vitenzi ishirini (20). Nomino kumi na tano (15) zilitolewa kwenye B1 na kumi na tano (15) kwenye B2. Vitenzi kumi (10) vilitolewa kwenye B1 na vingine kumi (10) vikatolewa kwenye B2. Kwa kuyatambua na kuyaandika maneno hayo lengo la kwanza la utafiti lilikuwa

limetimizwa. Mtafiti alizuru sehemu lengwa katika eneo la Mwala kijiji cha Makutano na kujitambulisha kwa mzee wa kijiji. Alipokelewa vizuri na kupata msaada katika kuteua wazee kumi (10) wenye umri wa miaka sabini na mitano (75) na zaidi.

Aidha, mtafiti aliizuru shule ya msingi ya Makutano, kaunti ya ndogo ya Mwala, kaunti ya Machakos. Kwa usaidizi wa mwalimu mkuu na walimu, watoto kumi (10) walio kati ya umri wa miaka kumi (10) na kumi na minne (14) waliteuliwa. Watoto hawa waliandikiwa ubaoni maneno ya Kikamba yaliyoteuliwa, nomino thelathini (30) na vitenzi ishirini (20). Kisha waliulizwa wataje maana au visawe. Majibu yao yalinakiliwa katika daftari. Hatimaye mtafiti aliendeleza usaili katika maeneo ya utafiti huku akiuliza maana ya maneno aliyoyateua. Majibu yote aliyanakili katika daftari huku pia akiyarekodi kwa rununu kwa urejeleaji wa baadaye.

## 3.5 Mbinu za Kuchanganua na Kuwasilisha Data

Data zote zilizorekodiwa na kuandikwa zilichunguzwa na kuwekwa katika orodha mbili: nomino na vitenzi. Mtafiti alizipanga nomino katika makundi mawili: nomino zilizoteuliwa kutoka Biblia ya Kikamba chapa ya UBS (1974) na nomino za Biblia ya Kikamba chapa ya IT (2011). Vitenzi navyo vilipangwa hivyo. Michakato ya kisemantiki iliyosababisha mabadiliko ya maana ya maneno ilibainishwa huku maneno yakipangwa vizuri katika jedwali. Aidha, sababu za mabadiliko ya maana zilijadiliwa. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Kwa mfano:

*Manzĩ* (N) katika Kikamba cha kale ilikuwa na maana mbili: maji na shahawa. Katika Kikamba cha sasa neno *kĩw'ũ* linatumika kwa maana ya 'maji' huku neno *manzĩ* likibaki na maana moja ya 'shahawa' lakini katika miktadha finyu. Nomino hii sasa imekuwa mwiko.

*Imisi* (N) inapatikana katika injili ya Mtakatifu Mathayo mlango wa tano (5)) katika Biblia ya zamani. Maana yake katika Injili ni ‘kitambaa kikubwa kilichotumiwa kufunika vitu’. Wasomaji wa karne hii ya ishirini na moja (21) watahusisha maana hii iliyofifia na maana ya neno *kamisi* (vazi la wanawake la kuvaliwa ndani ya nguo) na ambalo ukubwa ni *imisi.* Katika Biblia za kisasa neno *mbisũ* (chungu) limetumiwa badala ya *ĩmisi.*

*Vuta* (T) ni kitenzi ambacho katika Kikamba cha kale kilikuwa na maana tatu:

a) kumnyang’anya mtu mali b) kuachisha mtu kazi c) kuondoa maandishi

Kwa sasa maana zilizobaki ni mbili: a) kuachisha mtu kazi b) kuondoa maandishi. Maana ‘kumnyang’anya mtu mali’ imedondoshwa na kuhamishwa kwa kitenzi *vena*. Matokeo yaliwekwa katika majedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali 3.1: Michakato ya Kisemantiki inayoathiri Nomino na Vitenzi (M.Y)**

| Mananeno | Nomino | Kitenzi |
|---|---|---|
| Mifano | Manzĩ | Vuta |
| Maana asilia | Maji, shahawa | Nyang’anya mtu mali, achisha kazi, ondoa maandishi |
| Maana ya sasa | Shahawa | Achisha kazi, futa maandishi |
| Michakato ya kisemantiki | Usambaratikaji, ubanaji | Ubanaji wa maana |

Jedwali hili linabainisha michakato kadhaa iliyosababisha mabadiliko ya maana ya nomino *manzĩ* na kitenzi *vuta*. Ubanaji wa maana umejitokeza pale nomino *manzĩ* imedondosha maana moja ikabaki na moja. Maana iliyobaki ni hasi kwa maana inahusishwa na sehemu za uzazi ambazo ni mwiko kutaja. Kwa hivyo maana imesambaratika. Kitenzi *vuta* kimedondosha maana moja 'nyang'anya mtu mali'. Mchakato uliohusika ni ubanaji wa maana.

## 3.6 Maadili katika Utafiti

Maadili ya utafiti huhakikisha kuwa hatua zote za utafiti hazina madhara yoyote kwa wanaoshirikishwa katika utafiti wala haziwadunishi kwa vyovyote vile. Mtafiti alipata idhini ya kufanya utafiti kutoka Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI) ambayo ilihakikisha mtafiti amezingatia maadili ipasavyo. Barua ya kuidhinishwa imeambatishwa (kiambatisho VI). Mtafiti alijijulisha kwa watafitiwa na kuwaeleza nia yake. Aliwaeleza kuwa utafiti huo ulikuwa wa kiakademia na data ingekusanywa kwa sababu za kiakademia tu wala si kwa sababu zozote za kimadhehebu. Aliwapa wasailiwa hakikisho la usiri katika usaili. Majina ya wasailiwa hayakunakiliwa popote. Aidha, wasailiwa hawakulazimishwa kutoa maoni yao kuhusu mada ya utafiti.

## 3.7 Hitimisho

Sura hii ilitoa maelezo kuhusu jinsi utafiti ulivyofanyika. Eneo la utafiti lilibainishwa katika sehemu ya kwanza. Sampuli ya utafiti ikashughulikiwa katika sehemu ya pili. Vifaa vya utafiti vilifafanuliwa katika sehemu ya tatu. Aidha, ukusanyaji wa data na mbinu za kuchanganua na kuwasilisha data ziliangaziwa katika sehemu ya nne na ya tano. Sehemu ya sita ilishughulikia maadili katika utafiti na sehemu ya saba ni hitimisho.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

# MABADILIKO YA KISEMANTIKI YA MANENO YA KIKAMBA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa data kuhusu mabadiliko ya kisemantiki ya nomino na vitenzi katika lugha ya Kikamba. Uchanganuzi huo ulifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti ambayo yalimtaka mtafiti kuchunguza: nomino na vitenzi vilivyobadilika maana, mabadiliko ya kisemantiki yaliyotokea kwa baadhi ya nomino na vitenzi katika lugha ya Kikamba, sababu za mabadiliko hayo na michakato ya kisemantiki inayohusishwa na mabadiliko hayo na sababu za mabadiliko ya kisemantiki ya maneno yaliyotajwa katika kipindi kilichoangaziwa na utafiti ambacho ni kuanzia mwishoni mwa karne ya ishirini (20) hadi karne hii ya ishirini na moja (21).

## 4.1 Mabadiliko ya Kisemantiki ya Nomino na Vitenzi

Kama anavyosema Nordquist (2019), mabadiliko ya kisemantiki hayamaanishi kubadilika kwa maana ya neno kama tunavyofikiria, humaanisha pia kuongezwa kwa maana katika mfumo wa kisemantiki au kutoweka kwa maana katika mfumo huu huku umbo likibakia vivyo hivyo. Kwa mujibu wa Yule (2000), kila kizazi kipya hulazimika kuibua jinsi tofauti za kuitumia lugha ya kizazi kilichotangulia ili kukidhi mahitaji yao. Jambo hili husababisha mabadiliko bayana katika lugha. Mabadiliko ya kisemantiki yanaweza kutokea kwa njia nne kuu; kupanuka, kubanwa, usambaratikaji na uimarikaji wa maana (Nordquist,2019). Hata hivyo kuna njia nyinginezo za mabadiliko ya maana ambazo zilijitokeza katika utafiti huu.

Utafiti wetu ulijikita katika uchunguzi wa mabadiliko ya kisemantiki ya nomino na vitenzi katika Biblia mbili: Biblia ya Kikamba *Mbivilia* chapa ya UBS (1974) ambayo tuliiita B1, na Biblia ya Kikamba cha sasa *Mbivilia ya Kĩkamba kya Ivinda Yĩĩ* chapa ya IT (2011) ambayo katika utafiti huu tuliipa jina B2. Biblia hizi zinaweza kuwa na maneno mengi yaliyobadilika maana lakini tulijikita katika maneno hamsini (50) pekee yaliyoteuliwa kutoka idadi jumuia ya maneno mia mbili (200). Sehemu inayofuata inatoa maelezo zaidi kuhusu nomino na kubainisha nomino zilizoteuliwa kama data ya utafiti huu.

### 4.1.1 Kundi la Nomino katika Biblia

Nomino ni neno linalotaja jina la mahali, mtu, kitu, hali au tendo (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Kihore na wenzake (2003) wanasema kwamba nomino ni jina linalotaja kitu, kiumbe hai, dhana au tendo. Kwa mujibu wa kamusi iliyotajwa hapo juu, kuna aina nane za nomino; nomino ambatani, nomino dhahania, nomino mguso, nomino ya pekee, nomino ya jamii, nomino ya wingi, nomino ya kitenzi-jina na nomino ya kawaida. Mtafiti alitumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2016) kueleza aina za nomino ambazo zilitumiwa katika utafiti huu.

### a) Nomino dhahania

Hii ni nomino inayorejelea kitu ambacho hakiwezi kudhihirika kama vile malaika, uzuri na uwongo (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Kikamba kina nomino dhahania kama vile *wanake* (urembo), *ũw'o* (ukweli) na *ũtumanu* (ujinga). Katika utafiti wetu, fahiwa ya nomino *Asa* inayorejelea Mungu ni dhahania.

### b) Nomino mguso

Nomino mguso ni nomino inayotaja kitu kinachoweza kuguswa na kuonekana kama vile ‘kitabu’ (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Katika lugha ya Kikamba nomino hizi ni nyingi kwa mfano *kĩmũtũ*, *mbota*, *mbisũ* na *ikuu* ambazo ni baadhi ya nomino zinazochunguzwa katika utafiti huu.

### c)Nomino ya pekee

Nomino ya pekee hurejelea jina la mtu, mahali, kitu au taasisi na linapoandikwa huanza kwa herufi kubwa (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Kwa mfano *Mwîai* mi mojawapo ya majina ya Mungu.

### d) Nomino ya wingi

Hii ni nomino inayotaja vitu vinavyopatikana katika hali ya wingi tu kama vile maji, maziwa na mate (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Mifano ya nomino za wingi ambazo tulichunguza ni *mata*, *manzĩ* na *kĩw'ũ.*

### e) Nomino ya kitenzi-jina

Nomino hii imeundwa kutokana na kitenzi kwa kuambisha ku- kama vile ‘kuimba’ na ‘kucheza’ (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Katika lugha ya Kikamba nomino hizi zipo. Kwa mfano *kũvanda* (kupanda), *kũkoma* (kulala) na *kũsemba* (kukimbia). Utafiti wetu haukuchunguza nomino hizi ila katika kuchanganua vitenzi tulivyoteua, mara kwa mara tulilazimika kuambisha ku-. Kwa hivyo vitenzi vilivyoambishwa vilibadilika kuwa nomino kitenzi jina. Kwa mfano:

*i)Kumbatĩlya- Kũkumbatĩlya*.

*ii) Semba-Kũsemba*

### f) Nomino ya kawaida

Nomino ya kawaida ni nomino ambayo hutaja viumbe, vitu na hali kwa jumla kama vile mtoto, shule na kitabu (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2016). Mifano ya Kikamba ni *kĩsululu* (baiskeli), *kĩvĩla* (kiti) na *sukulu* (shule). Nomino nyingi tulizochunguza zilikuwa za kawaida. Kwa mfano *ĩthe* (baba), *mbisũ* (chungu), *mĩsyĩ* (mishale/ njiti za kiberiti) na *maangi* (mishale). Maana za nomino zilichunguzwa kwa kufuata vigezo vitatu:

i) Muktadha

ii) Maelezo ya wazee

iii) Maelezo ya watoto

## 4.1.1.1 Maana ya nomino kwa mujibu wa Muktadha

Muktadha ni vile vitu vinavyozunguka tukio la kimawasiliano (Charles, 2000). Nadharia ya Nyanja za Kisemantiki ilifaa katika uchanganuzi huu. Mhimili uliotumika katika uchanganuzi wa data ni usemi maarufu wa Firth (1951) ulionukuliwa na Prakasam na Abbi (2018) kwamba maana ya neno hujulikana kutokana na washirika wa neno hilo au maneno yanayolizunguka neno. Biblia mbili B1 na B2 zilitumiwa kutupatia muktadha wa matumizi ya nomino thelathini zilizoteuliwa. Nia ya kuangalia muktadha wa matumizi ni kuchunguza iwapo nomino za B1 zilipatikana katika B2 na iwapo maana ilikuwa sawa au ilibadilika. Mhimili mkuu ulioongoza uchanganuzi katika sehemu hii ni wa nadharia ya Dhana unaoshikilia kwamba maana ya leksimu ni dhana au taswira inayoibuliwa na leksimu hiyo akilini mwa mwanalugha wakati leksimu hiyo inapotajwa. Ufuatao ni uchanganuzi wa maana za nomino kwa mujibu wa muktadha wa B1 na B2:

B1

***Asa***- Maana zilizojitokeza katika B1 zilikuwa mbili. Maana ya kwanza ni 'baba' yaani mzazi wa kiume. Maana ya pili ya nomino hii ni 'Mungu'. Biblia yenyewe inasema kwamba Mungu ni baba (Zab. 68:5-6). Vifungu vifuatavyo vinaonyesha maana hizi mbili za nomino *asa*.

a) Kikamba: *…mwĩĩ na nthakame itikwonetye ũũ, ĩndĩ nĩ <u>Asa</u> wakwa ũla wĩ ĩtuni* (Mat.16:17).

Kiswahili: …mwili na damu havijakuonyesha hivyo, bali ni <u>Baba</u> yangu aliye mbinguni.

b) Kikamba: *Nĩngũkĩla nĩthi kwa <u>asa</u> wakwa*… (Lk. 15:18).

Kiswahili: Nitainuka niende kwa <u>baba</u> yangu...

Katika mfano wa kwanza (*a) Asa* yenye herufi kubwa mwanzoni ilikuwa na maana ya Mungu. Katika mfano wa pili (*b)* tunaona mwana mpotevu akiamua kumrudia *asa* (baba) na kumwomba msamaha baada ya kufuja mali yake yote kwa uasherati. Nomino hii iliyoanza kwa herufi ndogo ilirejelea 'baba mtu'. Katika B2 nomino *Asa* ipo lakini imetumiwa katika muktadha mmoja tu kurejelea *Mungu.* Hupatikana hasa katika sala ya Bwana (The Lords prayer) katika imani ya dini ya Kikristo (Mat.6:9-13) na hakuna muktadha mwingine ambapo nomino *asa* inapatikana.

B2

***ĩthe*** ni nomino mbadala iliyoandikwa katika B2 kurejelea dhana 'baba'. Dhana hii awali iliwakilishwa na nomino *asa* yenye herufi ndogo mwanzoni. Sentensi zifuatazo zimenukuliwa kutoka Biblia ya Kikamba cha sasa B2 ambapo 'mwana mpotevu' aliwaza moyoni na kuamua kurudi nyumbani kwa baba mzazi:

Kikamba: *Nĩngũkĩla nĩsyoke kwa* <u>*ĩthe*</u> *wakwa*…(Lk.15:18).

Kiswahili: Nitainuka nirudi kwa <u>baba</u> yangu…

Kutokana na maelezo haya, inabainika kwamba katika Biblia B2, dhana ya awali ya ‘baba mzazi’ inarejelewa kwa kutumia nomino *ĩthe* na nomino *Asa* yenye herufi kubwa mwanzoni ikabaki na maana moja ya ‘Mungu’. Tukio hili linafanya watoto wanaosoma B1 kitabu cha *Luka* (15:18) kuchukulia *asa* kama ‘Mungu’ anayerejelewa.

B1

***ĩkanga***- Nomino hii ilikuwa na maana ya ‘mlinzi wa jela’ katika muktadha wa B1. Maana hii inabainika katika kitabu cha Matayo sura ya tano (5) ambapo Yesu anawafundisha watu kuhusu kutafuta upatanisho na ndugu waliowakosea kabla hawajapeleka kesi kortini kwa hakimu. Hayo yanathibitishwa katika mfano ufuatao:

Kikamba: …*na mũsili aikũnengane kwa* <u>*ĩkanga*</u> *noyĩkw'a kolokolonĩ* (Mat. 5:25).

Kiswahili: …hakimu atakukabidhi kwa mlinzi wa jela utupwe korokoroni.

Kwa mujibu wa kifungu hiki, nomino *ikanga* ina maana ya ‘mlinzi wa jela’.

B2

***Mũsikalĩ***- Hii ni nomino iliyotumiwa katika B2 badala ya nomino *ĩkanga*. Nomino *mũsikalĩ* imekopwa kutoka nomino ya Kiswahili *askari* lenye maana ya ‘mtu anayelinda usalama wa nchi’. Ingawa muktadha wa matumizi ni mmoja nomino zilizotumiwa kurejelea dhana ile ile ni tofauti. Tuangalie sentensi zifuatazo kama zilivyoandikwa katika B2.

Kikamba: …*nake musili aikunengane kwa* <u>*asikali*</u> *makuvingie yela* (Mat. 5:25).

Kiswahili: …naye hakimu atakukabidhi kwa <u>askari</u> wakufungie jela.

Katika B2 nomino mbadala iliyotumiwa ni *asikali* ambayo ni wingi wa *mũsikalĩ*. Dhana ya awali 'mlinzi wa jela' imerejelewa kwa kutumia nomino 'mũsikalĩ' ambayo inazua maana pana zaidi. Kuna askari wa viwango mbalimbali kama vile askari jeshi, askari kanzu, askari jeshi na askari polisi. Maana inayojitokeza katika B2 ni pana. Nomino *ĩkanga* haipo katika B2.

B1

***ĩlawa***- Nomino hii ilikuwa na maana ya chachu. Chachu ilitengenezwa na kuvu hai kwenye mazingira baada ya kuacha unga uliokandwa bila kufunikwa. Baadaye unga uliumuka na kupata ladha ya chachu. Unga huu ndio uliotumiwa katika uokaji ili kuumua mikate na kuichachusha. Maana hii inajitokeza katika Biblia ya Kikamba cha kale B1 katika kitabu cha *Mathayo*. Mitume wa Yesu walikuwa wamesahau kubeba mikate katika safari yao.

Kikamba: *Na Yesu amea*, "*Imanyĩlĩĩlei na ĩsũvĩei* <u>*ĩlawa*</u> *ya Avalisi na Asatukai*" (Mat.16:5-6).

Kiswahili: Yesu akawaambia, "Muwe waangalifu na mtahadhari <u>chachu</u> ya Mafarisayo na Masadukayo."

Maana ya nomino *ĩlawa* kwa mujibu wa mitume wa Yesu ni *chachu* iliyotumiwa katika uokaji wa mikate. Lakini Yesu aliwaambia kuwa hakuzungumzia mikate wala chachu inayoumua na kuchachusha unga. Hayo yanathibitishwa katika B1 (Mat. 16:12) kama tunavyoona hapa:

Kikamba: *Na ĩndĩ mamanya kana ndanamatavya mesũvĩe* <u>*ĩlawa*</u> *ya imũtũ, ĩndĩ nĩ ĩlawa ya* <u>*ũmanyĩsyo wa Avalisi na Asatukai*</u> (Mat.16:12).

Kiswahili**:** Basi wakaelewa kwamba hakuwaambia watahadhari chachu ya mikate bali mafundisho hasi ya Mafarisayo na Masadukayo. Kutokana na muktadha wa B1 inabainika kwamba nomino *ĩlawa* ilikuwa na maana mbili katika B1:

i) Chachu asilia iliyotumiwa kuumua na kuchachusha unga

ii) 'Mafundisho hasi' ya Mafarisayo na Masadukayo

B2

***Mbota***- Hii ni nomino iliyotumiwa katika B2 badala ya nomino *ĩlawa* (B1). Poda ilitumiwa katika B2 kwa sababu njia ya zamani ya uokaji imepitwa na wakati na ndiyo maana nomino *ĩmisi* ilikoma kutumika. Katika Kiswahili neno hili ni *poda*. Poda inayozungumziwa katika kitabu cha Mathayo (16:5-6) ni kemikali mfano wa unga mweupe ambayo hutumiwa katika uokaji ili unga uwe mwepesi (*Oxford Advanced Learners' Dictionary,* 2020). Kemikali hii huumua unga wala haichachushi kwa kuwa unga hauhitaji kuwekwa kwa muda mrefu. Mbinu ya zamani ya kukanda unga na kuuacha kwa muda mrefu hadi ukapata chachu na ukaumuka imepitwa na wakati.

Mfano ufuatao ulithibitisha hayo:

Kikamba: *Yesu nĩwameie atĩĩ, ĩsũvĩei na mũyĩsianĩa na mbota ya Avalisi na Asatukai*

(Mat.16:5-6).

Kiswahili: Yesu akawaambia, tahadharini na mjikinge dhidi ya poda ya Mafarisayo na Masadukayo.

Maana ya *poda* katika mfano huu ni kemikali mfano wa unga mweupe ambayo hutumiwa katika uokaji. Maana nyingine ya nomino *mbota* ilipatikana katika kitabu

cha *Mathayo* (16:12) katika B2. Maana hiyo ni ‘mafundisho hasi ya Mafarisayo na Masadukayo’. Maana hiyo imethibitishwa katika sentensi ifuatayo:

Kikamba: *Na ĩndĩ mamanya kana ndanamatavya mesũvĩe mbota ya mikate, ĩndĩ nĩ* *mbota* *ya* *ũmanyĩsyo wa Avalisi na Asatukai* (Mat.16:12).

Kiswahili**:** Basi wakaelewa kwamba hakuwaambia watahadhari ‘poda’ ya mikate bali mafundisho hasi ya Mafarisayo na Masadukayo.

Kutokana na uchanganuzi huu wa Biblia B1na B2 tulibaini kwamba nomino *mbota* ilitumiwa kama kisawe cha nomino *ĩlawa* ingawa maana moja imebadilika. Nomino *mbota* ina maana zifuatazo:

i) Kemikali mfano wa unga mweupe ambayo hutumiwa kuumua unga wakati wa uokaji

ii) Mafundisho hasi ya Mafarisayo na Masadukayo

Tunabaini kuwa maana ya kwanza imebadilika lakini ya pili imebaki vivyo hivyo.

B1

***ĩmisi***- Nomino *ĩmisi* katika B1 inamaanisha ‘shuka maalumu nyeusi’ iliyotumiwa na wanawake kufunikia vitu vya aina yoyote au kutenga sehemu za kulala na kuleta faragha katika nyumba. Kitu chochote kilichofunikwa kwa shuka hii kisingeweza kutambulika. Nomino hii ilitumiwa katika mahubiri mlimani ambapo Yesu aliwaambia watu wasifunike matendo mema. Sentensi inayofuata imenukuliwa kutoka kitabu cha *Mathayo*:

Kikamba: *O na andũ maikwatasya taa na kũw’ia ungu wa ĩmisi ĩndĩ maw’iaa vala vatũlu* (Mat.5:15).

Kiswahili: Watu hawawashi taa na kuisetiri kwa shuka nyeusi, bali huiweka palipoinuka.

Mfano uliotolewa unabainisha kwamba kazi ya shuka hii nyeusi ilikuwa hasa kusetiri vitu visionekane. Katika jamii ya sasa shuka hii haipo na nomino *ĩmisi* haitumiwi katika mazungumzo ya kawaida. Biblia ya Kikamba cha sasa B2 haina nomino hii na wala haitumiwi katika mazungumzo ya kawaida katika jamii ya Wakamba.

B2

***Mbisũ***- Nomino hii inapatikana katika Biblia B2 ikitumiwa badala ya nomino *ĩmisi*. Maana ya *mbisũ* ni chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kukaushwa kwa kuchomwa kwa moto. Baada ya kuchomwa kifaa hiki hubadilika kuwa cheusi kutokana na moshi wa kuni. Baada ya kutoweka kwa *ĩmisi* katika jamii ya Wakamba, nomino *mbisũ* (chungu) ilitumiwa katika B2 badala ya nomino iliyokoma kutumiwa. Matumizi ya *mbisũ* ni tofauti na ya *ĩmisi* kwa kuwa *mbisũ* ni kifaa kilichotumiwa (na pia hutumiwa sasa) kupikia na kuhifadhia maji na nafaka ilhali *ĩmisi* ni kitambaa kilichotumiwa kufunikia vitu. Sentensi ifuatayo imenukuliwa katika B2 na inathibitisha hayo:

Kikamba: *Vai mũndũ ũkwatasya taa na kũw'ia uungu wa mbisũ, ĩndĩ nũwilĩĩlaa vandũ vatũlu* (Mat.5:15).

Kiswahili: Hakuna awashaye taa na kuifunika kwa chungu, bali huiweka palipo juu.

Kwa mujibu wa maelezo haya, maana ya nomino *ĩmisi* imesogezwa kwa kuzingatia mfanano wa rangi ya shuka iliyoitwa *ĩmisi* na *mbisũ* (chungu cha kupikia). Vitu hivi viwili ni vyeusi kwa hivyo huu ni usogezi wa kiistiara. Usogezi huu ulitokea kutokana na kutoweka kwa nomino *ĩmisi* pamoja na maana iliyowakilishwa na nomino hiyo.

Ikatokea haja ya kutafuta nomino nyingine inayofahamika maana miongoni mwa Wakamba wa karne hii ya ishirini na moja (21).

B1

***Isamũ***- Nomino hii iko katika wingi na umoja wake ni *kĩsamũ*. Maana yake kama ilivyotumiwa katika B ni ‘mavuno ya shambani’. Haijabainika aina ya mavuno yaliyotajwa. Maana hii inapatikana katika kitabu cha *Luka* mlango wa kumi na mbili (12). Yesu aliwafundisha watu akitumia mfano kuhusu 'tajiri mjinga' aliyepata mavuno mengi sana akashindwa mahali pa kuyahifadhi. Akajisemea:

Kikamba: *Ngathasya makũmbĩ makwa, nake angĩ manene; na vau ngatuĩsya isyo syakwa na <u>isamũ</u> syakwa syonthe* (Lk. 12:18).

Kiswahili: Nitabomoa maghala yangu, nijenge mengine makubwa; na humo nitahifadhi nafaka zangu na <u>mavuno</u> yangu yote.

Katika mfano huu tunaona kwamba tajiri huyu alinuia kuhifadhi nafaka katika maghala pamoja na vitu vinginevyo vyote vilivyovunwa shambani. Kwa hivyo nomino *isamũ* ilikuwa na maana ya jumla ya mavuno kama vile mihogo, viazi na maboga.

B2

***Syĩndũ***- Katika Kikamba cha sasa kilichoandikwa katika B2, nomino *isamũ* haipo. Badala yake nomino *syĩndũ* imetumika. Nomino hii inapatikana katika Biblia ya Kikamba cha sasa B2. Maana asilia ya nomino hii ni ‘vitu vya aina yoyote’. Limetumiwa katika B2 kurejelea vitu vya aina yoyote ambavyo mkulima aliyetajwa alikuwa navyo. Imebainika kwamba vitu hivyo havihusiani na mazao ya shambani. Kifungu kifuatacho kilichonukuliwa kutoka B2 kinathibitisha hayo:

Kikamba: …*na vau ngeekĩa ngetha yakwa yonthe na syĩndũ ila ingĩ nĩnasyo* (Lk. 12:18).

Kiswahili: ...humo nitahifadhi mavuno yangu yote pamoja na vitu vinginevyo nilivyo navyo.

Tajiri 'mjinga' aliyenukuliwa katika Biblia alihifadhi mavuno yote katika ghala na pia kuhifadhi vitu vinginevyo alivyomiliki. Huenda vitu hivyo vingine vilikuwa pembejeo za kilimo. Tafsiri hii ya B2 imebadilisha maana iliyokusudiwa katika B1.

B1

***Ĩthweo-*** Nomino hii imetumiwa katika B1 kurejelea 'mkusanyiko wa matone ya maji yaliyoganda juu angani'. Katika lugha ya Kiswahili ni 'wingu'. Imetumika katika kitabu cha *Mathayo* kurejelea yaliyotendeka mlimani wakati uso wa Yesu Kristo ulipogeuka ukang'aa sana (transfiguration):

Kikamba: *Akĩneena, sisya ĩthweo ĩtisũku yamekĩa muunyĩ; na sisya, wasya wauma ĩthweonĩ ũkyasya*… (Mat.17:5).

Kiswahili: Alipokuwa angali akizungumza, tazama wingu jeupe likawafunika; na tazama, sauti ikasikika kutoka winguni ikisema…

Tukiangalia Biblia B2 nomino *ĩthweo* haipo. Nomino badala iliyotumiwa ni *ĩtu*.

B2

***Ĩtu-*** Katika B1, nomino hii ilitumika kumaanisha 'mahali palipo juu zaidi' ambapo huaminika ni makao ya Mungu na vitu vingine kama vile nyota, mwezi na mawingu hupatikana. Katika Kiswahili ni 'mbingu'. Maana hiyo bado ipo katika B2. Kwa mfano katika kitabu cha Luka (Lk. 24:51):

Kikamba: *Aendee na kûmaathima nĩwoosiwe kuma vala maĩ ambatw'a ĩtunĩ* (Lk. 24:51).

Kiswahili: Angali akiwabariki alitwaliwa akapalizwa mbinguni. Maana iliyojitokeza hapa ni 'mahali, hasa makao ya Mungu'.

Nomino hii imetumiwa pia katika B2 badala ya nomino *ĩthweo* ambayo imekoma kutumika katika mazungumzo. Maana yake ni 'wingu'. Matumizi ya nomino hii ni kama ifuatavyo:

Kikamba: *Vetelo aendee kũneena, ĩtu yaĩ yeũ kw'ũ nĩyesĩlile ĩũlũ woo yamavw'ĩka onthe, na wasya weew'ika wumĩte ĩtunĩ yĩũ ũkwasya atĩĩ...* (Mat. 17:5).

Kiswahili: Petro angali akizungumza, wingu lililokuwa jeupe pe lilipita juu yao likawafunika wote, na sauti ikasikika katika wingu hilo ikisema hivi...

Wingu ni kitu kinachopatikana mbinguni kwa hivyo dhana inayorejelea sehemu kubwa *mbingu* imesogezwa kurejelea kitu kidogo *wingu* au dhana pana imetumiwa kuwakilisha dhana finyu. Aidha, nomino *ĩtu* imepanuka maana.

B1

***Kĩmũtũ***- Katika lugha ya Kikamba, wingi wa nomino hii ni *ĩmũtũ*. Kwa mujibu wa B1, hiki ndicho kilichokuwa chakula kikuu cha Wayahudi kwa kuwa ndicho chakula kilichotajwa mara nyingi katika Biblia B1. Vyakula vinginevyo vilivyotajwa ni kama vile *nyama* (nyama) katika *Mwanzo* (27:7), *ũsũũ* (uji) katika *Mwanzo* (25:29) na *makûyû* samaki (Mat.14:16). *Kĩmûtû* ni chakula ambacho kiliokwa kwa unga wa ngano kwa hivyo tunaweza kusema ni aina ya mkate. Baada ya Yesu kuwahubiria watu, ulifika wakati wa jioni na wakahisi njaa. Yesu aliwaamuru mitume wawape watu chakula nao wakamjibu:

Kikamba: *Vaa tuĩ na kĩndũ ateo imũtũ itano na makũyũ elĩ* (Mat.14:16).

Kiswahili: Hatuna chochote hapa ila mikate mitano na samaki wawili.

Chakula hiki (imũtũ) kilibarikiwa wakala wote wakashiba na kusaza. Wakati wote Yesu na mitume wake pia walionekana wakila chakula hiki. Jioni Alhamisi wakati wa chajio cha mwisho kabla Yesu hajakamatwa na Wayahudi, walikula *kĩmũtũ*. Hata hivyo, neno hili limepata maana hasi miongoni mwa wanajamii. Maana yake sasa ni chakula ambacho hakijaiva vizuri. Aghalabu utasikia mtu akisema, fulani hajui kusonga ugali, alitupikia *kĩmũtũ* tukashindwa kula! Biblia ya Kikamba B2 haina nomino hii na badala yake nomino *mũkate* (mkate) imetumiwa kuwakilisha dhana hiyo ya zamani. Kwa hivyo watoto wa sasa wakisoma Biblia B1, hawatafahamu maana ya neno hilo.

B2

***Mũkate***- Hii ni nomino mkopo kutoka lugha ya Kiswahili. Ilikopwa ili kuziba pengo la msamiati lililoachwa baada ya nomino *kĩmũtũ* kusambaratika au kupata maana duni. Tutazame matumizi ya nomino hii katika B2:

Kikamba: *Twĩna mĩkate o ĩtano na makũyũ elĩ vaa!* (Mat. 14:16).

Kiswahili: Tunayo mikate mitano tu na samaki wawili hapa!

Kama inavyoonekana katika sentensi iliyonukuliwa, nomino *imũtũ* haipo tena katika Biblia ya Kikamba cha sasa B2. Dhana ya awali sasa inarejelewa kwa kutumia nomino mkopo *mĩkate*. Sababu ni kwamba jina ambalo lilikuwa limebuniwa awali kurejelea chakula hiki lilipata maana duni kwa hivyo nomino *mũkate* ikakopwa kutoka lugha ya Kiswahili ‘mkate’.

B1

***Manzĩ-*** Hii ni nomino ya Kikamba cha kale inayopatikana katika B1. Maana yake ni kiowevu kipatikanacho katika mito, maziwa, mabwawa, visima, vinamasi na sehemu nyinginezo kama hizo. Kiowevu hiki hunywewa kukata kiu na kutumiwa katika shughuli mbalimbali kama vile kufulia nguo, kuogea na kunyunyizia mimea. Katika lugha ya Kiswahili ni 'maji'. Katika B1 kimuktadha:

Kikamba: …*ta mũtĩ ũvandĩtwe ũtee wa mbũsĩ syĩ manzĩ*... (Zab. 1:3).

Kiswahili: …kama mti uliopandwa kando ya mito yenye maji…

Katika mfano huu, nomino *manzĩ* inarejelea kiowevu kinachopatikana mitoni na ambacho pia hunawirisha mimea. Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba katika B1, *manzĩ* ni nomino inayorejelea 'maji'.

B2

***Kiw'u-*** Katika Biblia ya Kikamba B2, nomino *manzĩ* haipo na badala yake nomino *kĩw'ũ* imetumiwa. Nomino hii ni ya Kikamba cha sasa. Imetumiwa katika Biblia B2 kurejelea kiowevu kinywewacho ili kukata kiu. Sentensi ituatayo imenukuliwa kutoka Biblia ya Kikamba B2 na **inathibitisha maelezo hayo:**

Kikamba: …*ta mũtĩ ũvandĩtwe ũtee wa tũlũsĩ twĩ kĩw'ũ* (Zab. 1:3).

Kiswahili: …kama mti uliopandwa kando ya vijito vyenye maji.

Inadhihirika kwamba Biblia ya Kikamba cha sasa imetumia nomino *kĩw'ũ* kurejelea dhana asilia ya 'kiowevu kinywewacho'. Nomino *manzĩ* ilikoma kutumika.

B1

***Mata***- Katika Kikamba cha zamani nomino hii ilikuwa na maana mbili. Maana moja ilikuwa 'kiowevu kipatikanacho kinywani' ambacho katika lugha ya Kiswahili ni ‘mate’. Mfano ulitolewa kutoka kitabu cha *Mathayo*, sura ya ishirini na saba (27) mstari wa thelathini (30). Ni wakati wa mateso ya Yesu, baada ya kukamatwa na askari. Walimdhihaki, kumpiga na kumtemea mate. Maana ya pili ilikuwa 'upinde unaotumiwa kufumia mshale'. Maana hizi mbili zinaonekana katika sentensi zifuatazo zilizonukuliwa kutoka B1.

Kikamba: *Na mamũtw’ĩla mata*…(Mat.27:30)

Kiswahili: Na wakamtemea mate...

Kikamba: *Athũku makũĩte ũvyũ na nĩmakootete mata moo* (Zab.37:14).

Kiswahili: Waovu wamechomoa sime na wamekaza pinde zao.

Katika sentensi (a) nomino *mata* inarejelea ‘mate’ lakini katika sentensi (b) nomino hiyo maana inarejelea ‘upinde’. Kwa hivyo ilikuwa nomino ya kipolisemia. Hata hivyo katika Kikamba cha sasa kinachozungumzwa na kuandikwa katika karne hii ya 21, nomino *mata* inarejelea kiowevu kitokacho kinywani pekee. Katika Kiswahili ni ‘mate’. Maana moja imedondoshwa ikabakia maana moja tu. Maana iliyodondoshwa sasa inarejelewa kwa kutumia nomino *uta*.

B2

***Ũta***- Wingi wa nomino hii ni *ngũta* au *mbũta*. Ndiyo nomino iliyotumiwa katika B2 badala ya nomino *mata* kurejelea zana ya vita inayoitwa ‘uta’ kwa Kiswahili. Sentensi ifuatayo imetumia nomino *ũta* kurejelea zana ya vita:

Kikamba: *Ala athuĩku makũãa ũvyũ na kuĩkoota ũta*…(Zab.37:14).

Kiswahili: Walio waovu huchomoa sime na kukaza upinde...

Kama inavyobainika, dhana ya ‘zana ya vita ya kurushia mishale’ inarejelewa kwa kutumia nomino mkopo *ũta*. Sababu ya ukopaji ilikuwa kuondoa utata uliokuwapo wa kubainisha dhana iliyorejelewa na nomino *mata*. Ilikuwa vigumu kuelewa iwapo mzungumzaji alirejelea ‘mate’ au ‘upinde’. Kwa hivyo wakati wa kuchapishwa tena Biblia mwaka wa 1974 nomino mkopo *ũta* ilitwikwa jukumu la kurejelea ‘upinde’.

B1

***Mathatwa-*** Nomino mathatwa iliteuliwa kutoka B1. Maana yake ilikuwa ‘mifuko iliyoundwa kwa ngozi za wanyama’. Mifuko hii ilitumiwa hasa kuhifadhi mvinyo na asali. Maneno yafuatayo yanaonyesha matumizi ya nomino *mathatwa*:

Kikamba: *Vai mũndũ wĩkĩaa mbinyu mbĩthĩ mathatwanĩ makũũ; nĩkwĩthĩwa eekĩa, mbinyu mbĩthĩ ĩkatembũa mathatwa asu* (Lk.5:37).

Kiswahili: Hakuna anayetia mvinyo ‘mbichi’ katika mifuko mikuukuu; kwa kuwa mvinyo ‘mbichi’ utairarua mifuko ile. ‘Mvinyo mbichi’ hapa unarejelea mvinyo ambao ni safi na haujakaa ka muda mrefu.

Kutokana na kifungu kilicho hapa juu, tunapata mdokezo kwamba nomino *mathatwa* inarejelea chombo maalumu ambacho kilitumiwa kuhifadhia mvinyo. Malighafi yaliyotumiwa kuundia chombo hiki si chuma wala mbao kwa kuwa haya hayararuki kama tunavyoelezewa katika kifungu. Ngozi ya mnyama ndiyo iliyotumiwa kuundia mifuko, mavazi na bidhaa nyinginezo. Katika Biblia ya Kikamba cha sasa B2 nomino *mathatwa* haipo. Badala yake nomino *ikuu* imetumiwa.

B2

***Ikuu-*** Nomino hii iko katika wingi. Umoja wake ni *kĩkuu*. Katika lugha ya Kiswahili ni 'vibuyu'. Nomino hii imetumiwa katika Biblia ya Kikamba cha sasa ikiwa na maana ‘mazao ya mmea unaotambaa na ambayo hutumiwa kama vyombo vya kuhifadhia maji na vitu vingine viowevu’. Sentensi ifuatayo inathibitisha maana na matumizi ya nomino *ikuu*:

Kikamba: *O ta ũũ vai mũndũ wĩkĩaa ndivai nzaũ ikuunĩ ngũũ; akeka ũũ ndivai ĩsu nzaũ no yatũẽ ikuu isu na ĩyĩtĩka*... (Lk.5:37).

Kiswahili: Vile vile hakuna anayehifadhi divai mpya katika vibuyu vikuukuu; akifanya hivyo divai itapasua vibuyu na kumwagika…

Nomino *ikuu* imetumiwa badala ya nomino *mathatwa* kwa kuwa matumizi ya *mathatwa* yalipitwa na wakati. Baada ya kutoweka kwa mifuko hii iliyoitwa *mathatwa* Wakamba walianza kuhifadhi viowevu vyote katika *ikuu* au vibuyu.

B1

***Mĩsyĩ-*** *Mĩsyĩ* ni wingi wa *mũsyĩ*. Maana yake katika Kikamba cha kale ni zana za vita zilizoundwa kwa chembe na vijiti. Katika Kiswahili ni mishale. Hii ndiyo maana inayojitokeza katika B1 kama inavyonukuliwa katika wimbo wa Daudi akimsifia Mungu kwa kumwokoa dhidi ya maadui:

Kikamba: *Nake ekya mĩsyĩ yake na amanyaĩĩkya*… (Zab. 18:14).

Kiswahili: Naye akafuma mishale yake akawatawanya...

Katika Kikamba cha sasa, maana ya nomino *mĩsyĩ* imebadilika. Nomino hii sasa inarejelea dhana tofauti 'njiti za kiberiti'. Kwa hivyo katika muktadha wa B2 katika kitabu cha *Zaburi* 18:14 nomino *mĩsyĩ* haipo. Nomino mbadala iliyoandikwa ni *maangi*.

B2

***Maangi-*** Nomino hii iko katika wingi. Katika umoja ni *ĩangi*. Imetumiwa katika B2 badala ya nomino *mĩsyĩ* kurejelea 'mishale'. Sentensi ifuatayo inabainisha muktadha wa kimatumizi wa nomino *maangi*:

Kikamba: *Nĩwekisye <u>maangi</u> make na anyaĩĩkya amaitha make* (Zab.18:14).

Kiswahili: Alifuma <u>mishale</u> yake na kuwatawanya maadui zake.

Mfano huu ni dhihirisho kwamba Biblia ya Kikamba B2 imetumia nomino *maangi* kurejelea 'zana za vita zinazotumiwa pamoja na upinde au uta'. Sababu ni kwamba iliibuka miti mingine iliyofanana na mishale ambayo huwashwa kwa kiberiti. Matumizi ya maana hii shindani yalizidi yale ya kirejelewa asilia. Maana hiyo asilia hatimaye iliundiwa nomino tofauti ya kuiwakilisha. Nomino hiyo ni *maangi*.

B1

***Mwenyu-*** Nomino hii ilitumika katika Kikamba cha kale kumaanisha mzazi wa kike wa mtu. Katika Kiswahili ni 'mama yako' au pia 'mama yenu'. Mzizi *mw-* ndio unaobeba maana ya 'mama'. Tukiuambatanisha na kimilikishi cha nafsi ya kwanza wingi *-itũ* (-etu) tutaunda nomino *mwaitũ* yenye maana 'mama yetu'. Mzizi huo ukiambatanishwa na kimilikishi *-enyu* (enu) cha nafsi ya pili wingi tutapata nomino *mwenyu* (mama yenu). Katika nafsi ya tatu nomino inayotumiwa kurejelea mama ni *nyiny'a* (mama yake). Nomino hii ilikopwa kutoka Kiswahili cha kale 'nina'. Kifungu kifuatacho kinathibitisha maana ya nomino *mwenyu:*

Kikamba: *Mwenyu na ana-a-mwenyu maũngeme nza, nĩmekwenda ũkwona* (Lk. 8:20).

Kiswahili: Mama yako na wana wa mama yako (ndugu zako) wamesimama nje, wanataka kukuona.

Inadhihirika kwamba nomino hii ilitumika katika mazungumzo ya kawaida kurejelea mama wa mtu. Lakini katika Kikamba cha sasa nomino hii haitumiki kabisa katika muktadha wa mazungumzo ya kawaida. Hutumiwa na mtu aliyeudhika kuhusu jambo fulani au katika matusi. Kwa mfano iwapo mtu fulani msimamizi wa pesa za umma atatumia pesa hizo vibaya zikose kuwafaa waliokusudiwa itasikika walioudhika wakimwuliza, "*I mbesa ko sya mwenyu*?" (Kwani pesa hizi ni za mamako?). Biblia ya Kikamba chapa ya IT la 2011 inathibitisha kuwepo kwa mabadiliko ya maana. Nomino iliyotumiwa ni *iny'a*.

B2

***Inyia-*** Nomino hii pia hutamkwa *nyinyia* au *nyiny'a*. Maana yake ni mama (nina). Mara nyingi huambatanishwa na vimilikishi katika sentensi. Kwa mfano:

a) *Inyia wakwa, waku, wake* (Mama yangu, yako, yake).

b) *Inyia witu, wenyu, woo* (Mama yetu, yenu, yao).

Matumizi katika Biblia ya Kikamba cha sasa B2 ni kama ifuatavyo:

Kikamba: *Inyia waku na ana-a-inyia maku me vaya nza na nĩmekwenda ũkũtumũsya* (Lk.8:20).

Kiswahili: Mama yako na wana wa mama yako (ndugu) wako nje na wanataka kuzungumza nawe.

Biblia ya Kikamba cha sasa B2 imetumia nomino *inyia* katika vifungu vyote vinavyomtaja mama. Nomino *mwenyu* haijatajwa popote katika B2. Nomino hiyo haitumiwi katika mazungumzo ya kawaida katika jamii ya Wakamba.

B1

***Mwĩãi-*** Maana mbili za nomino hii hii zilipatikana katika kitabu cha *Mwanzo* sura ya kumi na nane (18). Maana ya kwanza ni 'Mungu'. Maana hii ilipatikana katika mazungumzo baina ya Ibrahimu na Mungu akimsihi Mungu asiwaangamize Wanasodoma na Wanagomora wote, wema kwa waovu pamoja. Sentensi ifuatayo ilinukuliwa ili kuchunguza maana ya nomino *Mwĩãi*:

Kikamba: *Na (Avalaamu) amwĩã, sisya yu, nĩñakwata kũñeena na* <u>*Mwĩãi*</u>. (Mw.18:31).

Kiswahili: (Ibrahimu) akamwambia, tazama sasa nimeanza kuzungumza na <u>Mungu</u>.

Nomino *Mwĩãi* inayoanza kwa herufi kubwa inarejelea Mungu. Maana hii imedumishwa katika B2 kwa maana mara nyingi jina *Mwĩãi* limetumiwa kumrejelea Mungu (taz. Mw.18:31, B2).

Maana ya pili ya nomino hii ni 'mume'. Maana hii ilidhihirika katika mazungumzo ya Sara mkewe Ibrahimu baada ya malaika wa Mungu kumpasha mumewe habari kwamba angepata mtoto wa kiume. Maneno ya Sara yamenukuliwa kama ifuatavyo:

Kikamba: *Nĩ mũtumĩũ ngeethĩwa na mũyo,* <u>*mwĩãi*</u> *wakwa nake e mũtumĩũ*? (Mw.18: 12).

Kiswahili: Katika uzee wangu nitaonaje raha (katika ndoa), <u>mume</u> wangu naye tayari amezeeka?

Nomino *mwĩai* katika kifungu hiki imeanza kwa herufi ndogo na ina maana ya mume. Katika B2, nomino *mwĩai* imetumiwa kumtajia Mungu peke yake. Haitumiwi kumtajia mume. Nomino iliyotumiwa kurejelea ‘mume’ ni *mũtumĩa*.

B2

***Mũtumĩa***- Hii ni nomino iliyoandikwa katika B2 badala ya nomino *mwĩai*. Katika muktadha huu inamaanisha ‘mume’. Sentensi ifuatayo imenukuliwa kutoka kitabu cha *Mwanzo* katika B2 na inatupatia muktadha wa nomino *mũtumĩa*:

Kikamb**a**: *Nyie nĩ mũkũũ na nditonya kwĩthĩwa na ũtanu wa kũmanyana kĩ-mwĩĩ na mũtumĩa wakwa nũndũ o nake nĩ mũkũũ* (Mw.18:12).

Kiswahili: Mimi ni mzee wala siwezi kufurahia kujuana kimwili na mume wangu kwa kuwa yeye pia ni mzee.

Nomino *mwĩai* haipo katika sentensi iliyonukuliwa hapa kwa kuwa kwa sasa inarejelea Mungu pekee. Dhana ‘mume’ hurejelewa kwa kutumia nomino *mũtumĩa* ambayo ndiyo iliyoandikwa katika B2.

B1

***Ndũa***- Nomino hii imetumiwa katika B1 kumaanisha 'eneo lenye mijengo mingi mikubwa na wakazi wengi'. Katika Kiswahili ni ‘mjî’. Kifungu kifuatacho kilichonukuliwa kutoka B1 kinafafanua hayo:

Kikamba**:** *Sisyai mwavota ndũanĩ (Yelũsalemu) mũkakomana na mũndũ...* (Lk.22:10).

Kiswahili: Tazameni mwingiapo mjini (Yerusalemu) mtakutana na mtu...

Kutokana na maneno haya tunaona kwamba mahali hapa walipotumwa mitume palikuwa mjini. Sababu ni kuwa palikuwa na majumba makubwa ya ghorofa kama lile

ambalo mitume walienda kuandaa karamu. ‘Atawapeleka juu kwenye chumba kikubwa ambacho tayari kimeandaliwa’ (Lk.22:12). Kwa hivyo nomino *ndũa* kama ilivyotumiwa hapa ilikuwa na maana ya ‘mji’. Katika B2, sentensi iliyonukuliwa hapa juu haijatumia nomino *ndũa*. Nomino mbadala iliyotumiwa ni *mũsyĩ.*

B2

***Mũsyĩ***- Katika muktadha wa B2, maana ya nomino *mũsyĩ* ni 'eneo kubwa lenye watu wengi na mijengo mikubwa mikubwa'. Maana hiyo inajitokeza katika kitabu cha *Luka* sura ya ishirini na mbili (22) mstari wa kumi (10). Maneno hayo yamenukuliwa hapa chini:

Kikamba: *Mwalika mũsyĩnĩ mũnene wa Yelũsalemu, nĩmũũkomana na mũndũ…*(Lk.22:10).

Kiswahili: Mkiingia katika mji mkuu wa Yerusalemu, mtakutana na mtu...

Kwa mujibu wa Biblia hii, maana ya nomino *mũsyĩ* ni eneo kubwa lenye wakazi wengi na mijengo mikubwa au 'mji'. Neno *mũnene* ni kivumishi ambacho kinaonyesha sifa ya 'ukubwa' wa mji Yerusalemu. Ilidhihirika kwamba nomino *ndũa* ilikumbwa na mabadiliko ya maana, ikawa hairejelei 'mji' tena. Ikapata maana ‘kijiji’. Kisha nomino *mũsyĩ* ikapewa jukumu la kuwakilisha dhana ya awali ‘mji’.

B1

***Ũkũngi***- Nomino hii ilikuwa na maana ya ‘upepo mwepesi’ unaovuma na kutoweka ghafla kwa mujibu wa Biblia ya Kikamba cha zamani B1. Matini hii ya Biblia imewafananisha watu waovu na makapi yanayopeperushwa na upepo mwepesi. Makapi hayana thamani yoyote na ni mepesi sana kiasi cha kuweza kupeperushwa na hewa inayovuma kwa kasi ya chini sana. Waovu hawana thamani yoyote na wala hawana

msimamo thabiti. Sentensi inayofuata inathibitisha maana na matumizi ya nomino *ũkũngi*.

Kikamba: *Indĩ mailyĩ ta wewa ũũlũkĩĩw'e nĩ ũkũngi* (Zab.1:4).

Kiswahili: Bali wao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo mwanana.

Mfano uliotolewa hapa unatudokezea kwamba nomino *ũkũngi* ina maana maalumu. Maana yake ni mojawapo ya aina za upepo kama vile *kĩuutani* na *kĩlingi*. *Ũkũngi* ni upepo mwanana ambao hupeperusha vitu vyepesi mno kama vile makapi. Biblia ya Kikamba cha sasa B2 imetumia nomino *kĩseve* badala ya *ũkũngi*.

B2

***Kiseve***: Nomino hii inarejelea hewa inayovuma kwa kasi ya kiwango chochote; kidogo, cha wastani au cha juu. Katika Kiswahili ni upepo. Kuna aina nyingi za upepo mathalani kimbunga, tufani, dhoruba, na aina nyinginezo. Kwa hivyo nomino *kĩseve* inawakilisha dhana pana. Tutazame mfano unaofuata:

Kikamba: *Ĩndĩ mailyĩ ta mavuti maũlũkĩĩw'e nĩ kĩseve* (Zab.1:4).

Kiswahili: Bali wao ni kama taka ipeperushwayo na upepo.

Inadhihirika kwamba nomino *ũkũngi* haipo katika B2. Nomino inayotumika sasa ni *kĩseve* ambayo ina maana pana. Kiseve ni aina yoyote ya upepo au hewa inayoenda kwa kasi ya kiwango chochote. Nomino zilizojadiliwa pamoja na maana zilizojitokeza ziliwekwa katika jedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.1: Maana za Nomino kwa mujibu wa Muktadha**

| Nomino B1 15 | Maana | Nomino B2 15 | Maana | Kitabu cha Biblia |
|---|---|---|---|---|
| Asa | Baba; Mungu | Ĩthe | Baba | Mat.16:17; Lk.15:18 |
| Ĩkanga | Mlinzi wa jela | Mũsikalĩ | Askari | Mat. 5: 25 |
| Ĩlawa | chachu | Mbota | Poda | Mat.16:6 |
| Ĩmisi | Kitambaa cheusi | Mbisũ | Chungu | Mat.5:15 |
| Isamũ | Mavuno | Syĩndũ | Vitu | Lk. 12: 18 |
| Ĩthweo | Wingu | Ĩtu | Wingu | Mat.17:5 |
| Kĩmũtũ | Mkate | Mũkate | Mkate | Mat.4:4 |
| Manzĩ | Maji | Kĩw'ũ | Maji | Zab. 1:3 |
| Mata | Uta, Mate | Ũta | Uta(zana ya vita) | Zab. 37:14, Mat.27:30 |
| Mathatwa | Mifuko ya ngozi | ikuu | Vibuyu | Lk.5:37 |
| Mĩsyĩ | Mishale | Maangi | Mishale | Zab. 18:14 |
| Mwenyu | Mama | Inyia | Mama | Lk. 8:20 |
| Mwĩai | Mume, Mungu | Mũtumĩa | Mume | Mw. 18:12,31 |
| Ndũa | Mji | Musyĩ | Mji | Lk. 22:10 |
| Ũkũngi | Upepo mwanana | Kĩseve | Upepo | Zab.1:4 |

Katika jedwali hili orodha ya kwanza ni ya nomino zilizoteuliwa kutoka B1 na orodha ya pili ni ya nomino zilizoteuliwa kutoka B2. Aidha, tunaona maana ya nomino hizo kwa mujibu wa muktadha wa B1 na B2. Nomino zote kumi na tano (15) za B1 zilipata nomino mbadala katika B2. Nomino kumi na moja (11) za B1 hazikuwamo tena katika Biblia B2 na ilibainika kwamba hazitumiwi tena katika maandishi. Hii ni asilimia sabini na tatu nukta tatu (73.3%) ya nomino kumi na tano (15). Nomino hizo ni *ĩlawa, ĩmisi, isamũ, ĩthweo, kĩmũtũ, manzĩ, mathatwa, mwenyu na ũkũngi*. Nomino tatu (3) za B1 bado zilikuwamo katika B2 lakini zikiwa na maana mojawapo ya maana zake asilia. Idadi hii ni asilimia ishirini (20%). Nomino hizo ni *Asa*, *mata* na *Mwĩai*. Nomino moja (1) *ndũa* ilikuwa na maana tofauti kinzani.

Baadhi ya nomino mbadala za B2 zilibeba maana ya awali na nyingine zilikuwa na maana tofauti. Kwa mfano, nomino tisa (9) za B2 zilikuwa na maana sawa na nomino zilizotumiwa katika B1 au zimetwikwa mojawapo ya maana asilia. Zilidhihirika kama visawe vya nomino za B1. Nomino hizo ni *ĩthe*, *ĩtũ*, *mũkate*, *mũtumĩa*, *kĩw'ũ*, *ũta*, *maangi*, *inyia* na *mũsyĩ*. Idadi hii ni asilimia sitini (60%). Nomino sita (6) zilikuwa na maana tofauti na nomino za B1, nazo ni *mũsikalĩ*, *mbota*, *mbisũ*, *syĩndũ*, *ikuu* na *kĩseve*. Idadi hii ni asilimia arubaini (40%). Maana zilizojadiliwa hapo juu ni kama zilivyojitokeza katika muktadha wa B1 na B2. Ilibainika kwamba michakato mbalimbali ya mabadiliko ya kisemantiki ilikuwa imezikumba nomino zilizochunguzwa. Ndiyo maana baadhi ya nomino zilitoweka zikakosa kuwepo katika B2 na nyingine zikawakilisha dhana tofauti. Uchunguzi zaidi kupitia usaili wa wazee ulibainisha jinsi nomino hizo thelathini (30) zilivyobadilika maana.

#### 4.1.1.2 Maana ya Nomino kwa mujibu wa wazee

Wazee kumi (10) walihojiwa ili kubaini maana asilia na ya sasa ya nomino. Aidha, walibainisha mabadiliko ya kisemantiki yaliyoathiri baadhi ya nomino za B1 na kusababisha kutotumiwa katika B2. Kwa mujibu wa Alawadi (2020) akimnukuu Ogden na Richards (1923), nadharia ya dhana inasisitiza kuwa mzungumzaji wa lugha huwa na taswira akilini mwake ikirejelea kitu halisia katika ulimwengu wa lugha. Aidha, inadai kuwa picha za akilini ni dhahania ya kutosha kuweza kuwakilisha nomino au vitenzi vya kawaida. Kwa hivyo mtafiti aliamini kwamba wazee walizifahamu maana asilia na maana za ziada za nomino zilizochunguzwa. Nomino zote za B1 na B2 zilitumika. Majibu yafuatayo yalitolewa na wazee:

B1

***Asa-*** Wazee sita (6) walisema kwamba maana asilia ya nomino *asa* ni mzazi mwanamume au baba. Kisha baadaye maana hiyo ilisogezwa kwa Mungu kutokana na sifa za ki-baba za Mungu. Mabadiliko ya usogezi wa kiistiari yakafanyika. Wazee wote kumi (10) walisema kwamba maana ya *Asa* ni Mungu. Kwa hivyo maana za nomino hii kwa mujibu wa wazee ni mbili; Mungu na baba mtu.

B2

***Ĩthe***- Hii ni nomino iliyotumiwa katika B2 badala ya nomino *asa*. Wazee wote kumi (10) waliohojiwa walisema kwamba maana ya nomino *ĩthe* ni baba. Nomino hii imebeba maana moja ya nomino *asa* ya B1. Baada ya nomino *asa* kuhusishwa na Mwenyezi Mungu, maana ilibadilika. Ikawa ikitumiwa kumrejelea Mungu pekee. Dhana 'baba mzazi' ikaundiwa nomino *ĩthe*.

B1

***Ĩkanga***- Nomino hii ilitumiwa katika muktadha wa B1 kurejelea 'mlinzi wa jela'. Usaili wa wazee ulitupatia maana tatu za nomino *ĩkanga*. Wazee wawili (2) walisema maana yake ni *mũsikalĩ wa yela* au kwa Kiswahili 'askari anayelinda jela'. Wengine wawili (2) walisema kuwa *ĩkanga* ni *mũsikalĩ* au askari wa aina yoyote. Maana hii ilikuwa pana kwa maana kuna askari wa aina nyingi kama vile askari jeshi na askari wa magereza. Wazee tisa (9) kati yao walisema kwamba *ĩkanga* ni 'mtu anayepakia abiria garini'. Maana ya nomino hii kwa mujibu wa muktadha ilithibitishwa na asilimia ishirini pekee (20%) huku asilimia ishirini (20%) ikitoa maana ya pili na asilimia tisini (90%) ikiibua maana ya tatu.

B2

***Mũsikalĩ-*** Nomino hii imetumiwa katika B2 badala ya 'ĩkanga'. Tuliwahoji wazee ili kujua iwapo nomino hii mbadala ilikuwa na maana tofauti na nomino *ĩkanga*. Wazee wote kumi (10) walisema kuwa maana ya nomino hii ni 'anayelinda usalama nchini'. Kwa Kiswahili ni 'askari'. Hii ni maana mojawapo ya maana mbili za nomino ya zamani *ĩkanga*. Utafiti ulibainisha kwamba nomino *ĩkanga* ilidondosha maana moja. Maana hii iliyodondoshwa ndiyo iliyotafutiwa jina, likakopwa kutoka msamiati wa Kiswahihi 'askari'. Wazee watatu (3) walitoa maana ya pili ya *mũsikalĩ* kama 'mlinda lango'. Kwa hivyo nomino hii ilikuwa na maana mbili.

B1

***Ĩlawa-*** Maana asilia ya nomino hii ilikuwa moja; chachu asili iliyotengenezwa baada ya unga kutiwa maji na kuachwa utulie kwa muda. Wazee wanane (8) walitoa maana hiyo. Wawili (2) hawakutaja maana.

B2

***Mbota***- Nomino hii mbadala tuliichunguza pia iwapo ilikuwa na maana tofauti na jinsi ilivyobadilika maana. Wazee kumi (10) waliohojiwa walisema kuwa nomino hii ilikuwa na maana ya kitu kama unga mweupe kinachotumiwa kuumua unga wakati wa uokaji. Unga huu ni kemikali na ni njia ya kisasa ya kuumua unga. Njia ya zamani isiyohusisha kemikali imepitwa na wakati. Ndiyo maana jina la zamani *ĩlawa* halipo katika B2 na badala yake nomino *mbota* yenye maana tofauti imetumiwa. Watano (5) kati yao walitoa maana nyingine; unga mweupe wa kujipaka au kujipodoa.

B1

***Ĩmisi***- Nomino hii ilikuwa na maana moja, 'shuka nyeusi' iliyotumiwa na wanawake kusetiri vitu. Maana hiyo ilitoka kwa asilimia arubaini (40%) ya wazee. Asilimia sitini (60%) haikujua maana.

B2

***Mbisũ***- Nomino mbadala iliyoandikwa katika B2 ni ***mbisũ***. Wazee wote (100%) walisema kwamba hiki ni chombo cha mfinyanzi cha kupikia. Maana hii haina uhusiano na maana ya nomino *ĩmisi* katika B1.

B1

***Isamũ*** - Kwa mujibu wa maelezo ya wazee, nomino hii ilikuwa na maana tatu (3). Maana ya kwanza iliyotajwa na wazee wote ni 'mali' au 'jumla ya vitu vya thamani anavyomiliki mtu'. Wazee sita (6) walitaja maana ya pili ambayo ni 'vitu vya aina yoyote' na kisawe chake *syĩndũ*. Maana ya tatu ilitoka kwa wazee sita (6) nayo ni *mamutha ma kĩmbithĩ* au sehemu za siri.

B2

***Syĩndũ***- Hii ni ndiyo nomino mbadala inayopatikana katika B2. Wazee tisa (90%) walisema maana ya nomino *syĩndũ* ni 'mali' yaani vitu vya thamani alivyo navyo mtu. Wanane (80%) kati yao wakataja maana ya pili 'vitu vya aina yoyote'. Maana hizi mbili ni miongoni mwa maana za nomino *isamũ* katika B1. Nomino *syĩndũ* ndiyo inayobeba maana za nomino ya B1 iliyopata mwelekeo hasi.

B1

***Ĩthweo-*** Nomino hii ilimaanisha mkusanyiko wa matone ya mvua yaliyoganda katika angahewa. Katika lugha ya Kiswahili ni ‘wingu’. Maana hii ilitajwa na wazee wote (100%) waliohojiwa huku wakitoa kisawe *ĩtu* (wingu).

B2

***Ĩtu-*** Hii ndiyo nomino iliyotumiwa katika B2 badala ya nomino *ĩthweo*. Wazee kumi (10) walitueleza maana yake kuwa ni ‘wingu’ katika Kiswahili. Wanane (8) kati yao wakatupatia maana ya pili ya nomino hii; ‘mbingu’. Walisema kuwa mbinguni *ĩtu(nĩ)* ni makao ya Mungu. Kwa hivyo maana mbili zilibainika.

B1

***Kĩmũtũ-*** Nomino hii ilimaanisha mkate uliookwa kwa unga uliochachushwa. Wazee wote (100%) ndio waliosema hivyo. Maana mbili zilijitokeza kutokana na uchanganuzi wa majibu ya watoto. Wawili (2) wakiwakilisha asilimia ishirini (20%) walitoa maana ya jumla kwamba *kĩmũtũ* ni *lĩũ* au chakula. Wengineo wanane (8), yaani asilimia themanini (80%) waliandika kwamba *kĩmũtũ* ni ‘lĩu ũtemũvye nesa’ au chakula ambachi hakijaiva vizuri. Maana ya zamani imepotea. Kuna upanuzi wa maana kwa kuwa nomino *lĩũ* ina maana ya jumla. Usambaratikaji wa maana unaonekana kwa kuwa watoto wamesema hiki ni chakula kibaya.

B2

***Mũkate-*** Nomino hii inapatikana katika B2 ikitumiwa badala ya nomino ya zamani *kĩmũtũ* kwa maana hiyo ya zamani. Wazee wote (100%) walieleza kwamba maana yake ni chakula kilichookwa kwa unga ngano au mkate kwa Kiswahili.

B1

***Manzĩ-*** Wazee walisema kuwa nomino hii ilikuwa na maana mbili. Wote (100%) walikubaliana kwamba maana moja ni kiowevu kinywewacho ili kukata kiu kiitwacho ‘maji’ katika lugha ya Kiswahili. Watano (5) kati yao ambao ni asilimia hamsini (50%) walitaja maana ya pili ‘kiowevu chenye mbegu za uzazi za wanaume’. Katika Kiswahili ni shahawa.

B2

***Kĩw’ũ-*** Nomino hii imetumiwa katika B2 badala ya nomino *manzĩ.* Wazee walitupatia maana moja. Wote (100%) walisema kwamba maana yake ni kiowevu kitokacho mitoni, baharini, visimani na kwingineko ambacho hunywewa na kutumiwa nyumbani.

B1

***Mata-*** Hii ni nomino ya wingi inayobaki vile vile katika umoja na wingi. Maana mbili zilibainika kutokana na mahojiano ya wazee. Asilimia themanini (80%) ya wazee ilisema maana yake ni zana ya vita ya kurushia mishale. Aidha, walitaja nomino mbadala *ũta* ambayo inabeba dhana hiyo hiyo. Wazee wote (100%) walitoa maana ya pili ambayo ni ‘kiowevu kitokacho kinywani’. Katika Kiswahili ni ‘mate’.

B2

***Uta-*** Kuhusu nomino mbadala ***ũta*** wazee walitoa maana mbili; zana ya vita na mate membamba yajulikanayo kama ‘uderere’ kwa Kiswahili.

B1

***Mathatwa-*** Katika muktadha wa B1, nomino hii ilirejelea mifuko, hasa ya ngozi ya mnyama iliyotumiwa kuhifadhia mvinyo**.** Wazee wanane (8) walisema kwamba maana

yake ni ‘mifuko ya ngozi ya mnyama ambayo ilitumiwa kuhifadhia asali au mvinyo’. Wazee wawili (2) hawakujua maana ya nomino hii.

B2

***Ikuu-*** Nomino hii iliandikwa katika B2 badala ya nomino *ikuu*. Wazee wote aliohojiwa (100%) walisema maana yake ni ‘vyombo vya kuhifadhia viowevu, ambavyo huzaliwa na mmea unaotambaa’. Kwa Kiswahili ni ‘vibuyu’. Maana hii ilikuwa tofauti na ile ya *mathatwa* ya B1.

B1

***Mĩsyĩ-*** Wazee walitupatia maana mbili za nomino hii. Wote asilimia mia (100%) walisema kwamba *mĩsyĩ* ni zana za vita zilizoundwa kwa chembe na vijiti. Katika Kiswahili ni ‘mishale’. Wote kumi (10) pia, walisema maana ya sasa ya nomino hii ni njiti (vijiti) za kiberiti. Watoto walipoulizwa waeleze maana ya nomino hii, wote kumi (100%) walisema kuwa maana yake ni 'njiti za kiberiti'. Nomino hii imedondosha maana moja.

B2

***Maang**i*- Nomino mbadala iliyoandikwa katika B2 ni ***maangi.*** Wazee wote (100%) walisema kwamba maana yake ni zana za vita zilizoundwa kwa vijiti na chembe. Asilimia sitini yao (60%) ikasema maana ya pili ni ‘mbegu za kiume’.

B1

***Mwenyu-*** Nomino hii inapatikana katika B1 na wazee wote (100%) walithibitisha kwamba neno hili lilikuwa na maana moja. Lilitumiwa kurejelea mama likiwa na maana ya ‘mama yako’. Pia walisema kisawe cha *mwenyu* ni *inyia* (nyinyia). Watoto waliohojiwa walidhihirisha mtazamo hasi kuhusu nomino hii. Wote (100%) walisema

kuwa nomino hii ni ya matusi. Kila mmoja wao alisema nomino hii ni *kũumana* au kutukana. Walikiri kuwa hawaitumii katika mazungumzo yao. Maana asilia imepotea miongoni mwa watoto.

B2

***Inyia***- Nomino hii imetumia katika B2 kama nomino mbadala ya *mwenyu*. Wazee wote kumi (10) alisema kwamba hii ndiyo nomino inayotumiwa katika mazungumzo. Walibaini kwamba nomino hii hutumiwa kumrejelea mama wa mtu.

B1

***Mwĩai***- Katika B2, nomino hii ilirejelea Mungu (Mw.18:31) na mume (Mw.18:31). Wazee walitupatia maana hizi mbili na nyingine moja. Wazee wote (100%) walisema kuwa maana ya *mwĩai* ni Mungu. Saba (7) kati yao ambao ni asilimia sabini (70%) wakatupatia maana nyingine ‘mume’. Sita (6) kati yao (60%) walitoa maana ya tatu ‘mtu yeyote mwenye mamlaka’.

B2

***Mũtumĩa***- Wazee wote kumi (10) walisema kwamba maana ya nomino hii ni ‘mtu yeyote aliyezeeka, awe mwanamume au mwanamke’. Wanane (8) kati yao waliongezea maana ya pili; ‘mume wa mtu’. Maana hii ndiyo iliyopatikana katika muktadha wa B2. Kwa hivyo maana mbili zilipatikana.

B1

***Ndũa***- Maana asilia za nomino hii zilikuwa mbili, kwa mujibu wa uelewa wa wazee. Wote kumi (10) wakiwakilisha asilimia mia (100%) walisema maana ya nomino hii ni 'eneo dogo lenye watu wachache'. Kwa Kiswahili ni 'kijiji'. Wazee saba (7); asilimia

sabini (70%) kati yao wakatupatia maana ya pili, 'eneo kubwa lenye watu wengi'. Kwa Kiswahili ni 'mji' au 'jiji'. Kwa hivyo wazee walitupatia maana mbili kinzani.

B2

***Mũsyĩ-*** Nomino musyi inapatikana katika B2 ikichukua nafasi ya *ndũa* katika B1. Wazee wanane (8) walisema kwamba maana ya *mũsyĩ* ni 'sehemu ndogo katika jamii ambapo ni makao ya watu wa nasaba moja'. Sita (6) kati yao walisema kwamba maana ya nomino hii ni 'eneo kubwa lenye watu wengi na mijengo mikubwa mikubwa'. Kwa mfano *mũsyĩ wa Yelũsalemu* (Mji wa Yerusaleme) katika kitabu cha Luka mlango wa ishirini na mbili na mstari wa kumi (Lk.22:10). Katika Kiswahili ni mji au jiji. Watatu (3) walisema kwamba *mũsyĩ* pia ni 'watu ambao ni wa nyumba moja''ambao pia huitwa 'familia'. Kutokana na maelezo ya wazee nomino hii ilikuwa na maana tatu. Maana mbili zilizotajwa kwanza ndizo maana za nomino *ndũa* ya B1. Kwa hivyo nomino *mũsyĩ* ina maana mbili za nomino ya B1 *ndũa*, na maana nyingine tofauti.

B1

***Ukũngi-*** Nomino hii ilipatikana katika B1. Maana katika muktadha ilikuwa 'upepo mwanana'. Wazee wote (100%) walitueleza maana yake kuwa ni 'upepo mwanana unaovuma kwa kasi ya wastani'. Wazee hawakutupatia maana ya ziada.

B2

***Kiseve-*** Hii ni nomino iliyoandikwa katika B2 badala ya nomino *ũkũngi*. Maana yake kwa mujibu wa muktadha ilikuwa upepo unaovuma kwa kasi yoyote ile, ya chini, ya wastani au ya juu. Wazee wote (100%) walisema kwamba maana yake ni 'hewa inayovuma kwa kasi yoyote; ya chini, ya kati au ya juu'. Kwa Kiswahili ni upepo. Hatukupata maana ya ziada. Majibu ya wazee kuhusu maana za nomino yaliwekwa katika jedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.2: Maana ya nomino kwa mujibu wa wazee**

| Nomino B1 (15) | Maana | Asilimia (%) | Nomino B2 (15) | Maana | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Asa | Baba wa mtu | 60 | Ĩthe | Baba | 100 |
| | Mungu | 100 | | | |
| Ĩkanga | Mlinzi wa jela | 20 | Mũsikalĩ | Anayelinda usalama | 100 |
| | Anayelinda usalama; askari | 20 | | Mlinda lango | 30 |
| | Anayepakia abiria garini | 90 | | | |
| Ĩlawa | Chachu inayoumua unga | 80 | Mbota | Unga mweupe wa kuokea | 100 |
| | Hawakujua maana | 20 | | Kipodozi | 50 |
| Ĩmisi | Shuka nyeusi | 40 | Mbisũ | Chombo cha kupikia | 100 |
| | Hawakujua maana | 60 | | | |
| Isamũ | Mali | 100 | Syĩndũ | Mali | 90 |
| | Vitu vya aina yoyote | 60 | | Vitu vya aina yoyote | 80 |
| | Sehemu za siri | | | | |
| Ĩthweo | Wingu | 100 | Ĩtu | Wingu | 100 |
| | | | | Mbingu | 80 |
| Kĩmũtũ | Mkate uliochachushwa | 100 | Mũkate | Chakula cha unga ngano | 100 |
| Manzĩ | Maji | 100 | Kĩw’ũ | Kiowevu kitokacho mitoni, baharini n. k | 100 |
| | Maji yabebayo mbegu za uzazi | 50 | | | |
| Mata | Upinde | 80 | Ũta | Upinde | 10 |
| | Kiowevu kilicho kinywani | 100 | | Mate membamba | 50 |
| Mathatwa | Mifuko ya ngozi | 80 | Ikuu | Vibuyu | 100 |
| | Hawakujua maana | 20 | | | |
| Mĩsyĩ | Mishale | 100 | Maangi | Mishale | 100 |
| | Njiti za kiberiti | 100 | | Mbegu za uzazi | 60 |
| Mwenyu | Mama | 100 | Inyia | Mama | 100 |
| Mwĩai | Mungu | 100 | Mũtumĩa | Mtu yeyote aliyezeeka | 100 |
| | Mume | 70 | | Mume wa mtu | 80 |
| Ndũa | Mji au jiji | 100 | Mũsyĩ | Makao ya familia moja | 80 |
| | Eneo dogo; kijiji | 70 | | Mji au jiji | 60 |
| Ũkũngi | Upepo mwanana | 100 | Kĩseve | Upepo | 100 |

Jedwali linaeleza maana za nomino kwa mujibu wa wazee. Maana walizoeleza wazee kuhusu nomino za B1 na B2 zilithibitisha ukweli wa maana za muktadha. Hata hivyo, baadhi yao walionekana kutofahamu au kusahau maana za kimuktadha za baadhi ya nomino za B1. Nomino hizo ambazo baadhi ya wazee hawakufahamu maana ya kimuktadha ni *ĩkanga* (80%), *ĩlawa* (20%), *ĩmisi* (60%), *isamũ* (40%), *mata* (20%), *mathatwa* (20%) na *mwĩai* (30%). Idadi iliyo mabanoni ni ya wazee ambao hawakujua maana ya kimuktadha. Aidha, nomino kumi na moja (11) zilipata maana za ziada ambazo hazikujitokeza katika Biblia. Nomino hizo ni:

| Nomino | Maana ya ziada |
|---|---|
| *Ĩkanga* | Anayepakia abiria garini |
| *Isamũ* | Sehemu za siri |
| *Mbota* | Kipodozi |
| *Manzĩ* | Kiowevu kinachobeba mbegu za uzazi kwa wanaume |
| *Ũta* | Mate membamba |
| *Mĩsyĩ* | Njiti za kiberiti |
| *Maangi* | Mbegu za uzazi (sitiari) |
| *Mũsyĩ* | Eneo dogo wanamoishi watu wa nasaba moja, watu wa familia moja |
| *Mũtumĩa* | Mtu wa jinsia yoyote ambaye amezeeka |
| *Mwĩai* | Mtu mwenye mamlaka |
| *Ndũa* | Eneo dogo wanamoishi watu; kijiji |

### 4.1.1.3 Maana ya Nomino kwa mujibu wa watoto

Watoto kumi (10) walihojiwa ili kubaini iwapo walizifahamu maana za nomino kama zilivyotokea katika Biblia na kama wazee walivyoeleza. Majibu ya watoto ndiyo yaliyotupatia taswira kamili ya hali ya lugha ya Kikamba katika karne hii ya ishirini na moja (21). Nomino thelethini (30) ziliandikwa ubaoni, kumi na tano (15) kutoka B1 na

kumi na tano (15) kutoka B2. Watoto waliulizwa kueleza maana za nomino hizo na visawe kama walivyoelewa wao. Ilibainika kwamba baadhi ya maana zilipotoshwa. Mhimili uliosaidia kufahamu hayo ni wa nadharia ya dhana. Mhimili huo unafafanua kwamba maana inayojengwa hutegemea zaidi ukomo wa fikra za msikilizaji au mzungumzaji. Kwa hivyo utofauti katika uwezo wa kujenga dhana akilini kuhusu leksimu fulani unaweza kupunguza au kubadili maana ya kitu kinachojengewa dhana. Haya ndiyo yaliyodhihirika:

B1

***Asa-*** Nomino *asa* ilikuwa na maana mbili; 'Mungu' na 'mzazi wa kiume wa mtu'. Watoto wote (100%) walisema kwamba maana ya nomino *asa* ni 'Mungu'. Maana hii ni miongoni mwa maana asilia. Hawakuitambua maana ya pili. Nomino hii ilidondosha maana moja.

B2

***Ithe-*** Nomino hii ilikuwa na maana moja kwa mujibu wa muktadha na maelezo ya wazee; mzazi wa kiume wa mtu**.** Watoto watano (5) ambao ni asilimia hamsini (50%) walisema kwamba maana ya nomino *ĩthe* ni *mũsyai mũndũũme*. Maana yake ni 'mzazi mwanaume'. Wanne (4) ambao ni asilimia arubaini (40%) walisema kuwa kisawe cha nomino *ĩthe* ni *tata*. Nomino *tata* ina maana ya mzazi wa kiume. Mmoja (10%) alitoa kisawe kingine *nau* chenye maana 'mzazi wa kiume'. Kwa hivyo maoni ya watoto wote (100%) ni kuwa nomino hii ilikuwa na maana ya 'mzazi wa kiume' ambaye huitwa 'baba'. Nomino *ĩthe* imebeba maana moja ambayo ilidondoshwa na nomino *asa* katika B1.

B1

***Ĩkanga***- Maana za nomino hii zilikuwa tatu. Maana hizo ni 'mlinzi wa jela', 'askari/ mtu anayelinda usalama' na 'mtu anayepakia abiria garini'. Watoto waliohojiwa walikosa kutambua maana mbili za nomino hii; mtu anayelinda usalama au askari na mlinzi wa jela. Watoto sita (6) ambao ni asilimia sitini (60%) walisema maana ya nomino *ĩkanga* ni 'mtu anayepakia abiria garini na kukusanya nauli'. Kisawe walichojua ni *kondakita,* neno lililotoholewa kutoka Kiingereza 'conductor'. Hii ni maana moja kati ya zile asilia tulizopewa na wazee. Wanne (4) kati yao hawakujua maana ya nomino hii. Kwa mujibu wa watoto, nomino hii ilikuwa na maana moja.

B2

***Mũsikalĩ-*** Nomino hii ilikuwa na maana mbili; 'mtu anayelinda usalama wa nchi' na **'**mlinda lango'. Watoto watatu (3) ambao ni asilimia thelathini (30%) walisema kuwa maana ya *mũsikalĩ* ni *volisi* (polisi). Wanne (40%) walieleza maana kwa kutumia jina la Kiswahili 'askari' na watatu (30%) wakasema maana ya nomino hii ni *mũndũ wĩthwaa na ĩvuti* (mtu mwenye bunduki). Kwa mujibu wa watoto wote (100%) *mũsikalĩ* ni mtu yeyote alindaye usalama kwa mfano askari wa magereza, askari polisi na mwanajeshi. Maana iliyotolewa na watoto ni mojawapo ya maana tulizopata kutoka kwa wazee. Nomino *mũsikalĩ* ilidondosha maana moja ikabaki na moja.

B1

***Ĩlawa***- Maana asilia ya nomino hii ni 'chachu itokanayo na kuvu hai ambayo huchachusha na kuumua unga'. Majibu ya watoto yalileta maoni tofauti. Watoto wanne (4) ambao ni asilimia arubaini (40%) walisema kuwa nomino *ĩlawa* ilimaanisha 'mashua' katika Kiswahili. Kisawe chake wakasema ni *ĩsiwa*. Watoto wawili (2), asilimia ishirini (20%) wakasema *ĩlawa* ni 'ngalawa' katika lugha ya Kiswahili.

Nomino hii katika Kikamba ni *ngalawa* pia. Watoto wanne (4), asilimia arubaini (40%) hawakujua maana. Kutokana na uchanganuzi huu, Watoto hawakutaja maana ya nomino hii.

Ilibainika kwamba maana ambazo watoto waliandika zilikuwa zimepotoshwa. Nomino mbili (2) *ĩlawa* na *ngalawa* zinakaribiana kimatamshi na kiumbo ndiyo maana watoto walichagua maana hiyo. Waliosema kwamba maana ya *ĩlawa* ni 'mashua' walikuwa na dhana ya 'ngalawa' akilini. Kisha kwa kuwa ngalawa na mashua ni vyombo vya majini wakasema *ĩlawa* ni 'mashua'. Mimi kama mtafiti mkamba mwenye dhana za Kikamba akilini sikukubaliana na maana walizotoa watoto kuhusu nomino *ĩlawa*. Majibu ya watoto yalibaini kwamba nomino hii imetoweka katika mazingira ya watoto hawa, na walichofanya hapa ni kupotosha maana.

B2

***Mbota***- Maana mbili za nomino hii zilibainika baada ya usomaji wa B1 na mahojiano ya wazee. Maana hizo ni 'kitu kama unga mweupe kinachotumiwa katika uokaji ili kuumua unga', na 'aina ya kipodozi'. Watoto walitupatia maana mbili za nomino hii. Watoto watano (5) asilimia hamsini (50%) walisema kuwa maana ya *mbota* ni kitu kama unga kinachotiwa ndani ya unga wa kuokea. Watano (50%) nao wakasema maana ya nomino hii ni kitu cha kujipodoa. Maana zote zilikuwa sawa na za wazee.

B1

***Imisi-*** Maana asilia ya nomino hii ni 'shuka nyeusi iliyotumiwa na wanawake kusetiri au kufunika vitu'. Watoto walipoambiwa wataje maana ya nomino hii, watatu (3) walisema maana yake ni 'vazi la ndani ambalo huvaliwa na wanawake'. Kisawe walichotaja ni *kamisi* (kamisi/shimizi). Watatu wao (3) walisema kuwa maana ya *ĩmisi* ni 'kamisi kubwa'. Kwa hivyo asilimia sitini (60%) ya watoto ilikuwa na dhana 'vazi

la ndani la wanawake’. Watoto wanne (4) hawakutoa jibu lolote. Ilidhihirika kwamba maana ya nomino hii haikueleweka na ilipotoshwa. Shuka inayorejelewa haipo tena katika jamii na matumizi yake yamepitwa na wakati. Watu sasa wana makabati na mashubaka ya kuhifadhia bidhaa. Aidha, nyumba za sasa zina vyumba kadhaa ambavyo huwapa wakazi faragha. Usasa uliopo umefanya maana ya nomino hii kupotea katika mazungumzo na maandishi ya kisasa.

B2

***Mbisũ-*** Maana asilia ya nomino hii ilikuwa moja; kifaa cha mfinyanzi cha kupikia. Watoto wote (100%) walikubaliana na maana hiyo asilia kwa kusema kuwa maana ya nomino *mbisũ* ni 'chombo cha kupikia'.

B1

***Isamũ-*** Nomino hii ilikuwa na maana tatu; vitu vya aina yoyote, mali anayomiliki mtu na sehemu za siri. Majibu ya watoto yalibainisha kusambaratika kwa maana. Watoto wanane (8) ambao ni asilimia themanini (80%) walishindwa kuandika maana wala kisawe cha nomino hii. Wawili (2), asilimia ishirini (20%) waliandika maana iliyoandikwa na wazee ‘sehemu za siri’. Maana mbili asilia za nomino hii zimedondoka na ile iliyobaki haitumiwi kwa kuwa inarejelea sehemu za siri ambazo ni mwiko kuzitaja. Sehemu nyeti (za siri) ambazo ni mwiko kuzitaja katika jamii ya Wakamba zilipewa jina *isamũ* (vitu). Sasa ni vigumu sana neno hili kutumiwa katika mazungumzo ya kawaida na wala halipo katika vitabu vilivyoandikwa au kuchapishwa karne hii ya 21.

B2

***Syĩndũ-*** Tulipata maana mbili za nomino hii baada ya kuwahoji wazee. Maana moja ni 'mali aliyo nayo mtu' na maana ya pili ni 'vitu vya aina yoyote'. Watoto wote waliohojiwa (100%) walikubaliana na wazee kuhusu maana moja; 'bidhaa au vitu vya aina yoyote'. ilibainika kwamba nomino hii ilichukua mahali pa nomino *isamũ* ambayo ilipata maana hasi kutokana na kuhusishwa na sehemu za siri au za uzazi. Watoto hawakutaja maana 'vitu vya thamani alivyo navyo mtu'. Maana moja ya nomino hii ilidondoshwa.

B1

***Ithweo-*** Maana asilia ya nomino hii ilikuwa 'mkusanyiko wa matone ya mvua katika angahewa (atmosphere)'. Katika Kiswahili ni 'wingu'. Watoto wote kumi (10) ambao ni asilimia mia moja (100%) hawakujua maana ya nomino hii. Ilibainika kuwa nomino hii haikuwapo katika hazina ya msamiati wa watoto.

B2

***Ĩtu-*** Nomino hii ilitumiwa katika B1 badala ya nomino *ĩthweo*. Ilikuwa na maana mbili; mkusanyiko wa matone ya maji katika angahewa, na mahali juu sana ambapo huaminika kuwa ni makao ya Mungu. Watoto wote (100%) walifahamu maana ya nomino hii na wakasema ni 'wingu'. Wawili (2) kati yao waliitaja maana ya pili 'mahali Mungu hukaa'. Maana walizotaja watoto ndizo zilizopatikana katika muktadha na katika majibu ya wazee.

B1

***Kĩmũtũ-*** Maana asilia ya nomino hii ni 'mkate uliookwa kwa unga uliochachushwa'. Maana mbili zilijitokeza kutokana na uchanganuzi wa majibu ya watoto. Wawili (2)

wakiwakilisha asilimia ishirini (20%) walitoa maana ya jumla kwamba *kĩmũtũ* ni *lĩũ* au chakula. Wengineo wanane (8), yaani asilimia themanini (80%) waliandika kwamba *kĩmũtũ* ni 'lĩũ ũtemũvye nesa' au chakula ambacho hakijaiva vizuri. Maana ya asilia ilitoweka. Tulishuhudia upanuzi wa maana kwa kuwa nomino *lĩũ* ina maana ya jumla. Pia usambaratikaji wa maana ulitokea kwa kuwa watoto walisema hiki ni 'chakula ambacho hakijaiva vizuri'.

B2

***Mũkate-*** Nomino hii ilitumiwa katika B2 kurejelea aina ya chakula kilichookwa kwa kutumia unga wa ngano. Watoto wote (100%) walikubaliana na wazee kwa kusema kwamba *mũkate* ni chakula kilichookwa kwa unga wa ngano. Maana ya nomino hii ilifahamika miongoni mwa watoto.

B1

***Manzĩ-*** Nomino hii ilikuwa na maana mbili. Maana moja ni kiowevu kinywewacho kukata kiu ambacho katika Kiswahili ni maji. Maana ya pili ni kiowevu kinachobeba mbegu za uzazi kwa wanaume. Katika Kiswahili ni shahawa. Watoto wote kumi (10) hawakusema maana wala kisawe cha nomino hii. Ilibainika kwamba haikuwa katika hazina ya msamiati ambao watoto hawa walitumia katika mazungumzo. Maana moja ya nomino hii ilihusishwa na sehemu za uzazi na hivyo ikasababisha kusambaratika kwa maana ya nomino *manzĩ*.

B2

***Kĩw'ũ-*** Maana asilia ya nomino hii ni kiowevu kinachopatikana mitoni, baharini na sehemu nyinginezo kama hizo na ambacho hunywewa ili kukata kiu. Watoto walipohojiwa, wote (100%) walikubaliana na maana hiyo ya wazee. Wote kumi

walisema kwamba *kĩwũ* ni *kĩla kĩnyusawa mũndũ ayĩw'a waũni* (kinachonywewa na mtu anapoona kiu). Maana hii ni mojawapo ya maana za nomino ya zamani *manzĩ.*

B1

***Mata-*** Nomino hii ilikuwa na maana mbili. Maana ya kwanza ni 'zana ya vita inayotumiwa kurushia mishale'. Katika Kiswahili ni upinde au uta. Maana ya pili ni 'kiowevu kitokacho kinywani kiitwacho 'mate' kwa Kiswahili. Asilimia sabini (70%) ya watoto iliandika kwa lugha ya Kiswahili 'mate'. Watatu (30%) waliandika maana ya neno hilo *kĩndũ kĩĩlye kĩw'ũ kanywanĩ* (kitu mfano wa maji kinachokuwa kinywani). Kwa hivyo watoto wote (100%) walitoa maana sawa ya nomino hii ambayo ni 'kiowevu kilicho kinywani'. Hii ni mojawapo ya maana tulizopewa na wazee. Maana ya pili ya nomino *mata* haikujulikana miongoni mwa watoto. Kwa hivyo maana moja ilidondoka nomino ikabaki na maana moja.

B2

***Ũta-*** Nomino *ũta* ilitumiwa kurejelea 'zana ya vita ya kurushia mishale'. Maana hii ilikuwa maana mojawapo ya maana za nomino mata. Maana ya pili ilikuwa 'mate membamba yatokayo kinywani hasa mtu anapolala'. Watoto wote (100) waliifahamu maana yake kama 'zana ya vita' ambayo katika Kiswahili ni 'upinde'. Hakuna aliyetaja maana ya pili ya nomino hii. Nomino hii pia ilidondosha maana moja.

B1

***Mathatwa-*** Maana asilia ya nomino hii ilikuwa mfuko wa ngozi uliotumiwa kuhifadhia asaliWatoto walipoulizwa kutaja maana ya nomino hii, wote (100%) walishindwa kueleza maana. Msamiati huu umetoweka miongoni mwa watoto waliohojiwa.

B2

***Ikuu-*** Nomino *ikuu* ilikuwa na maana moja; vyombo vinavyotumiwa kuhifadhia viowevu ambavyo ni zao la mmea unaotambaa. Watoto watano (5) walisema maana yake ni 'vitu vinavyotumiwa kuhifadhia viowevu kama vile maji'. Katika Kiswahili ni 'vibuyu'. Watoto watano (5) hawakujua maana. Katika mahojiano hayo, ilibainika kuwa kutokana na usasa uliopo, vibuyu (ikuu) hupatikana katika familia chache Ukambani. Watu hutumia vyombo vya plastiki kama vile mitungi na matangi kuhifadhia maji na viowevu vingine.

B1

**Mĩsyĩ-** Nomino hii ilikuwa na maana mbili. Maana moja ni 'zana za vita zilizoundwa kwa chembe na vijiti'. Kwa Kiswahili ni 'mishale'. Maana nyingine ni 'njiti za kiberiti'. Watoto walipoulizwa waeleze maana ya nomino hii, wote kumi (100%) walisema kuwa maana yake ni 'njiti za kiberiti'. Nomino hii imedondosha maana moja.

B2

***Maangi-*** Nomino hii ilikuwa na maana mbili. Maana moja ni zana za vita ambazo zimeundwa kwa chembe na vijiti au mishale. Maana ya pili ambayo ni ya kitasfida ni mbegu za kiume za uzazi. Watoto saba (70%) walijua maana moja. Walisema kuwa maana yake ni *syĩndũ sya kũãtha* au vitu vya kufumia. Walikuwa wakirejelea mishale. Watatu (30%) hawakujibu. Maana ya pili ya nomino hii ambayo ni ya kitasfida haipo katika msamiati wa watoto.

B1

***Mwenyu-*** Maana asilia ya nomino hii ni 'mama'**.** Watoto waliohojiwa walidhihirisha mtazamo hasi kuhusu nomino hii. Watoto tisa (9) walisema kwamba hayo yalikuwa ni matusi. Mtoto mmoja (1) hakujibu. Maana asilia haikupatikana miongoni mwa watoto.

B2

***Inyia-*** Maana asilia ya nomino hii ni ‘mama’ na ndiyo iliyotumiwa katika B2 badala ya *mwenyu*. Watoto watano (5) walisema nomino *inyia* ilimaanisha ‘mum’. Hili ni neno la Kiingereza linalotumiwa kurejelea mama. Wanne walitupatia nomino nyingine iliyotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza ‘mami’ wakasema ndiyo maana ya *inyia*. Mtoto mmoja alisema kwamba inyia ni *mũsyai mũndũ mũka* au mzazi wa kike. Watoto wote walifahamu maana ya nomino hii kwa kuwa walirejelea mzazi wa kike ingawa maelezo yao yalikuwa tofauti. Idadi iliyofahamu maana ikiwa asilimia mia (100%), tuligundua kwamba nomino hii ilikuwa katika msamiati wao wa mazungumzo.

B1

***Mwĩai-*** Nomino *mwĩai* ilikuwa na maana tatu; mungu, mume na mtu mwenye mamlaka. Watoto wote (100%) walisema kuwa maana ya nomino *mwĩai* ni 'Mungu'. Maana hii ni miongoni mwa maana tatu ambazo wazee walitupatia. Kwa hivyo watoto walifahamu maana moja.

B2

***Mũtumĩa-*** Nomino hii ilikuwa na maana mbili. Maana ya kwanza ilikuwa ‘mtu wa jinsia yoyote ambaye amezeeka’. Maana ya pili ilikuwa ‘mume’. Watoto wote (100%) walisema maana ya nomino hii ni ‘mwanamume aliyezeeka’. Kutokana na maana asilia nomino hii imedondosha maana moja. Aidha, maana ya kwanza ‘mtu wa jinsia yoyote ambaye amezeeka’ ambayo ilikuwa pana ilibanwa.

B1

***Ndũa-*** Maana mbili kinzani zilipatikana baada ya kuangalia muktadha na kuwahoji wazee. Maana moja ilikuwa 'eneo kubwa lenye wakazi wengi na mijengo mikubwa' na

maana ya pili ilikuwa 'eneo dogo lenye wakazi wachache na mijengo midogo midogo'. Maana hizi zilirejelea 'mji' na 'kijiji' mtawalia. Watoto wanane (80%) walitoa jibu tofauti. Walisema kwamba maana ya *ndũa* nĩ *vala andũ mekalaa* 'ushago' kumaanisha 'wanapoishi watu mashambani'. 'Ushago' ni neno la lugha ya sheng' lenye maana 'mashambani'. Mashambani ni vijijini wala si mjini. Kwa hivyo maana hii ilikuwa miongoni mwa maana ambazo wazee walitaja. Wawili (20%) hawakujibu. Maana moja ilidondoshwa, neno likawa lina maana moja.

B2

***Mũsyĩ-*** Nomino hii ilirejelea dhana tatu kwa mujibu wa wazee na pia muktadha. Dhana ya kwanza ilikuwa mji, ya pili mahali wanamoishi watu wa aila moja na tatu familia au watu wa familia moja. Watoto watano (5) walisema maana yake ni mahali wanapoishi watu. Watatu (3) walisema kwamba ni mahali wanapoishi wazazi na watoto wao. Wawili (2) walijibu kwamba *mũsyĩ* ni 'nyumbani'. Maoni ya watoto wote (100%) yalikuwa kwamba *mũsyĩ* ni taasisi ndogo zaidi katika jamii ambamo watu wa nasaba moja huishi. Maana iliyofahamika miongoni mwa watoto ni moja na ilikuwa miongoni mwa maana asilia zilizotajwa na wazee. Nomino *mũsyĩ* ilidondosha maana mbili.

B1

***Ukũngi-*** Maana asilia ya nomino hii ni upepo mwanana unaovuma kwa kasi ya chini. Watoto walitoa majibu tofauti na wazee. Wawili (20%) walitoa maana ya jumla wakasema maana ya *ũkũngi* ni *kĩseve* au kwa Kiswahili 'upepo'. Mtoto mmoja (1) akiwakilisha asilimia kumi (10%) alisema kwamba maana ya nomino hii ni 'uchafu unaotolewa kwenye nafaka kama vile mahindi'. Katika Kiswahili ni 'makapi'. Watoto saba (70%) hawakujua maana. Ilibainika kuwa maana asilia ya nomino *ũkũngi* inafifia kwa kuwa ilijulikana miongoni mwa asilimia ishirini (20%) pekee.

B2

***Kĩseve-*** Nomino hii ilikuwa na maana moja**;** hewa inayovuma kwa kasi yoyote. Kwa Kiswahili ni upepo. Asilimia mia (100%) ya watoto walikubaliana na maana hiyo. Kwa hivyo ilikuwa katika msamiati wa watoto. Muhtasari wa majibu ya watoto kwa nomino zote (B1 na B2) umewekwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.3: Maana ya Nomino kwa mujibu wa watoto**

| Nomino | Kisawe | Asilimia (%) | Maana na maelezo |
|---|---|---|---|
| Asa | Ngai | 100 | Mungu |
| Ĩthe | Mũsyai mũndũũme | 50 | Mzazi mwanaume |
| | Tata | 40 | Baba |
| | Nau | 10 | Baba |
| Ĩkanga | Kondakita | 60 | Anayepakia abiria na kukusanya nauli |
| | - | 40 | Hawakujua maana |
| Mũsikalĩ | Volisi | 30 | Askari polisi |
| | - | 40 | Askari |
| | Mũndũ wĩthwaa na ĩvuti | 30 | Mtu mwenye bunduki |
| Ĩlawa | Ĩsiwa | 40 | Mashua |
| | Ngalawa | 20 | Ngalawa |
| | - | 40 | Hawakujua maana |
| Mbota | Kamũtu keũ ka kwĩkĩa nganũnĩ | 50 | Kitu kama unga cha uokaji |
| | Kĩndũ kya kwĩvaka | 50 | Kipodozi |
| Ĩmisi | Kamisi | 30 | Kamisi |
| | Kamisi kanene | 30 | Kamisi kubwa |
| | Ngũa | 20 | Nguo |
| | - | 20 | Hawakujua maana |
| Mbisũ | Kĩndũ kiũ kya kũuĩa | 100 | Chombo (cheusi) cha kupikia |
| Isamũ | - | 80 | Hawakujua maana |
| | - | 20 | Sehemu za siri |
| Syĩndũ | - | 100 | Bidhaa au vitu vya aina yoyote. |
| Ĩthweo | - | 100 | Hawakujua maana |
| Ĩtu | - | 100 | Wingu |
| | | 20 | Mahali anapokaa Mungu |
| Kĩmũtũ | Lĩu | 20 | Chakula |
| | Lĩu ũtemũvye nesa | 80 | Chakula ambacho hakijaiva vizuri |
| Mũkate | Lĩu ũuĩtwe na mũtu wa nganũ | 100 | chakula kilichookwa kwa ngano |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Manzĩ | - | 100 | Hawakujua maana |
| Kĩw’ũ | Kĩla kĩnyusawa uyĩwa’ waũni | 100 | Kinachonywewa kukata kiu; Maji |
| Mata | ‘Mate’ | 70 | Mate |
| | Kĩndũ kĩilye kĩw'ũ kanywanĩ | 30 | Kitu mfano wa maji kinywani |
| Ũta | | 100 | Zana ya vita; Upinde |
| Mathatwa | - | 100 | Hawakujua maana |
| Ikuu | | 50<br>50 | Vyombo vya kuhifadhia viowevu<br>Hawakujua maana |
| Mĩsyĩ | Mĩtĩ ya kĩlĩvĩtĩ | 100 | Njiti za kiberiti |
| Maangi | Syindũ sya kũatha | 70 | Vitu vya kufumia/ mishale |
| | - | 30 | Hawakujua maana |
| Mwenyu | Kũumana | 90 | Matusi ya kumtukana mtu |
| | - | 10 | Hakujibu |
| Inyia | Mũsyai wa mũndũ mũka | 10 | Mzazi wa kike |
| | Mami | 40 | Mama |
| | Mum | 50 | Mama |
| Mwĩai | Ngai | 100 | Mungu |
| Mũtumĩa | Mũndũũme mũkũũ | 100 | Mwanamume mzee |
| Ndũa | Vala andũ mekalaa ‘ushago’ | 80 | Wanapoishi watu mashambani , kijiji |
| | - | 20 | Hawakujibu |
| Mũsyĩ | Vala andũ mekalaa | 50 | Mahali wanapoishi watu |
| | Vala syana na asyai mekalaa | 30 | Wanapoishi wazazi na watoto |
| | | 20 | Nyumbani |
| Ũkũngi | Kĩseve | 20 | Upepo |
| | Mavuti ma mbemba | 10 | Makapi |
| | | 70 | Hawakujibu |
| Kĩseve | | 100 | Upepo |

Kutokana na usaili wa watoto kuhusu nomino, tuligundua mambo yafuatayo:

i. Nomino za B1 ambazo hazikufahamika maana na watoto ni nane (8); *ĩthweo*, *ĩmisi*, *kĩmũtũ*, *manzĩ*, *mathatwa*, *mwenyu*, *ũkũngi* na *ĩlawa*. Hii ni asilimia hamsini na tatu (53%) ya nomino kumi na tano za B1.

ii. Nomino za B1 ambazo watoto walifahamu maana moja kati ya maana asilia au maana tofauti ni saba (7); *asa*, *ĩkanga*, *isamũ*, *mata*, *mĩsyĩ*, *mwĩai* na *ndũa*. Hii ni asilimia arubaini na saba (47 %).

iii. Nomino za B2 ambazo zilikuwa na maana tofauti na nomino za B1 ni tano (5); *mbisũ, ikuu, mũtumĩa na ndũa.* Idadi hii ni asilimia ishirini na saba (27%).

iv. Nomino za B2 ambazo watoto walifahamu maana zake ni kumi na tano (15). Hii ni asilimia mia moja (100%).

v. Nomino za B2 ambazo zimebadilika maana kwa mujibu wa maelezo ya watoto ni saba (7); *syĩndũ, kĩw'ũ, ũta, maangi, mũsikalĩ, mũtumĩa* na *ndũa*. Baadhi ya nomino hizi zimedondosha maana moja asilia, nyingine zikapata maana ya ziada na moja ikapata maana tofauti. Hii ni asilimia arubaini na saba (46%) ya nomino zote kumi na tano (15) za B2.

Kwa kukosekana kwa asilimia sabini na tatu (73%) ya nomino za B1 katika matini ya B2, tulidhani watoto hawakufahamu maana ya nomino yoyote katika B1. Utafiti ulibainisha vingine huku watoto wakifahamu maana moja moja asilia ya nomino saba (7) kwa kumi na tano (15) za B1 (47%).

Utafiti huu ulichunguza nomino thelathini (30) zilizobadilika maana. Kumi na tano (15) zilitolewa katika B1 na kumi na tano (15) zilitolewa katika B2. Maana za nomino zilichunguzwa kwa kuzingatia vigezo vitatu: muktadha, maana kwa mujibu wa wazee na maana kwa mujibu wa watoto. Nomino tulizojadili ziliakisi kategoria za nomino ambazo tulieleza katika sehemu ya 4.1.1 tukitumia ufafanuzi wa *Kamusi Sanifu ya Kiswahili* (2016). Nomino hizi tuliziweka katika kategoria hizi kwa kutegemea uelewa wa mtafiti kuhusu maana za nomino hizo.

Nomino *manzĩ*, *mata*, *ũta*, *kĩw'u* na *mbota* zilikuwa nomino za wingi. Idadi hii ilikuwa asilimia kumi na saba (17%). Nomino za wingi ni nomino ambazo hutaja vitu vinavyopatikana katika hali ya wingi tu. Nomino dhahania zilikuwa tatu: *Asa*, *Mwiai* na *ĩtu*. Nomino hizi zilirejelea vitu ambavyo haviwezi kuguswa wala kuonekana. Idadi ya nomino dhahania ilikuwa asilimia kumi (10%) ya nomino thelathini (30). Nomino zote zilizoteuliwa zilikuwa za mguso ila nomino Asa (Mungu), Mwiai (Mungu) na *ĩtu* (wingu) ambazo ni nomino dhahania. Nomino mguso ni nomino ambazo zinaweza kuguswa na kuonekana. Kwa hivyo idadi ya nomino mguso katika utafiti huu ilikuwa asilimia tisini (90%). Aidha, nomino zote zinaingia katika kategoria ya nomino za kawaida ila nomino *Asa* (Mungu) na *Mwĩai* (Mungu). Nomino za kawaida ni zile zinazorejelea viumbe, vitu na hali. Idadi ya nomino za kawaida zilizochunguzwa ilikuwa asilimia tisini na tatu (93%).

### 4.1.2 Kundi la Vitenzi katika Biblia

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2016), kitenzi ni neno ambalo huarifu tendo linalofanyika. Katika sentensi, kitenzi huwa elekezi au sielekezi. Akifafanua kuhusu vitenzi vya Kiswahili, Mohammed (2001) anasema kwamba kitenzi cha Kiswahili kina sehemu tatu: kiambishi awali, mzizi na kiambishi tamati. Mzizi wa kitenzi ni sehemu ya shina ambayo haina viambishi au haijaambishwa. Ni sehemu ya kitenzi ambayo haiwezi kupunguzwa zaidi kimofolojia. Mzizi wa kitenzi ndio unaobeba maana ya kileksia ya kitenzi. Mzizi huo unapoongezewa viambishi vyake, tunapata shina la kitenzi. Katika lugha ya Kiswahili, shina la kitenzi huisha na *–a* isipokuwa kwa maneno mkopo. Kwa mfano *cheza*, *pika* na *kula*. Vitenzi *shukuru*, *fasiri* na *samehe* ni mfano wa vitenzi vilivyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Matinde (2012) anaeleza kwamba kitenzi ni neno linalotoa taarifa kuhusu tendo linalofanyika, lililofanyika na litakalofanyika. Akifafanua maana ya kiarifu, Habwe na Karanja (2007)

wanasema kuwa katika sehemu ya kiarifu ndipo kitenzi kikuu huwa. Kiarifu ni sehemu ya sentensi ambayo inatoa taarifa kuhusu kiima. Kwa mujibu wa maelezo haya tunaweza kusema kuwa kitenzi ni sehemu muhimu ya kiarifu inayotoa taarifa kuhusu kinachotendwa na kiima. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2016) inatoa aina tano za vitenzi; kitenzi halisi, kitenzi kikuu, kitenzi kisaidizi, kitenzi kishirikishi na vitenzi sambamba.

Kitenzi halisi huonesha tendo halisi katika sentensi na hutokea peke yake katika sentensi. Kwa mfano:

i) Mtoto anasoma.
ii) Mwashi amefika.

Mifano ya vitenzi halisi katika Kikamba ni:

i) *Mũĩmi nĩwavika* (Mkulima amefika).
ii) *Kĩw'ũ nĩkyathela* (Maji yameisha).

Kitenzi kikuu ni kitenzi kinachowasilisha tendo lenyewe katika muktadha wa sentensi yenye vitenzi viwili. Kwa mfano:

i) Mwalimu alikuwa akifundisha.
ii) Mtoto anaweza kutembea.

Katika lugha ya Kikamba, vitenzi vikuu vipo. Kwa mfano:

i) *Mwalimũ eĩthwa ayĩandĩka* (Mwalimu atakuwa akiandika).
ii) *Mwende nĩwĩsĩ kũvũa* (Mwende anajua kufua).

Kitenzi kisaidizi huandamana na kitenzi kikuu katika sentensi na hufafanua hali mbalimbali. Kwa mfano:

i) Mwalimu alikuwa akifundisha.

ii) Mtoto angali analala.

Mifano ya kitenzi kisaidizi katika lugha ya Kikamba ni:

i) *Mwana no ũkomete* (Mtoto angali analala).

ii) *Mũẽni nũkwenda kũthi* (Mgeni anataka kwenda).

Kitenzi kishirikishi huonesha hali katika sentensi bila kuonesha tendo halisi. Kwa mfano:

i) Ogutu ni mhariri.

ii) Ogutu alikuwa mhariri.

Katika Kikamba kuna vitenzi vya aina hii. Kwa mfano:

i) *Mwaka nĩ mwalimũ* (Mwaka ni mwalimu).

ii) *Kĩkombe kĩõ mesanĩ* (Kikombe kingali mezani).

iii) *Mwaka aĩ mwalimũ* (Mwaka alikuwa mwalimu).

Vitenzi sambamba ni vitenzi viwili au zaidi vinavyotumika kwa pamoja katika sentensi moja. Kwa mfano:

i) Ambani alikuwa angali anasoma.

ii) Furaha alikuwa anajua kupika.

Mifano ya kitenzi sambamba katika Kikamba ni kama vile:

i) *Mũũi nũkwenda kwambĩĩa kũũa* (Mpishi anataka kuanza kupika).

ii) *Mwini no waendee kwina* (Mwimbaji alikuwa angali akiimba).

Habwe na Karanja (2007) wanasema kwamba kuna vitenzi vya silabi moja pia. Hivi ni vitenzi ambavyo vimeundwa kwa silabi moja pekee. Ili kuleta maana kamili, huambatanishwa na kiambishi *ku* katika kauli ya kutenda. Maneno yaliyoorodheshwa

hapa chini ni mifano ya vitenzi vya silabi moja. Maneno yaliyo mabanoni ni tafsiri ya Kikamba ya vitenzi hivyo:

i) -la (ya)

ii) -cha (kya)

iii) -nywa (nywa)

iv) -fa (kw'a)

Uchanganuzi unaofuata unahusu vitenzi kama hivi. Vitenzi kumi (10) viliteuliwa kutoka B1 na vingine kumi (10) kutoka B2. Kisha maana ilichunguzwa kwa kuzingatia vigezo vitatu: muktadha wa matumizi, usaili wa wazee wa na usaili wa watoto. Uchanganuzi wa maana ya vitenzi kulingana na muktadha ni kama ifuatavyo:

### 4.1.2.1 Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa Muktadha

Nadharia ya Nyanja za Kisemantiki ilifaa katika uchanganuzi huu. Mhimili uliotumika katika uchanganuzi wa data ni usemi maarufu wa Firth (1951) ulionukuliwa na Prakasam na Abbi (2018) kwamba maana ya neno hujulikana kutokana na washirika wa neno hilo au maneno yanayolizunguka neno. Biblia mbili B1 na B2 zilitumiwa kutupatia muktadha wa matumizi ya vitenzi ishirini vilivyoteuliwa. Maana za vitenzi ziliangaliwa kulingana na jinsi vitenzi hivyo vilivyotumiwa katika Biblia. Aidha, tulichunguza iwapo maana za vitenzi vya B1 zilihusiana na maana za vitenzi vya B2 au zilikuwa tofauti. Ufuatao ni uchanganuzi wa maana za vitenzi kwa mujibu wa muktadha wa B1 na B2:

B1

***Kũka***- Maana ya kitenzi hiki kama kilivyotumiwa katika B1 ni 'kimbia'. Kitenzi hiki kimetumiwa pale ambapo wafalme wa mataifa mbalimbali walikuwa wakipigana vita,

kisha wafalme wa Sodoma na Gomora wakazidiwa nguvu na wenzao. Hayo yamenukuliwa hapa:

Kĩkamba: *Na asumbĩ ma Sotomo na Ngomola makũka maelete kĩĩmanĩ* (Mw.14:10).

Kiswahili: Na wafalme wa Sodoma na Gomora wakakimbia wakielekea mlimani.

Kiambishi awali -*ma* kilichoambishwa kitenzi *kũka* kinawakilisha nafsi ya pili wingi. Katika Kiswahili ni –*wa*. Biblia imeeleza kwamba baada ya kuona wanashindwa, wafalme hawa waliamua kukimbia wakielekea mlimani kujificha. Biblia ya Kikamba cha sasa B2 imetumia kitenzi kingine tofauti kurejelea dhana 'kimbia'.

B2

Sentensi inayofuata imenukuliwa katika B2 na inathibitisha matumizi ya kitenzi tofauti katika mazingira sawa ya Biblia:

Kikamba: Na yĩla asumbĩ ma Sotomu na Ngomola masembie makĩĩte kaũ…

Kiswahili: Wafalme wa Sodoma na Gomora walipokimbia wakihofia vita…

Katika sentensi hii, sehemu ya neno iliyopigiliwa mstari *semb*- ni mzizi wa kitenzi *semba*. Mzizi huu unapoongezewa viambishi tamati –*ie* tunapata dhana ya wakati uliopita, yaani wafalme waliotajwa walikimbia wakati huo. Kitenzi *kũka* hakipo katika B2 lakini kitenzi *semba* kimetumiwa mahali pake.

B1

***Kwatwa***- Maana ya kitenzi hiki katika muktadha wa Biblia ya Kikamba B1 ni 'kamatwa'. Baada ya kupata chajio cha mwisho, Yesu na mitume wake walienda shambani Gethsemane kusali. Hapo ndipo askari na makuhani walipomwendea baada

ya kuelekezwa na Judasi Iskarioti. Hayo yanaonekana katika kifungu kilichonukuliwa hapa.

Kikamba: *Namo mamuĩkwata, na mamuĩtongoesya...* (Lk. 22:54).

Kiswahili: Nao wakamkamata, na kumwongoza…

Maana ya kitenzi *kwatwa* hapa ni ‘kamatwa’ kama vile mhalifu afanyiwavyo. Hata hivyo, tunaona matumizi mengine ya kitenzi hiki ambapo maana yake si kukamatwa. Sentensi inayofuata imenukuliwa kutoka kitabu cha Mwanzo, katika B1:

Kikamba: …*na (Noa) anywa mbinyu akwatwa nĩyo* (Mw.9:21).

Kiswahili: ...na akanywa divai akalewa.

Maana ya pili ya *kwatwa* ni lewa. Maana hii ni maana ya kiistiari iliyotokana na maana asilia kwa kuwa pombe huteka nyara hisia na mawazo ya mtu, akakosa uhuru wake, akawa ni kama aliyekamatwa na polisi. Katika B2 maana moja ‘kamatwa’ ndiyo inayopatikana. Maana ya kiishara ‘lewa’ haipo tena.

B2

***Milwa-*** Dhana ya kulewa katika B2 inawakilishwa na kitenzi tofauti *milwa* kama inavyoonekana katika mfano huu:

Kikamba: …*(Noa) nĩwanywie ndivai amilwa, aumya ngũa syake*…(Mw.9:21).

Kiswahili: (Nuhu) alikunywa divai akalewa, akavua nguo zake...

***Milwa*** ndicho kitenzi badala kilichoandikwa katika Biblia ya Kikamba cha sasa B2. Kitenzi *kwatwa* kilikoma kutumiwa kiishara kuwakilisha dhana ya kulewa.

B1

***Meta***- Hiki ni kitenzi cha Kikamba cha kale chenye maana ‘huzunika’. Kitenzi hiki kimetumiwa katika B1 pale wafuasi wa Yohane walipomwendea Yesu wakimtaka kuwaeleza sababu ya mitume wake kutoshiriki mfungo. Yesu aliwajibu kwa mafumbo na kusema:

Kikamba: *Aeni matonya ata kũmeta o yĩla mũtwaani wĩvamwe nao?* (Mat.9:15)

Kiswahili: Wageni wanawezaje kuhuzunika wakati bwana harusi yu pamoja nao?

Yesu alimaanisha kwamba mitume wake walistahili kula, kunywa na kufurahi kwa kuwa bwana harusi (Yesu) alikuwa nao.

B2

***Ithĩwa na Kyeva***-Tukiangalia B2, kitenzi *meta* hakipo. Badala yake kauli *ĩthĩwa na kyeva* imetumiwa. Tuangalie muktadha wa matumizi katika B2:

Kikamba: *Aeni nĩmatonya kwĩthĩwa na kyeva yĩla mũtwaani wĩkatĩwoo?* (Mat.9:15)

Kiswahili: Wageni wanawezaje kuwa na huzuni wakati bwana harusi yu kati yao?

Ingawa vitenzi vilivyotumiwa katika muktadha wa B1 na B2 ni tofauti, maana iliyokusudiwa ni moja; kuhuzunika.

B1

***Tambũka***- Kitenzi *tambũka* kimetumiwa katika B1 kuashiria kitendo cha kutembea kwa miguu. Vitau kadhaa vimetumia kitenzi hiki lakini mfano wetu umenukuliwa kutoka kitabu cha *Mwanzo* sura ya tatu (3) mstari wa nane (8):

Kĩkamba: *Na meew'a wasya wa Yeova Ngai aitambũka mũũndanĩ*... (Mw.3:8)

Kiswahili: Wakasikia sauti ya Jehova Mungu aki<u>tembea</u> shambani...

Adamu na Hawa walikuwa wamekula tunda la mti wa kati kinyume na maagizo ya Mungu, kisha wakajificha. Ndipo Mungu alipokuwa akitembea shambani alikosa kuwaona kisha akawaita kuwajulia hali. Maandiko yanaeleza kwamba Mungu alizoea kutembea shambani humo. Kwa hivyo maana ya kitenzi *tambũka* katika muktadha huu ni 'tembea kwa miguu'.

B2

***Tembea***: Kitenzi hiki kinapatikana katika B2. Ndicho kilichoandikwa badala ya kitenzi *tambũka*. Maana ya kitenzi hiki inapatikana katika kitabu cha Mwanzo katika B2 katika maneno yaliyonukuliwa hapa chini:

Kikamba: *Na meew'a wasya wa Mwĩai Ngai ai<u>tembea</u> mũũndanĩ*…(Mw.3:8)

Kiswahili: Wakasikia sauti ya Bwana Mungu aki<u>tembea</u> shambani...

Kitenzi *tembea* katika B2 kimetumiwa katika muktadha ule wa matumizi ya kitenzi *tambũka* katika B1. Katika sentensi hizi mbili Mungu anawaita Adamu na Hawa akiwa katika matembezi yake shambani. Vitenzi hivi viwili vinamaanisha 'tembea kwa miguu'.

B1

***Thilĩka***- Kitenzi hiki kinapatikana katika kitabu cha *Mwanzo*, sura ya thelathini na moja (31) mstari wa thelathini na sita (36). Yakubu alikuwa ametoroka nyumbani kwa Labani mjomba wake, kisha Labani akamfuata mbio akimtuhumu kwa kubeba miungu wake. Akatafuta kwenye vifurushi alivyobeba Yakubu asipate kitu. Jambo hili lilimwudhi Yakubu sana. Hayo yamenukuliwa hapa chini:

Kikamba: Na Yakovo athilĩka mũno na amũkandĩa Lavani, Yakovo amwĩa Lavani, "Ĩvĩtyo yakwa nĩ yaũ?" (Mw.31:36).

Kiswahili: Yakubu aliudhika sana na akamkaripia Labani, akamwambia, "Kosa langu ni lipi?"

B2

***Thata***- Katika Biblia B2, kitenzi *thilĩka* hakipo. Badala yake kitenzi *thata* kimetumiwa. Sentensi ifuatayo imenukuliwa kutoka kitabu cha Mwanzo katika B2:

Kikamba: *Yakovo nĩwathatie na athũkĩa Lavani aimwĩa, "Nĩkĩte ĩvĩtyo yĩva*?" (Mw.31:36)

Kiswahili: Yakubu aliudhika akamgombeza Labani na kumwambia, "Nimetenda kosa gani?"

Kitenzi *thata* kina mzizi *that*- na kiishio au kiambishi tamati *a* kuleta maana ya kauli ya kutenda. Katika mfano ulionukuliwa katika kitabu cha *Mwanzo* (31:36) katika B2, mzizi *that*- umeongezewa kiambishi *–i* kinachoashiria wakati uliopita kisha kiishio *e*. Kwa hivyo kitenzi mbadala cha *thilĩka* ni *thata*.

B1

***Mumunya***- Kitenzi hiki kimetumiwa katika Biblia ya B1 kurejelea kitendo cha kumgusisha mtu midomo iliyobebeduliwa kama ishara ya upendo. Kwa Kiswahili ni 'kubusu'. Hakuna kitabu chochote cha Biblia kati ya vilivyoteuliwa kinachotoa maana nyingine. Tutatoa mfano wa kifungu kilichotumia kitenzi kilichotajwa.

Kiswahili: …*amamumunya ana make na eĩtu make, na amaathima* (Mw.31:55).

Kiswahili: ...akawabusu wanawe wa kiume na mabinti zake, akawabariki.

B2

***Kumbatĩlya***- Biblia ya Kikamba B2 imetumia kitenzi hiki badala ya kitenzi *mumunya*. Maana yake ni ‘kumbatia’. Tuangalie matumizi ya kitenzi mbadala *kumbatĩlya*:

Kikamba: *...amakumbatĩlya ana make na eĩĩtu make, na amaathima* (Mw. 31:55).

Kiswahili: ...akawakumbatia wanawe wa kiume na wa kike, akawabariki.

Maana ya kitenzi *kumbatĩlya* katika muktadha wa B2 ni 'shika mtu na kumzungushia mikono shingoni au mabegani'. Kwa Kiswahili ni 'kumbatia' au 'piga pambaja'. Inadhihirika kwamba maana katika B1 na B2 ni tofauti.

B1

***Nyala***- Kitenzi hiki kimetumiwa katika Biblia ya B1 kumaanisha hali ya mwili kuhitaji chakula. Katika lugha ya Kiswahili ni ‘kuona njaa’. Maana hii imejitokeza katika vifungu kadhaa katika vitabu vya Biblia vilivyotumiwa kupata data yetu. Mfano umetolewa kutoka kitabu cha Mwanzo.

Kikamba: *Na Yakovo aua ũsũũ; na Esaũ auma kĩthekanĩ, na aĩ mũnyalu; na Esaũ amwĩa Yakovo, Ngathĩsya, nĩngũkwĩsũva ...nũndũ nĩ mũnyalu* (Mw.25:29).

Kiswahili: Yakubu akapika uji; na Esau akarejea toka porini, ana njaa; naye Esau akamwambia Yakubu, Nakusihi nigawie...kwa maana nina njaa.

Kutokana na kifungu hiki tunaona kwamba Yakubu ameshinda mawindoni. Amerudi nyumbani akampata kaka yake Esau ametayarisha uji. Akamsihi amgawie uji ule. Sababu ya kuomba uji ameitaja pia- *nũndũ nĩ mũnyalu* (kwa maana nina njaa).

B2

Katika B2 kitenzi *nyala* hakipo katika muktadha huo wa *Mwanzo* 25:29. Kitenzi mbadala kilichoandikwa ni *iw'a nzaa* (ona njaa). Maana ya fungu hili la maneno inabainika katika mfano unaofuata:

Kikamba: *Esaũ nĩwookie aumĩte kũsyĩma ew'ĩte nzaa mũno. Nĩvo ĩndĩ Esaũ weeie Yakovo atĩĩ, "Mbĩkĩe mĩtũkĩ ...nĩw'ĩte nzaa mũno"* (Mw.25:29).

Kiswahili: Esau alirejea kutoka mawindoni akihisi njaa sana. Basi Esau akamwambia Yakubu hivi, "Nipakulie haraka...ninahisi njaa sana".

Kifungu hiki kimebainisha kwamba katika B2, dhana 'hisi njaa' imeundiwa msamiati mpya wa kuiwakilisha. Msamiati huo ni *ĩw'a nzaa.*

B1

***Vikĩla***- Mzizi wa kitenzi hizi *vik*- umebeba maana 'fika'. Kwa hivyo kitenzi *vikĩla* kinamaanisha 'fika kwenye' au 'nenda palipo kitu au mtu'. Mitume wa Yesu walitaka kujua ni wapi wangeandaa sherehe ya Pasaka. Yesu akawaambia waende mjini ambapo wangekutana na mtu aliyebeba kibuyu cha maji. Maelezo hayo yamenukuliwa kutoka kitabu cha *Luka* katika B1:

Kikamba: ... *mũkakomana na mũndũ ũkuĩte kĩkuu kya manzĩ; mũvikĩlei* (Lk. 22: 10).

Kiswahili: ...mtakutana na mtu amebeba kibuyu cha maji; nendeni alipo.

B2

***Atĩĩa***- Katika B2, kitenzi atĩĩa kimetumiwa badala ya *vikĩla*. Maana inayojitokeza katika B2 ni ile iliyokusudiwa katika B1.

Kikamba: …*nĩmũũkomana na mũndũ-ũme ũkuĩte kĩkuu kya kĩw'ũ. Mũatĩĩeĩ*…

Kiswahili: ...mtakutana na mwanamume aliyebeba kibuyu cha maji.

Vifungu vya Biblia vilivyotajwa hapo juu vimenukuliwa kutoka Biblia mbili: chapa ya UBS la mwaka wa 1974 na chapa ya IT la mwaka wa 2011. Matini ya kwanza imetumia kitenzi *mũvikĩlei* yaani mkaribieni au nendeni karibu naye. Katika Biblia ya Kikamba chapa ya IT la 2011 kitenzi hicho hakipo. Mahali pake pamewekwa kitenzi *mũatĩĩei*. Kitenzi *mũatĩĩei* kinamaanisha 'mfuateni', yaani 'endeni nyuma yake hadi mahali fulani'. Ni kitenzi kipya kilichoundwa na ambacho kina maana ile ile ya kitenzi cha B1.

B1

***Vuta-*** Maana asilia ya kitenzi hiki kama iliyorekodiwa katika Biblia B1 ni ‘chukua mali ya mtu bila idhini yake’ au ‘nyang’anya’. Mtu aliyenyang’anya watu mali yao aliitwa *mũvutani* au mnyang’anyi katika Kiswahili. Wingi wa *mũvutani* ni *avutani*. Haya tunayaona katika Biblia ya B1.

Kikamba: *Mũndũ ũmwe nĩwaumie Yelũsaleme athee Yeliko; nake akwatwa nĩ avutani ala mamũvutie ngũa na mamũkũnanga* (Lk.10:30).

Kiswahili: Mtu mmoja alitoka Yerusalemu kwenda Yeriko; naye akakamatwa na wanyang’anyi ambao walimnyang’anya nguo na wakampigapiga.

Maana ya nomino *avutani* ni ‘wanyang’anyi’. Kitenzi *vuta* kimeundwa kutokana na nomino hiyo kwa hivyo maana yake ni ‘nyangany’a’.

B2

***Umya-*** Hiki ndicho kitenzi kilichoandikwa katika B2 badala ya *vuta*. Maana yake itaonekana katika sentensi zifuatazo:

Kikamba: *Ve mũndũ ũmwe waumĩte Yelũsalemu atheete Yeliko. E nzĩanĩ nĩwavithuĩkĩiwe nĩ ing'endilĩ syamumya ngũã* na syamũkũna.

Kiswaihili: Mtu mmoja alitoka Yerusalemu akielekea Yeriko. Akiwa njiani alifumaniwa na majambazi wakamvua nguo na kumpiga.

Kitenzi *vuta* chenye maana 'nyang'anya' hakijatumiwa. Badala yake kitenzi *umya* chenye maana 'vua' kimetumiwa. Kwa hivyo katika muktadha wa B1 majambazi walimnyang'anya nguo yule mtu kisha wakampiga lakini katika B2 walimvua nguo tu kisha wakampiga. Haijasemwa iwapo majambazi walizibeba nguo hizo.

B1

***Ya ĩvu***- Katika B1, kitenzi *ya* kina kimeambatanishwa na nomino *ĩvu* kuunda nahau *ya ĩvu*. Nahau ni fungu la maneno ambayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida (Ndalu, 2015). Kitenzi *ya* kikiambatanishwa na nomino *ĩvu* (tumbo) kilileta maana ya 'himili' au 'pata mimba'. Haya yanaonekana katika Biblia ya Kikamba B1.

Kikamba: *Na Atamu amanya Eva mũka wake; nake aya ĩvu…* (Mw. 4: 1).

Kiswahili: (Adamu 'akamjua' Eva mke wake; naye akahimili.

Ingawa maana ya wazi ya nahau hii ni 'kula tumbo', muktadha wake hapa unaonyesha maana iliyokusudiwa ni 'akahimili' au 'akapata mimba'.

B2

***Itava***- Kitenzi hiki kilipatikana katika B2 kama kisawe cha *ya ĩvu*. Maana yake katika muktadha wa B2 ni ile ya kitenzi cha B1. Matumizi katika sentensi ni kama ifuatavyo:

Kikamba: *Atamu na mũka wake nĩmamanyanie kĩ-mwĩĩ na mũka wake aitava* (Mw. 4:1).

Kiswahili: (Adamu na mke wake walijuana kimwili na mke wake ‘akawa mzito’[akahimili]).

Katika mfano ulio hapa juu, tunaona kwamba fungu la maneno *aya ĩvu* ambayo yalitumiwa katika B1 limeondolewa na badala yake kitenzi *aitava* kimetumiwa kuleta maana ile ile ya akapata mimba. Hata hivyo kitenzi hiki kimetumiwa kiistiari. Maana halisi ni 'akawa mzito'. Istiari hii imetumiwa kuficha uzito wa dhana ya kuhimili kwa hivyo mabadiliko ya kiistiari yameshuhudiwa. Matokeo ya uchanganuzi wa maana kimuktadha yaliwekwa katika jedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.4: Maana ya vitenzi kwa mujibu wa muktadha**

| Vitenzi B1 (10) | Maana | Vitenzi B2 (10) | Maana | Kitabu ktk. Biblia |
|---|---|---|---|---|
| Kũka | Kimbia | Semba | Kimbia | Mw.14:10 |
| Kwatwa | Lewa | Milwa | Lewa | Mw.9:21 |
| Meta | Huzunika | Ĩthĩwa na kyeva | Huzunika | Mat.9:15 |
| Mumunya | Busu | Kumbatĩlya | Kumbatia | Lk.15:20 |
| Nyala | Hisi njaa | Ĩw’a nzaa | Hisi njaa | Mw.25:30 |
| Tambũka | Fanya ziara | Tembea | Fanya ziara | Mw.3:8 |
| Thilĩka | Udhika | Thata | Udhika | Mw.31:36 |
| Vikĩla | Fika alipo mtu | Atĩĩa | Fuata | Lk.9:23 |
| Vuta | Nyang’anya | Umya | Vua | Lk.10:30 |
| Ya ĩvu | Himili | Ĩtava | Himili | Mw.16:4 |

Vitenzi vilivyochanganuliwa vilikuwa ishirini. Ilibainika kwamba vitenzi vyote kumi vya B1 vilitoweka, yaani havikuwapo katika B2. Tuligundua kwamba vitenzi saba (7) vya B1 vilitoweka na maana ikahawilishwa kwa vitenzi saba (7) vilivyopatikana katika B2. Vitenzi hivyo ni *kũka*, *kwatwa*, *meta*, *nyala*, *tambuka*, *thilĩka* na *ya ĩvu*. Vitenzi vinginevyo vitatu (3) vya B1 vilitoweka lakini vitenzi mbadala vya B2 vilikuwa na

maana tofauti. Vitenzi hivyo ni *mumunya*, *vikĩla* na *vuta*. Katika sehemu inayofuata, maana ya vitenzi ilichanganuliwa kwa mujibu wa wazee:

### 4.1.2.2 Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa wazee

Kwa mujibu wa Alawadi (2020) akimnukuu Ogden na Richards (1923), nadharia ya dhana inasisitiza kuwa mzungumzaji wa lugha huwa na taswira akilini mwake ikirejelea kitu halisia katika ulimwengu wa lugha. Aidha, inadai kuwa picha za akilini ni dhahania ya kutosha kuweza kuwakilisha nomino au vitenzi vya kawaida. Kwa hivyo mtafiti aliamini kwamba wazee walizifahamu maana asilia na maana za ziada za vitenzi vilivyochunguzwa. Wazee kumi (10) walihojiwa ili kupata maana asilia na maana ya sasa ya vitenzi hivi. Aidha, tulihitaji kufahamu sababu ya kutoweka kwa vitenzi vyote vya B1. Walitaja visawe vya vitenzi vya B1 na maana. Yafuatayo ndiyo majibu yao:

B1

***Kũka***- Kwa mujibu wa wazee, kitenzi hiki kilitumiwa katika Kikamba cha kale kurejelea dhana mbili: ‘Kutoka kwa kitu mahali kilipokuwa kimeota au kimejishikiza (ng'oka)’, na ‘kimbia’. Wazee kumi (100%) walisema kuwa maana ya *kũka* ni *ng'oka*. Wanane (80%) walisema kitenzi hiki pia kilimaanisha 'kimbia'. Ilidhihirika kwamba maana hizo ndizo maana asilia za kitenzi hiki.

B2

***Semba***- Hiki ni kitenzi mbadala kilichopatikana katika B2. Wazee wote (100%) walisema kwamba maana yake ni ‘kimbia’. Watano (50%) wakatoa maana ya pili ‘toroka’. Kwa hivyo maana mbili zilipatikana kutokana na mahojiano ya wazee.

B1

***Kwatwa***- Katika Kikamba cha kale kitenzi hiki kina maana nne. Maana moja ni 'lewa', ya pili ni 'kamatwa au tiwa mbaroni', ya tatu ni 'kupatwa kwa jua au mwezi' na ya nne ni 'tendewa dhuluma za kingono'. Wazee wote kumi (100%) walitupatia maana 'tiwa mbaroni au kamatwa'. Tisa (9) kati yao (90%) walisema kitenzi hiki kilitumiwa kitasfida kumaanisha 'kutendewa dhuluma za kingono'. Saba kati yao (70%) wakasema maana ya kitenzi hiki ni 'lewa' na watano (50%) wakaibua maana nyingine 'kupatwa kwa jua au mwezi'.

B2

***Milwa***- Kitenzi hiki kimetumiwa katika B2 badala ya kitenzi *kwatwa*. Wazee wote (100%) walitueleza kwamba kitenzi hiki kinamaanisha 'kuwa katika hali ya kutojielewa kutokana na kunywa mvinyo'. Katika Kiswahili ni 'lewa'. Wanne (4) kati yao, asilimia arubaini (40%) wakasema pia ni 'zidiwa na furaha au majonzi kiasi'.

B1

***Meta***- *Kũmeta* ni kuwa na huzuni au kuwa na majonzi. Maana hii ni kwa mujibu wa wazee wote (100%). Hii ndiyo maana asilia na maana ambayo ilikusudiwa katika B1.

B2

***Ĩthiwa na kyeva***- Hii ndiyo kauli iliyotumiwa katika B2 badala ya kitenzi *meta* cha B1. Wazee wote (100%) walisema kwamba kauli hii ina maana sawa na kitenzi *meta* cha B1. Maana yake ni kuwa na huzuni, majonzi au kutokuwa na furaha.

B1

***Mumunya***- Maana ya kitenzi hiki katika muktadha wa B1 ilikuwa 'kubusu'. Wazee wawili (2) ambao ni asilimia ishirini (20%) ya jumla ndio walioiunga mkono maana hiyo. Wengine wawili (2), asilimia ishirini (20%) wakatupatia kitenzi kilichotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza 'kũkisi' kama maana ya kitenzi *mumunya*. Kukisi maana yake ni kubusu. Kwa hivyo wazee ambao walitoa maana ya kubusu walikuwa wanne (4). Idadi hii ni asilimia arubaini (40%). Wazee sita (6) walisema maana ya *mumunya* ni 'kubana kitu hasa kitu kitamu baina ya ulimi na kaakaa ngumu kisha kukifyonza'. Maana kwa mujibu wa muktadha ilijulikana na asilimia arubaini (40%) pekee ya jumla ya wazee waliohojiwa.

B2

***Kumbatĩlya***- Hiki ni kitenzi kilichoandikwa katika B2 badala ya kitenzi *mumunya*. Maana yake katika B2 ilikuwa shika mtu na kumzungushia mikono mabegani kama ishara ya upendo. Katika Kiswahili ni 'kumbatia'. Wazee saba (7) walitupatia maana 'fumbata kitu kiganjani' na watatu (3) wakasema maana yake ni 'kumbatia mtu'. Ni asilimia thelathini (30%) pekee ambayo iliifahamu maana kulingana na muktadha.

B1

***Nyala***- Maana ya kitenzi hiki kwa mujibu wa muktadha ni 'hisi njaa'. Lakini hakuna aliyeitaja maana hiyo. Wazee wote (100%) walisema kuwa maana yake ni 'tokwa na jasho'. Ilibainika kwamba maana ya muktadha imepotea na haipo tena katika msamiati wa wazee.

B2

***Ĩw'a nzaa***- Kitenzi hiki kilitumiwa katika B2 kumaanisha 'hisi njaa'. Maana ya kauli hii kwa mujibu wa wazee wote (100%) ni 'hisi njaa'. Maana hii ndiyo iliyowakilishwa na kitenzi *nyala* ambacho sasa huwakilisha dhana 'tokwa na jasho'.

B1

***Tambũka***- Kitenzi hiki kilitumiwa katika B1 kumaanisha 'tembea kwa migu'. Baada ya usaili wa wazee tulipata maana mbili za kitenzi hiki. Wazee wote (100%) walisema kwamba maana yake ni 'fanya ziara kwa kutumia chombo cha usafiri'. Sita (6) kati yao wakiwakilisha asilimia sitini (60%) walisema maana yake ni 'tembea kwa miguu'. Kwa hivyo kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili.

B2

***Tembea***- Hiki ni kitenzi mkopo kutoka lugha ya Kiswahili. Ndicho kilichoandikwa katika B2 badala ya kitenzi asilia *tambũka.* Wazee walipoulizwa maana yake, wote (100%) walisema kuwa kinamaanisha 'nenda kwa miguu'. Saba (70%) kati yao walisema kuwa maana yake ni 'fanya ziara kwa chombo cha usafiri'. Maana mbili za kitenzi *tembea* zimehawilishwa kwa kitenzi mkopo *tembea*.ni sawa na zile za kitenzi cha awali *tambũka*.

B1

***Thilĩka***- Kitenzi hiki kilipatikana katika B1 kikimaanisha 'udhika au kasirika'. Wazee wote (100%) walisema kwamba maana yake ni 'udhika au kasirika'. Maana ya kitenzi hiki ni moja.

B2

***Thata***- Kitenzi hiki kiliandikwa katika B2 badala ya kitenzi *thilĩka*. Katika muktadha huo kilikuwa na maana ‘kasirika’. Wazee wote kumi (100%) waliohojiwa walisema maana yake ni '‘dhika au kasirika'. Watatu wao (30%) walitoa maana ya ziada; 'kufura kwa sehemu ya mwili'. Kwa hivyo kutokana na majibu ya wazee maana mbili zilipatikana.

B1

***Vikĩla***- Katika Biblia B1, kitenzi hiki kilitumiwa kumaanisha fuata. Baada ya kuwahoji wazee kilipata maana ya ziada. Wazee wanne (40%) walisema kuwa maana yake ni 'kutembea nyuma ya mtu ambaye tayari ameanza safari, kwa nia ya kufika alipo'. Kwa kiswahili ni 'fuata'. Maana hii ndiyo iliyopatikana katika muktadha wa B1. Wanane wao (80%) walisema kuwa maana nyingine ya *vĩkila* ni ‘kuweza kugusa kitu kilicho mbali’. Kutokana na majibu ya wazee ilibainika kwamba maana ya kwanza ya kitenzi hiki inajulikana na wazee wachache (40%). Wengi wao (80%) wanafahamu maana ya pili pekee.

B2

***Aĩĩĩa***- kitenzi hiki kilitumiwa katika B2 badala ya kitenzi *vikĩla* na maana yake ilikuwa ‘fuata’. Wazee wote (100%) walitoa maana hiyo 'fuata'. Ilibainika kwamba nomino hii ilitwikwa jukumu la kuwakilisha dhana fuata kutokana na hali ya kitenzi asilia vikĩla kuwa na maana mbili. Aidha, wazee watatu (3) ambao ni asilimia thelethini (30%) walitupatia maana ya ziada; shika maagizo au mafunzo ya mtu fulani. Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili.

B1

***Vuta***- Maana ya kitenzi hiki katika muktadha ni 'nyang'anya mtu mali'. Ni wazee wanne (4) Idadi hii ni ndogo kwa kuwa ni asilimia arubaini (40%) ya jumla ya wazee waliohojiwa. Maana hii ilionekana kufifia au kusahaulika miongoni mwa wazee. Wazee wote (100%) walitaja maana nyingine ya kitenzi hiki, 'achisha mtu kazi'. Wazee wanane (80%) miongoni mwao walisema kitenzi hiki pia kilimaanisha 'ondoa maandishi'. Kutokana na mahojiano hayo tulipata maana tatu za kitenzi hiki.

B2

***Umya***- Kitenzi hiki ndicho kilichoandikwa katika B2 badala ya kitenzi *vuta*. Katika muktadha huo kilimaanisha 'vua mavazi mwilini'. Wazee tisa (9) walisema maana yake ni 'ondoa kitu kilipokuwa'. Sita (6) kati yao walitupatia maana 'vua mavazi au mapambo mwilini'. Watano (5) walisema maana yake ni 'toa mali au fedha kwa ajili ya Mungu au kusaidia mwenye mahitaji'. Kwa mujibu wa wazee, kitenzi hiki kilikuwa na maana tatu.

B1

***Ya ĩvu***- Ktika muktadha wa B1, kitenzi hiki kilikuwa na maana ya 'pata mimba au himili'. Wazee wote (100%) walisema maana ya kauli hii ni himili au pata mimba. Maana asilia ya kitenzi hiki ilikuwa moja.

B2

***Itava***- Hiki ndicho kitenzi kilichoandikwa katika B2 badala ya 'ya *ĩvu'*. Katika muktadha huo kilimaanisha 'pata mimba' au 'himili'. Wazee wote (100%) walisema maana yake ni 'pata mimba'. Wanane (80%) kati yao waliongezea maana ya pili, 'kuwa zito'. Kwa hivyo kitenzi hiki kina maana mbili. Jedwali lifuatalo linaonyesha muhtasari

wa maana za vitenzi kwa mujibu wa wazee. Idadi hapa ni idadi ya wahojiwa waliotoa maana ya kitenzi au waliokosa kueleza maana.

**Jedwali 4.5: Maana ya vitenzi kwa mujibu wa Wazee**

| Vitenzi B1 (10) | Maana | Idadi | Vitenzi B2 (10) | Idadi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| Kũka | Ng'oka<br>Kimbia | 10<br>8 | Semba | 10<br>5 | Kimbia<br>Toroka |
| Kwatwa | Kamatwa na polisi<br>Lewa<br>Dhulumiwa kingono<br>Kupatwa kwa jua | 10<br>7<br>9<br>5 | Milwa | 10<br>4 | Lewa pombe<br>Zidiwa na furaha au majonzi |
| Meta | Kuwa na huzuni/ majonzi<br>au kukosa furaha | 10 | Ithĩwa na kyeva | 10 | Kuhuzunika na kukosa furaha |
| Mumunya | Piga busu<br>'Kisi'<br>Bana kitu baina ya ulimi na kaakaa na kukifyonza | 2<br>2<br>6 | Kumbatĩlya | 7<br>3 | Fumbata kitu kiganjani<br>Kumbatia mtu |
| Nyala | Tokwa na jasho | 10 | Iw'a nzaa | 10 | Hisi njaa |
| Tambũka | Fanya ziara kwa kutumia chomo cha usafiri<br>Tembea kwa miguu | 10<br>6 | Tembea | 10<br>7 | Nenda kwa miguu<br>Fanya ziara kwa kutumia chombo cha usafiri |
| Thilĩka | Kasirika/ udhika | 10 | Thata | 10<br>3 | Kasirika/ udhika<br>Kufura kwa sehemu ya mwili |
| Vikĩla | Fuata<br>Weza kugusa kitu kilicho mbali | 4<br>8 | Atĩĩa | 10<br>3 | Fuata nyuma<br>Shika maagizo/mafunzo |
| Vuta | Nyang'anya<br>Achisha mtu kazi<br>Ondoa maandishi | 4<br>10<br>8 | Umya | 9<br>6<br>5 | Ondoa kitu kilipokuwa<br>Vua mavazi au mapambo<br>Toa mali/fedha kwa Mungu au kusaidia mtu |
| Ya ĩvu | Himili/ Pata mimba | 10 | Itava | 10<br>8 | Himili/ Pata mimba<br>Kuwa -zito |

Jedwali lililochorwa hapa juu linaonyesha vitenzi ishirini (20), kumi (10) kutoka B1 na kumi (10) kutoka B2. Maana za vitenzi hivi ni kwa mujibu wa wazee waliohojiwa. Maana tulizopata kwa mujibu wa muktadha zilijitokeza katika majibu ya wazee na kisha vitenzi vikapata maana za ziada. Ilibainika kuwa vitenzi kumi na vinne (14) vilikuwa vya kipolisemia. Idadi hii ni asilimia sabini (70%) ya vitenzi ishirini (20). Vitenzi hivyo ni *kuĩka*, *semba*, *kwatwa*, *milwa*, *mumunya*, *kumbatĩlya*, *tambuĩka*, *tembea*, *vikĩla*, *atĩĩa*, *vuta*, *umya*, *itava* na *thata*.

Maana za vitenzi kwa mujibu wa muktadha zilibainika kuwa maana asilia au miongoni mwa maana asilia za vitenzi. Sababu ni kuwa maana hizo za kimuktadha zilitajwa na wazee kuwa maana za vitenzi hivyo. Hata hivyo, idadi kubwa ya wazee waliohojiwa ilishindwa kubaini maana asilia za kimuktadha. Maana hizo asilia za kimuktadha zimesahaulika. Kwa mfano, idadi ndogo ya wazee ilifahamu maana asilia za vitenzi vifuatavyo:

*Tambuĩka*- Tembea kwa miguu- 60%

*Mumunya*- Busu-40%

*Vikĩla*- Fuata- 40%

*Vuta*- Nyang'anya- 40%

*Nyala*- Hisi njaa- 0%

Maana zilizoambatanishwa na vitenzi hivi ni maana asilia lakini baadhi ya wazee hawakuzifahamu. Utafiti uligundua kwamba maana asilia za maneno zilizidi kuathiriwa na michakato ya mabadiliko ya maana kama vile kufifia kwa maana. Watoto walihojiwa ili kubaini iwapo walifahamu maana kama walivyoeleza wazee au walifahamu maana tofauti. Uchanganuzi wa majibu ya watoto kuhusu maana za vitenzi unaelezwa hapa chini:

### 4.1.2.3 Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa watoto

Watoto walihojiwa ili kubaini iwapo walizifahamu maana za vitenzi kama zilivyotokea katika Biblia na kama wazee walivyoeleza. Vitenzi ishirini (20) viliandikwa ubaoni, kumi (10) kutoka B1 na kumi (10) kutoka B2. Watoto waliulizwa kueleza maana ya vitenzi hivyo na visawe kama walivyoelewa wao. Ilibainika kwamba baadhi ya maana zilipotoshwa. Mhimili uliosaidia kufahamu hayo ni wa nadharia ya dhana. Mhimili huo unafafanua kwamba maana inayojengwa hutegemea zaidi ukomo wa fikra za msikilizaji au mzungumzaji. Kwa hivyo utofauti katika uwezo wa kujenga dhana akilini kuhusu leksimu fulani unaweza kupunguza au kubadili maana ya kitu kinachojengewa dhana. Majibu ya watoto kuhusu vitenzi yameandikwa kama ifuatavyo:

B1

***Kuƙa***- Watoto walidhihirisha uelewa wa maana ya kitenzi hiki pale ambapo watano (50%) walikubaliana na wazee kuwa maana yake ni 'kimbia'. Wawili (20%) wakasema maana ya kitenzi hicho ni 'toka mahali kitu kilikuwa kimejishikisha' au 'ng'oka'. Mmoja (10%) akasema maana yake ni 'kuku', maana ambayo kwa maoni ya mtafiti ilikuwa imepotoshwa. Wawili (20%) hawakujibu. Maana mbili za kitenzi hiki zilijitokeza miongoni mwa watoto ingawa kwa asilimia hamsini (50%) na asilimia ishirini (20%) mtawalia.

B2

***Semba***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili kwa mujibu wa wazee; ‘kimbia’ na ‘toroka’. Watoto saba (70%) waliandika maana ‘kimbia’ na watatu (30%) wakaandika ‘toka mbio’. Maana walizotoa zilikuwa sawa. Maana moja ‘kimbia’ ilieleweka miongoni mwa watoto lakini maana ya pili ‘toroka’ ikadondoshwa.

B1

***Kwatwa***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana nne kwa mujibu wa wazee; kamatwa na polisi, kutendewa dhuluma za kingono, lewa na kushikwa kwa jua. Watoto wote (100%) walitoa maana moja, 'kamatwa na polisi' au 'tiwa mbaroni'. Maana nyinginezo tatu zilidondoshwa.

B2

***Milwa***- Maana za kitenzi hiki kwa mujibu wa wazee zilikuwa mbili; lewa kutokana na kunywa mvinyo na zidiwa na furaha au huzuni. Watoto wanane (80%) walieleza maana kwa kutumia lugha ya Kiswahili 'lewa pombe'. Wawili (20%) hawakujibu. Maana iliyojitokeza kwa mujibu wa watoto ni moja. Maana nyingineyo haikujitokeza.

B1

***Meta***- Maana asilia ya kitenzi hiki ni 'kuwa na huzuni'. Watoto watano (50%) waliandika 'ng'aa' kama maana ya kitenzi hicho. Watatu (30%) wakajibu 'metameta'. Mmoja (10%) akasema maana yake ni 'waite' katika Kiswahili. Mtoto huyu alifasiri kitenzi agizi cha Kikamba *mete* chenye maana 'waite!' ambacho sicho kilichoandikwa na mtafiti. Mtoto mmoja (10%) hakujibu. Tuligundua kwamba watoto hawakuifahamu maana ya kitenzi hiki na kilikuwa hakipo katika msamiati wao. Walichofahamu maana ni kitenzi cha Kiswahili 'meta' chenye umbo sawa na kile cha Kikamba.

B2

***Ĩthĩwa na Kyeva***- Maana asilia ya kitenzi hiki ni kuwa na huzuni. Watoto saba (70%) walithibitisha maana hiyo. Watatu (30%) hawakujibu. Kutokana na ugunduzi wetu, huu ndio msamiati unaotumiwa sana katika jamii kueleza hali ya huzuni na majonzi. Kitenzi cha B1 chenye maana sawa na hiki hakitumiki miongoni mwa watoto hawa.

B1

***Mumunya***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili; ‘busu mtu’ na ‘fyonza kitu kilichobanwa baina ya ulimi na kaakaa’. Watoto watatu (3) walijibu 'weka kitu ulimini na kukifyonza'. Wawili (2) walijibu 'tafuna' na watano (5) hawakujibu. Ilibainika maana ya kitenzi hiki ilieleweka na asilimia thelathini (30%) ya watoto. Asilimia sabini (70%) haikufahamu maanaya kitenzi hiki.

B2

***Kumbatĩlya***- Wazee walitupatia maana mbili za kitenzi hiki; ‘kumbatia mtu kama ishara ya upendo’ na ‘fumbata kitu kiganjani’. Watoto wanane (80%) walisema maana yake ni ‘fumbata kitu kiganjani’. Wawili hawakujibu. Maana moja ilidondoshwa.

B1

***Nyala***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili. Maana moja ‘tokwa na jasho’ ilitolewa na wazee na maana ya pili ‘hisi njaa’ ikapatikana katika muktadha. Watoto wote (100%) walisema maana yake ni ‘tokwa na jasho’. Hawakujua maana nyingineyo.

B2

***Ĩw’a nzaa***- Maana asilia ya kitenzi hiki ni ‘hisi njaa’. Maana hii ilipatikana katika B2 na katika maelezo ya wazee. Watoto wote (100%) walisema maana ya kitenzi hiki ni ‘hisi njaa’. Kitenzi hiki kilikuwa na maana moja.

B1

***Tambũka***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili. Maana ya kwanza ni ‘fanya ziara’ au ‘safiri kwa kutumia chombo cha usafiri’. Maana ya pili ni ‘kutembea kwa miguu’. Watoto walikuwa na utata katika kufasiri maana ya kitenzi hiki. Watano (50%)

walisema maana yake ni ‘nyooka’. Maana hii ilikuwa imepotoshwa kwa kuwa kitenzi chenye maana hii ni *tambũĩka*. Watatu (30%) walitupatia maana potovu inayokaribiana na hii; ‘kunjuka’. Wawili (20%) hawakujibu. Ilibainika kwamba watoto wote (100%) hawakujua maana ya kitenzi hiki.

B2

***Tembea***- Hiki ni kitenzi kilichokopwa kutoka lugha ya Kiswahili chenye maana mbili. Maana ya kwanza ni ‘safiri au kwenda kwa miguu’ na maana ya pili ni ‘fanya ziara kwa kutumia chombo cha usafiri’. Watoto wote (100%) walikubaliana na maana hii kwa kusema maana ya kitenzi hiki ni ‘nenda mahali kwa miguu’ na wawili (20%) wakasema pia kinamaanisha ‘fanya ziara kwa kutumia chombo cha usafiri’.

B1

***Thilika-*** Maana asilia ya kitenzi hiki ni kasirika. Watoto walipoulizwa kueleza maana ya kitenzi hiki, mmoja (10%) alisema kwamba maana yake ni ‘tetemeka’. Mwengine (10%) alisema maana yake ni ‘chomeka’. Mtoto mwengine (10%) mmoja alitupatia maana ‘funguka’. Watoto saba (70%) hawakujibu. Watoto hawakuifahamu maana ya kitenzi hiki. Maana walizotoa zilikuwa zimepotoshwa kwa kuwa ‘tetemeka’ ni *thĩĩĩã*, ‘chomeka’ ni *vya* na ‘funguka’ ni *vinguĩka* katika Kikamba. Ilibainika kwamba kitenzi hiki hakikuwapo katika msamiati wa watoto.

B2

***Thata***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana sawa na kitenzi *thilĩka* cha B1. Maana yake ni ‘kasirika’. Watoto wote (100%) walitupatia maana ‘kasirika’. Kutokana na majibu yao, walielewa maana ya kitenzi hiki na walikitumia katika mazungumzo.

B1

***Vikĩla***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili kwa mujibu wa wazee; 'weza kugusa kitu kilicho mbali kwa kupanua mkono.' Maana ya pili ni 'fuata'. Maana hii ya pili ndiyo maana iliyojitokeza katika B1. Watoto saba (70%) walisema maana *vikĩla* yake ni 'fikia'' yaani kuweza kugusa kitu kilicho mbali hata kama ni kwa ncha ya vidole. Maana hii ni sawa na maana moja iliyotajwa na wazee. Watatu (30%) hawakujibu. Kitenzi hiki kimedondosha maana moja.

B2

***Atĩĩa***- Maana asilia ya kitenzi hiki ni 'tembea nyuma ya mtu aliyeanza safari kwa nia ya kufika alipo' au 'fuata'. Watoto wote (100%) walitupatia maana hii. Maana hii ni miongoni mwa maana za kitenzi *vikĩla*. Tuligundua kwamba watoto walifahamu maana ya kitenzi hiki.

B1

***Vuta***- Kitenzi hiki kilikuwa na maana mbili: Maana ya kwanza ni 'nyang'anya mtu mali yake', maana ya pili ni 'ondoa maandishi' na maana ya tatu ni 'achisha mtu kazi'. Watoto sita (60%) walisema maana yake ni 'ondoa maandishi' na wanne (40%) wakatoa maana 'achisha mtu kazi'. Maana mbili ambazo watoto walitupatia kuhusu kitenzi *vuta* ni sawa na tulizopata kutokana na usaili wa wazee. Watoto hawakuitambua maana ya tatu ya kitenzi hiki ambayo ni 'nyanganya mtu mali'. Hii ni maana ambayo ilikuwa katika B1. Maana hiyo moja imedondoshwa.

B2

***Umya***- Wazee walitupatia maana tatu za kitenzi hiki. Maana moja ni vua vazi au pambo mwilini. Maana nyingine ni toa kitu mahali kilipokuwa na ya tatu ni toa mali au fedha

kama sadaka kwa Mungu au kwa mtu maskini. Watoto walizitambua maana tatu za kitenzi hiki sawasawa na wazee. Sita (6) walisema maana ya kitenzi hiki ni ‘vua mavazi au mapambo yaliyovaliwa mwilini’. Wawili (2) wakasema maana yake ni ‘ondoa kitu mahali kilipokuwa’ na wawili (2) wakasema ‘toa kitu kama sadaka kwa Mungu au kwa mtu’. Ilibainika kwamba kitenzi hiki kilikuwapo katika msamiati uliotumiwa miongoni mwa watoto.

B1

***Ya ĩvu***- Maana asilia ya kitenzi hiki ni ‘pata mimba’ au ‘himili’. Watoto wanane (80%) walisema maana yake ni ‘kula matumbo’. Majibu yao yalitokana na maana halisi ya kitenzi *ya* ambayo ni ‘kula’ na nomino *ĩvu* yenye maana ‘tumbo’. Wawili (20%) hawakujibu. Kauli hii haikueleweka miongoni mwa watoto kutokana na kutokuwapo katika msamiati wao wa mazungumzo.

B2

***Itava***- Kitenzi itava kilikuwa na maana mbili. Maana moja ni himili na ya pili ni -kuwa zito. Watoto walielewa maana ya kitenzi hiki. Saba (7) kati yao, sambao ni asilimia sabini (70%) walisema kwamba maana ya kitenzi hiki ni ‘kuwa na mimba’ na watatu (3) ambao ni asilimia thelathini (30%) wakasema maana ya kitenzi hiki ni ‘kitu kuwa kizito’. Jedwali lifuatalo linaonyesha muhtasari wa maana za vitenzi kwa mujibu wa watoto:

**Jedwali 4.6: Maana ya Vitenzi kwa mujibu wa watoto**

| Vitenzi B1 (10) | Idadi | Maana | Vitenzi B2 (10) | Idadi | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| Kũka | 5 | Kimbia | Semba | 7 | Kimbia |
| | 2 | Ng'oka | | 3 | Enda mbio |
| | 1 | Kuku | | | |
| | 2 | Hawakujibu | | | |
| Kwatwa | 10 | Kamatwa na polisi | Milwa | 8 | Lewa pombe |
| | | | | 2 | Hawakujibu |
| Meta | 5 | Ng'aa | Ĩthĩwa na kyeva | 7 | Kuwa na huzuni |
| | 3 | Metameta | | 3 | Hawakujibu |
| | 1 | Waite | | | |
| Mumunya | 3 | Weka kitu ulimini na kukifyonza. | Kumbatĩlya | 8 | Fumbata kitu kiganjani |
| | 2 | Tafuna | | 2 | Hawakujibu |
| | 5 | Hawakujibu | | | |
| Nyala | 10 | Tokwa na jasho | Ĩw'a nzaa | 10 | Ona njaa |
| Tambũka | 5 | Nyooka | Tembea | 10 | Nenda kwa miguu |
| | 3 | Kunjuka | | 2 | Safiri kwa chombo |
| | 2 | Hawakujibu | | | |
| Thilĩka | 1 | Tetemeka | Thata | 10 | Kasirika |
| | 1 | Chomeka | | | |
| | 1 | Funguka | | | |
| | 7 | Hawakujibu | | | |
| Vikĩla | 7 | Fikia | Atĩĩa | 10 | Fuata |
| | 3 | Hawakujibu | | | |
| Vuta | 6 | Ondoa maandishi | Umya | 10 | Nyang'anya |
| | 2 | Hawakujibu | | | |
| Ya ĩvu | 8 | Kula matumbo | Itava | 7 | Kuwa na mimba |
| | 2 | Hawakujibu | | 3 | Kuwa -zito |

Tunapolitazama jedwali *4.6* tunagundua kwamba:

i) Vitenzi vyote kumi (10) vya B1 vilivyotumiwa kama data ya utafiti huu havikuwamo katika B2. Idadi hii ni asilimia mia moja (100%).

ii) Vitenzi vya B1 vya kipolisemia ni sita (6). Vitenzi hivyo ni *kũka*, *kwatwa*, *mumunya*, *tambũka*, *vikĩla* na *vuta*. Idadi hii ni asilimia sitini (60%).

iii) Vitenzi vyote vya kipolisemia katika B1 vilidondosha maana moja kati ya maana zake.

iv) Vitenzi tisa (90%) vya B2 vilibeba maana moja ya vitenzi vya B1. Hii ni maana iliyodondoshwa na vitenzi vya B1. Kitenzi kimoja cha B2 *iw'a nzaa* (hisi njaa) kilikuwa na maana tofauti na kitenzi *nyala* (tokwa na jasho) cha B1.

v) Vitenzi vya B1 ambavyo havikueleweka maana kwa hivyo vilipotoshwa maana na baadhi ya watoto vilikuwa vinane (8). Vitenzi hivyo ni *kũka*, *meta*, *tambũka*, *thilĩka*, *vikĩla*, *vuta* na *ya ĩvu*. Idadi hii ni asilimia hamsini na tatu (53%).

vi)Vitenzi vya B1 ambavyo vilihamisha maana kisha vikatoweka ni vinne: *meta*, *tambũka*, *thilĩka* na ya *ĩvu*.

vii) Watoto walifahamu maana ya vitenzi vyote (100%) vya B2 na walitoa maana sawa na wazee.

viii) Vitenzi vyote (100%) vya B2 havijabadilika maana. Maana walizotoa wazee ndizo tulizopewa na watoto.

Tukiangalia kigezo cha tatu (iii), cha tano (v) na cha sita (vi), vitenzi vya B1 vimebadilika maana. Vitenzi vilivyo katika B2 ndivyo vinavyotumiwa na watoto katika mawasiliano yao (taz. vii na viii). Uchanganuzi wa majibu ya watoto kuhusu nomino na vitenzi ulitupatia picha kamili ya hali ya lugha ya Kikamba ilivyo katika karne hii ya 21. Sababu ni kwamba watoto hawa ndio waliorithishwa lugha hii na ndio wanaotarajiwa kurithisha vizazi vijavyo huku tukiwa na matumaini kwamba lugha hii itadumishwa. Maneno ya Kikamba yaliyoteuliwa yamedondosha maana kwa kiasi

kikubwa bila kupata maana zaidi. Nomino ndizo zilizoathirika zaidi kutokana na mabadiliko ya kisemantiki; tulishuhudia nomino za B1 ambazo hazifahamiki kabisa miongoni mwa watoto (53%) na nyingine ambazo watoto walifahamu maana moja moja (47%). Iwapo hali hii itaendelea, basi huenda baadhi ya maneno mazima ya Kikamba katika B1 yakafa pindi vitabu vya kale vitakapoisha. Sehemu inayofuata ilishughulikia michakato mbalimbali ya kisemantiki ambayo imeathiri nomino na vitenzi vilivyochunguzwa:

## 4.2 Michakato ya Kisemantiki inayosababisha Kubadilika kwa Maana

Kuna michakato kadhaa ambayo huchangia mabadiliko ya kisemantiki ingawa baadhi ya michakato ina athari kubwa zaidi kuliko mingine (McWhorter, 2020). Michakato hiyo ya kisemantiki ni kama vile usogezi, ubanaji, upanuzi, utowekaji, usambaratikaji, uimarikaji wa maana, uhamishaji wa maana, upolisemia, miongoni mwa mingine.

### 4.2.1 Usogezi wa Maana

Usogezi wa maana ni kuhamishwa kwa maana kutoka kwa neno moja hadi kwa neno jingine. (Lehnann, 1962). Maana uhamishwa kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine. Usogezi wa maana unaweza kutokea kwa njia tatu:

i. Metonimu
ii. Sitiari
iii. Sinedoche

Data ya utafiti wetu iliathiriwa na usogezi wa kisitiari na sinedoche pekee. Matumizi ya metonimu hayakujitokeza katika utafiti huu.

#### 4.2.1.1 Sitiari

Sitiari ni hali ya kutumia dhana moja kurejelea dhana nyingine yenye mfanano na dhana ya kwanza (Hollmann, 2009). Kwa mfano mpishi hodari Gordon Ramsay hutumia sitiari *doughnuts* kurejelea wapishi wanaokosa kutia fora katika shindano la upishi. Doughnuts huliwa tu wala hazina kazi nyingine yoyote. Hazifai mtu vinginevyo ila kuliwa. Gordon anawafananisha wapishi hawa na *doughnuts* kuonyesha kwamba hawana akili pevu au hawajiwezi katika mapishi. Watoto wazawa wa karne ya 21 hutumia jina la kisitiari *mũsinga* kurejelea ‘pombe’. Pombe inafananishwa na *mũsinga* (mzinga) kutokana na uwezo wake wa ‘kumlipua’ mtu aliyeibugia kwa wingi akawa hoi hajiwezi.

Nomino *asa* katika utafiti huu ilikumbwa na usogezi wa kisitiari. Maana asilia ya nomino hii ni 'mzazi wa kiume' au 'baba'. Kwa kuwa Mungu ana sifa za ki-baba kama vile kulinda, kusamehe na kutunza 'wanawe', jina *asa* likawa likitumiwa kumrejelea. Sasa maana ya nomino *asa* imebadilika kuwa Mungu. *Ukũngi* ni aina ya upepo mwanana ambao huvuma kwa taratibu. Maana tuliyopata kwa asilimia kumi (10%) ya watoto ni 'uchafu unaotoka kwenye nafaka kama vile mahindi wakati wa kupepeta'. Katika Kiswahili ni ‘makapi’. Dhana hizi mbili zina mfanano na mwingiliano wa kimwonekano.

*Ukũngi* hupeperusha vitu vyepesi kama vile makapi. Daima upepo huu huwa umebeba mchanga, makapi na vitu vinginevyo vyepesi. Haiwezekani kuwa upepo utavuma pasipo kupeperusha uchafu au makapi japo kidogo. Pana uwezekano wa baadhi ya watu kutotofautisha baina ya dhana hizi mbili, na hivyo ndivyo ilivyofanyika kwa watoto.

Nomino *mĩsyĩ* pia ilibadilika kutokana na usogezi wa kisitiari. Wazee walithibitisha kwamba maana asilia ya nomino hii ni zana za vita zinazojulikana kama 'mishale' kwa

Kiswahili. Baada ya kiberiti kuvumbuliwa, vile vijiti vyake vikawa vinafanana na mishale; vilikuwa na kichwa kama chembe cha mshale na vilifanya kazi kama vile upinde na mshale vinavyofanya. Vijiti hivyo vikapewa jina *mĩsyĩ.* Mabadiliko ya kisitiari yameathiri nomino tatu (3). Idadi hii ni asilimia sita (6%) ya maneno katika utafiti huu.

### 4.2.1.2 Sinedoche

Sinedoche ni uhusiano wa sehemu ya kitu kwa kitu kizima au kitu kizima kwa sehemu (Traugott, 2002). Kwa mfano matumizi ya nomino ya Kiingereza *tongue* (ulimi) kumaanisha *language* au 'lugha'. Mfano mwingine wa sinedoche ni matumizi ya neno sikio kumaanisha mwili mzima. Kwa mfano iwapo unataka mtu akusikilize unaweza kumwambia, "Nipe sikio!" Ingawa mzungumzaji ameongea kuhusu sikio huwa anaomba mtu mwenyewe (mzima) amakinike katika kusikiliza wala si sikio lake.

Nomino mbili *mũsyĩ* na *ndũa* zilibadilika kutokana na mchakato wa sinedoche. Kwa mujibu wa asilimia themanini (80%) ya wazee na watoto wote (100%), *mũsyĩ* ni 'eneo dogo wanamoishi watu wa familia moja''. Wazee sita (6) kati yao (60%) walisema kwamba *mũsyĩ* ni 'eneo kubwa la nchi lenye watu wengi na mijengo mikubwa mikubwa au mji'. Awali maana ya nomino *ndũa* ilikuwa 'eneo kubwa lenye watu wengi na mijengo mikubwa mikubwa'. Maana yake ni mji au jiji. Maana inayofahamika sasa ni 'eneo dogo lenye watu wachache' au 'kijiji'. Mji ni dhana pana na kijiji ni dhana finyu. Aidha, mji ni eneo kubwa na kijiji ni eneo dogo na dhana hizi mbili zina uhusiano.

### 4.2.2 Upanuzi wa Maana

Upanuzi wa maana ni mchakato ambapo maana za neno huongezeka (Crowley & Bowern, 2010). Aidha, neno linapopanuka maana husemekana limepata maana ya jumla; kwa hivyo linawasilisha dhana mbalimbali au linatumika katika miktadha

mipana zaidi. Kwa mfano nomino ya Kiingereza *dog* ilikuwa na maana bayana, 'mbwa wa aina maalum mwenye nguvu nyingi'. Hatimaye maana ya nomino hiyo ilipanuka, ikaanza kurejelea mbwa wa aina yoyote. Maana asilia ya nomino *tingatinga* ni kifaa maalumu kinachotumika kuchimba ardhi na kuchota udongo aghalabu wakati wa kutengeneza barabara (Rajab, 2017). Katika muktadha wa siasa ni 'kiongozi mwenye nguvu kiutendaji'. Katika utafiti wetu, nomino nne (4) zilipanuka maana (8%). Nomino hizo ni *ukũngi, kĩmũtũ, mĩsyĩ* na *maangi.*

Maana ya nomino *ũkũngi* ni aina moja ya upepo ambao ni mwanana, usiovuma kwa nguvu. Watoto wawili (20%) walielewa maana ya nomino hii kama *kĩseve* au upepo. Upepo wa aina yoyote unaovuma waliupa jina hili. Kwa hivyo maana ya nomino hii imepanuka.

*Kĩmũtũ* ni aina ya mkate ambao uliokwa baada ya unga kukandwa na kuachwa kwa muda uumuke na kuchachuka. Watoto walisema kwamba maana yake ni 'chakula'. Kuna aina nyingi za vyakula kwa hivyo ikiwa *kĩmũtũ* ni chakula basi nomino hii inawakilisha aina nyingi za chakula kama vile kande, sima na wali.

Tulithibitisha kuwa nomino *mĩsyĩ* awali ilirejelea dhana 'zana za vita' zinazoitwa kwa Kiswahili 'mishale'. Matumizi ya viberiti yalipoanza katika jamii ya Wakamba, vile vijiti vikahitaji jina la kuvirejelea. Nomino *mĩsyĩ* ilitumiwa kuiwakilisha dhana hiyo mpya na ikapata maana ya pili. Miktadha ya matumizi ikaongezeka.

Hatimaye dhana 'mishale' ilidondoshwa kutoka nomino *mĩsyĩ.* Maana ilihawilishwa hadi kwa nomino *maangi* (katika umoja *ĩangi*). Nomino *maangi* pia ikapewa jukumu la kuwakilisha dhana 'mbegu za uzazi' kwa sababu za kitasfida. Nomino *maangi* vile vile ikapanuka maana.

### 4.2.3 Ubanaji wa Maana

Ubanaji wa maana ni hali ambapo maneno hupoteza maana zake za jumla na kurejelea maana zilizo bayana zaidi kuliko zamani (Campbell, 2004). Neno ambalo awali liliwakilisha dhana pana hudondosha baadhi ya dhana na kuwasilisha dhana finyu au moja. Kwa mfano kitenzi cha Kiingereza *starve* kilichotokana na Kiingereza cha zamani (Old English) *steorfan* kilimaanisha *to die* au kufa kutokana na sababu yuyute kama vile uzee, ugonjwa au njaa. Maana ya kitenzi *starve* ilikuwa pana au ya jumla. Hatimaye kilipata ubanaji wa maana kikawa kinarejelea *die of hunger* (kufa kwa njaa pekee). Maana hii ni bayana. Katika utafiti huu kuna maneno kumi na sita (16) ambayo yamebadilika maana kupitia mchakato wa ubanaji. Nomino kumi na moja (11) na vitenzi vitano (5). Idadi hii ni asilimia thelathini (32%) ya jumla ya maneno hamsini (50). Nomino zilizosambaratika ni *asa*, *ĩkanga, isamũ, mũsikalĩ, syĩndũ, mata*, *ũta*, *mĩsyĩ*, *maangi*, *mwĩai* na *mũtumĩa*.

Nomino *asa* ilikuwa na maana mbili ambazo wazee walitueleza; ‘mzazi wa kiume’ na ‘Mungu’. Kwa mujibu wa watoto nomino hii ilikuwa na maana moja; ‘Mungu’. Dhana ‘mzazi wa kiume’ ilidondoshwa ikabaki dhana moja.

Nomino *ĩkanga* ilirejelea dhana mbili. Dhana moja ni ‘askari’ na ya pili ni ‘mtu anayepakia abiria garini’. Watoto walifahamu maana moja, ‘mtu anayefanya kazi ya kupakia abiria garini’. Dhana moja ilidondoshwa ikabaki moja. Nomino hii ambayo ilikuwa na dhana pana imebadilika kuwa na dhana finyu.

Nomino *isamũ* ilikuwa na maana tatu; mali au utajiri, vitu vya aina yoyote na sehemu za siri. Watoto wawili (20%) waliitambua maana ‘sehemu za siri’. Maana nyinginezo zilidondoshwa.

*Mũsikalĩ* ni nomino iliyorejelea dhana mbili; 'afisa wa kulinda usalama wa nchi' na 'mlinda lango'. Watoto waliifahamu maana moja ya nomino hii 'afisa wa kulinda usalama wa nchi'. Katika Kiswahili ni 'askari'. Maana za nomino hii zimepungua.

Nomino *syĩndũ* ilitumiwa kurejelea 'mali au utajiri alio nao mtu'. Maana ya pili ilikuwa 'vitu vya aina nyingine yoyote'. Watoto walitambua maana moja kati ya hizo mbili, 'vitu vya aina yoyote'. Maana imebanwa.

Nomino *mata* ilikuwa na maana mbili. Maana moja ni 'kiowevu kitokacho kinywani' au 'mate' katika Kiswahili. Maana nyingine ni 'zana ya vita itumiwayo kurushia mishale'. Watoto hawakufahamu maana 'zana ya vita'. Walisema maana ya nomino hii ni 'kiowevu kinachotoka kinywani' ambacho huitwa 'mate' kwa lugha ya Kiswahili. Nomino hii ilidondosha maana moja.

*Uta* maana yake ni 'zana ya vita inayotumiwa kurushia mishale'. Pia ni 'mate membamba yanayotoka kinywani hasa wakati mtu anapolala usingizi'. Mahojiano ya watoto yalibainisha maana moja ya nomino hii, 'zana ya vita inayotumiwa kurushia mishale' au 'upinde'. Nomino hii imebaki na maana moja.

Aidha, nomino *mĩsyĩ* imepoteza maana moja. Kwa mujibu wa wazee nomino hii ilikuwa na maana mbili, 'zana za vita zinazoundwa kwa chembe na vijiti' au 'mishale' na 'njiti za kiberiti'. Maana iliyofahamika na watoto ni 'njiti za kiberiti'. Maana nyingineyo hawakuijua.

Nomino *maangi* ilikuwa na maana mbili. Maana moja ni 'zana za vita zilizoundwa kwa chembe na vijiti'. Maana nyingine ni ya kiistiari; 'mbegu za kiume za uzazi'. Watoto walifahamu maana moja 'zana za vita zinazoitwa mishale'. Maana ya pili imedondoshwa na haipo katika msamiati wao.

*Mwĩai* ni nomino ya kipolisemia na maana zake zilikuwa tatu; Mungu, mume na mtu mwenye mamlaka. Watoto walifahamu maana moja, 'Mungu'. Maana nyinginezo mbili hawazifahamu. Nomino hii imedondosha maana mbili na sasa inawakilisha dhana finyu.

Nomino *mũtumĩa* awali ilikuwa na maana mbili. Maana ya kwanza ni 'mtu yeyote aliyezeeka, awe mwanamume au mwanamke'. Maana ya pili ilikuwa 'mume wa mtu'. Watoto walifahamu maana moja mpya 'mwanamume mzee'. Maana zote asilia zilidondoshwa. Aidha, maana imefinyika kwa kuwa sasa inarejelea 'mtu wa jinsia ya kiume pekee ambaye amezeeka' badala ya mtu yeyote aliyezeeka.

Vitenzi vitano (5) viliathiriwa na ubanaji wa maana; *semba*, *kwatwa*, *milwa*, *vikĩla* na *vuta*. Kitenzi *semba* kilikuwa na maana mbili ambazo wazee walitupatia; kimbia na toroka. Maana ambayo watoto walifahamu ni moja, kimbia. Kitenzi hiki kilidondosha maana moja.

*Kwatwa* ni kitenzi cha Kikamba cha zamani ambacho kilikuwa na maana nne; 'kamatwa hasa na polisi', 'lewa kutokana na kunywa mvinyo', 'kupatwa kwa mwezi au jua' na 'kutendewa dhuluma za kimapenzi au ngono'. Watoto waliohojiwa walitambua maana moja, 'kamatwa na polisi'. Maana ya kitenzi *kwatwa* sasa imebanwa.

*Milwa* ni kitenzi ambacho kilikuwa na maana mbili. Maana moja ni 'lewa kutokana na kunywa mvinyo' na maana ya pili ni 'kuwa katika hali ya kutojifahamu kwa kuzidiwa na furaha au majonzi'. Maana ambayo watoto waliifahamu ni 'lewa kutokana na kunywa mvinyo au pombe'. Maana ya pili imedondoshwa.

Kitenzi kingine kilichopitia mchakato wa ubanaji ni *vikĩla*. Wazee walisema kwamba kilikuwa na maana mbili. Maana hizo ni 'fuata' na 'weza kugusa kitu kilicho mbali'.

Watoto waliitambua maana moja ‘weza kugusa kitu kilicho mbali’. Maana ya kwanza ilidondoshwa na sasa kitenzi hiki kina maana moja.

Kitenzi cha mwisho katika kategoria hii ni *vuta*. Maana zake zilikuwa tatu; nyang’anya, achisha mtu kazi na ondoa maandishi. Watoto walifahamu maana mbili za kitenzi hiki; achisha mtu kazi na ondoa maandishi. Maana moja haikujulikana miongoni mwa watoto.

### 4.2.4 Usambaratikaji wa Maana

Usambaratikaji wa maana ni mchakato ambapo neno lililokuwa na maana chanya hubadilika na kuwa na maana hasi au duni. Pia huitwa udhalilikaji au msawajiko wa maana (Massamba 2004).

Usambaratikaji wa maana unatokea pale ambapo msamiati hubadilika na kuanza kuhusishwa na masuala duni hivyo kupunguza ukubalikaji wake katika mazungumzo (Crystal, 2003).

Maana ya neno ambayo ilikuwa chanya hubadilika na kuwa hasi. Kwa mfano nomino *toilet* ilimaanisha ‘kitambaa cha meza’. Baadaye ikaanza kutumiwa badala ya nomino ya Kiingereza *lavatory* yenye maana ‘mahali pa kujisaidia au choo’. Mabadiliko haya yalisababishwa na uwepo wa miiko kama vile kutotaja sehemu za kufanya haja, kwa hivyo neno *toile*t likatumiwa kitasfida. Kutokana na kurejelea mahali pa kujisaidia, nomino hii ilisambaratika (Crystal, 2003).

Katika utafiti wetu, nomino nne (4) *isamũ, kĩmũtũ, manzĩ* na *mwenyu* zilisambaratika maana. Nomino *isamũ* ilikuwa na maana tatu; mali au utajiri, vitu vya aina yoyote na sehemu za siri. Asilimia themanini (80%) ya watoto waliohojiwa haikufahamu maana.

Asilimia ishirini (20%) ya watoto ilifahamu maana ‘sehemu za siri’. Nomino hii ilikuwa na maana hasi miongoni mwa watoto.

Nomino *kĩmũtũ* awali ilimaanisha ‘aina ya mkate ambao uliokwa baada ya unga kuwekwa kwa muda ili uumuke na kupata ladha ya chachu’. Watoto walisema kuwa maana yake ni 'chakula kibaya au chakula ambacho hakikuiva vizuri'. Maana hii ni duni.

Maana asilia ya nomino *manzĩ* ni kiowevu kinachonywewa ili kukata kiu. Maana ya pili ni 'maji yanayobeba mbegu za kiume za uzazi' au 'shahawa'. Watoto wote (100%) waliotafitiwa hawakufahamu maana ya nomino hii. Nomino hii ilibeba maana moja duni inayorejelea sehemu za uzazi na ni mwiko katika jamii ya Wakamba kutaja sehemu za uzazi au vitu vyovyote vinavyohusiana na sehemu hizo. Kwa hivyo nomino hii imesambaratika maana na haitumiwi katika muktadha wa mazungumzo ya kawaida miongoni mwa watoto.

Nomino *mwenyu* awali ilitumiwa kurejelea ‘mama’ katika mazungumzo ya kawaida. Wazee walithibitisha hayo. Kati ya watoto wote kumi (10) waliohojiwa, tisa (9) walisema kwamba neno hilo lilikuwa la matusi. Hakuna aliyeeleza maana ya nomino hii. Maana ya nomino hii imesambaratika. Usambaratikaji umeathiri asilimia nane (8%) ya jumla ya maneno hamsini (50) yaliyochunguzwa.

### 4.2.5 Uimarikaji wa Maana

Uimarikaji wa maana ni mabadiliko ya maana ambayo yana thamani chanya (Traugott, 2002). Uimarikaji hutokea iwapo neno lililokuwa na maana hasi au duni hubadilika maana ikawa chanya au nzuri (Glassman, 2011). Kwa mfano, maana asilia ya nomino ya Kihispania *casa* ilikuwa *hut* (kichuguu) au *cottage* (nyumba ndogo). Maana ya nomino hiyo sasa ni *house* (nyumba) au *dwelling* (makao). Kivumishi *nice* awali

kilimaanisha *foolish* au mjinga. Katika Kiingereza cha sasa kivumishi *nice* kinarejelea dhana –*zuri* (Anttila,1989).

Kati ya maneno hamsini (50) tuliyoteua kama data ya utafiti wetu, kitenzi kimoja (1) *kwatwa* ndicho kilichoimarika maana. Idadi hii ni asilimia mbili (2%). Maana za kitenzi hiki zilikuwa nne; kamatwa na polisi, lewa kwa kunywa mvinyo, kushikwa kwa jua au mwezi na dhulumiwa kingono. Maana moja ya kitenzi hiki 'dhulumiwa kingono' ilikuwa hasi. Mabadiliko ya kisemantiki yalipotokea, kitenzi hiki kilibaki na maana moja; 'kamatwa na polisi'. Maana hasi ilidondoshwa na kusababisha uimarikaji wa maana.

## 4.2.6 Tasfida

Tasfida ni mchakato wa mabadiliko ya maana unaorejelea matumizi ya lugha ya heshima badala ya kutumia moja kwa moja lugha ya matusi au yenye kukera ili kuficha ukali wa maneno na kufunika aibu (Gichuru, 2020). Kwa mfano nomino 'ngono' ilikuwa na maana ya 'usingizi'. Ili kuficha aibu ya kutaja tendo la kujamiiana, nomino 'ngono' ikatwikwa jukumu la kuiwakilisha dhana hiyo. Matumizi ya nomino hii kuficha aibu ya kitendo cha kujamiiana yaliifanya kusambaratika au kupata maana duni.

Miongoni mwa data ya utafiti wetu, maneno matatu (3) yalitumiwa kitasfida. Idadi hii ni asilimia sita (6%) ya jumla ya maneno hamsini (50). Nomino *isamũ* awali ilimaanisha 'vitu vya thamani alivyo navyo mtu au utajiri'. Pia ilirejelea aina yoyote ya vitu kama vile nguo, viatu, redio, vikombe na mavuno kutoka shambani. Kutokana na aibu ya kutaja sehemu za siri, nomino *isamũ* ilitwikwa jukumu la kuwakilisha 'sehemu za siri'. Hivyo ndivyo nomino hiyo ilivyopata maana za kipolisemia. Baada ya

kuwahoji watoto, ilibainika kuwa asilimia ishirini (20%) ya watoto ilifahamu maana ‘sehemu za siri’.

Nomino *maangi* ilitumiwa katika B2 ili kubeba dhana ‘zana za vita’ ambayo ilidondoshwa kutoka kwa nomino *mĩsyĩ.* Hatimaye mbegu za kiume za uzazi zilipewa jina *maangi* ili kuficha aibu ya kuzitaja hadharani. Nomino *maangi* ikapanuka maana.

*Kwatwa* ni kitenzi cha Kikamba chenye maana ‘lewa’ katika muktadha wa Biblia ya 1974. Kitenzi hiki kimepata maana zaidi katika muktadha wa wazee. Kutokana na aibu ya kutaja kitendo cha ngono hadharani, wazee walikitwika kitenzi *kwatwa* jukumu la kuwakilisha dhana ya ‘kukamatwa na kutendewa tendo la ngono bila hiari’. Kwa hivyo kitenzi hiki kiliongezewa maana ya kitasfida.

### 4.2.7 Utowekaji wa Maana

Utowekaji wa maana ni hali ambapo matumizi ya neno fulani husitishwa kabisa (Abuga, 2013). Aidha, dhana yenyewe iliyorejelewa na neno hilo hutoweka. Baadhi ya dhana zinaweza kutoweka kabisa katika jamii kutokana na kupitwa na wakati. Kwa mfano, katika lugha ya Ekegusii, nomino iliyotumiwa kurejelea ‘kibuyu’ ni *ekerandi*. Aina hii ya kibuyu haipo tena katika jamii na nomino yenyewe imetoweka. Neno *esoreti* limekopwa kutoka lugha ya Kinandi kurejelea kibuyu ambacho hutumiwa siku hizi.

Katika lugha ya Kikamba, kuna maneno yaliyobadilika maana kutokana na mchakato huu. Neno *kĩĩnga* lilitumiwa kuashiria aina ya kikapu kilichotumiwa zamani kuhifadhia nafaka. Sasa hivi nafaka huhifadhiwa katika *ĩkumbi* yaani ghala. Neno ‘kĩĩnga’ limetoweka pamoja na kifaa chenyewe. Utafiti wetu ulibainisha nomino tatu (3) zilizopitia mchakato huu: *ĩlawa*, *ĩmisi* na *mathatwa*. Idadi hii ni asilimia sita (6%) ya jumla ya maneno hamsini (50).

Maana asilia ya nomino *ĩlawa* ilikuwa aina ya mkate uliookwa baada ya unga kukandwa na kuachwa kwa muda ili uumuke na kupata ladha ya chachu. Hii ndiyo ilikuwa mbinu ya asili ya uokaji. Mbinu hii imepitwa na wakati na haitumiki tena. Nomino *ĩlawa* haitumiki tena katika mazungumzo.

*Imĩsĩ* ni shuka nyeusi iliyotumiwa kusetiri vitu na kudumisha faragha katika nyumba. Matumizi yake katika jamii yamepitwa na wakati. Kuna njia za kisasa za kudumisha faragha na vitu visivyofaa kuonekana na wageni huhifadhiwa katika makabati na mashubaka. Nomino yenyewe pia haitumiwi katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii.

Nomino *mathatwa* pia imetoweka. Wazee walitueleza kwamba hii ni mifuko iliyoshonwa kwa kutumia ngozi ya mnyama. Mifuko hii ilitumiwa kuhifadhia asali na mvinyo. Katika karne hii ya ishirini na moja (21) asali huhifadhiwa katika ndoo na chupa. Mvinyo huhifadhiwa katika vyombo maalum kama vile chupa na mitungi. Mifuko ya aina hii haipo tena na nomino yenyewe haitumiki katika mazungumzo. Nomino tatu zilizotajwa hapa hupatikana katika vitabu vya Kikamba cha kale kama vile Biblia iliyochapishwa mwaka 1974.

### 4.2.8 Kuhamisha maana

Nabhany (1982) anasema kwamba huu ni mchakato ambapo maana ya neno huhawilishwa kwa neno jingine ambalo tayari linatumiwa katika lugha, kisha neno lililohamisha maana hutoweka (Kresse, 2007)). Dhana ya zamani hubaki huku ikiwakilishwa na umbo jingine tofauti. Umbo hili linaweza kuwa limekopwa kutoka lugha nyingine, likawa limeundwa na wanajamii au likachukuliwa kutoka msamiati ambao tayari unatumika. Kwa mfano, zifuatazo ni leksia katika lugha ya Kiswahili zilizotoweka na dhana zikahawilishwa kwa maneo mengine:

| Kikale | Kisasa |
|---|---|
| Gongwa | Ikulu |
| Ng'andu | Dhahabu (Nabhany,1982) |

Katika utafiti wetu tuligundua neno moja ambalo lilihamisha maana. Nomino *ĩthweo* ilimaanisha mkusanyiko wa matone ya mvua yaliyoganda katika angahewa. Mkusanyiko huu huitwa 'wingu'. Ilibainika kuwa nomino hii iliihawilisha maana yake kwa nomino *ĩtu* ambayo awali ilirejelea 'mahali palipo juu zaidi ambapo huaminika ndipo makao ya Mungu'. Nomino *ĩtu* ikapata maana ya ziada, nayo nomino *ĩthweo* ikatoweka. Maneno yaliyohamisha maana katika utafiti wetu yalikuwa asilimia mbili (2%).

Kulingana na utafiti wetu, mchakato wa ubanaji ndio mbinu kuu ya kubadilika kwa maana za nomino na vitenzi katika lugha ya Kikamba. Maneno yaliyobadilika maana kutokana na mchakato huu ni asilimia thelathini na mbili (32%) ya jumla ya maneno hamsini (50). Michakato mingineyo imeathiri maneno yaliyochunguzwa kwa kiwango kilicho chini ya asilimia kumi (10). Muhtasari wa michakato ya kisemantiki iliyosababisha mabadiliko ya maana katika utafiti wetu umewekwa katika jedwali kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.7: Muhtasari wa michakato ya Kisemantiki katika Nomino na Vitenzi**

| Michakato ya Kisemantiki | Kiwango (%) | Nomino | Vitenzi |
|---|---|---|---|
| Upanuzi | 8 | Ũkũngi | Hakuna |
| | | Kĩmũtũ | |
| | | Mĩsyĩ | |
| | | Maangi | |
| Ubanaji | 32 | Asa | Kwatwa |
| | | Ĩkanga | Milwa |
| | | Maangi | Nyala |
| | | Manzĩ | Semba |
| | | Mata | Vikila |
| | | Mĩsyĩ | Vuta |
| | | Mũsikalĩ | Hakuna |
| | | Ũta | |
| | | Mũtumĩa | |
| | | Mwĩai | |
| Usogezi wa kisitiari | 6 | Asa | Hakuna |
| | | Ukũngi | |
| | | Mĩsyĩ | |
| Usogezi wa kisinedoche | 4 | Ndũa | Hakuna |
| | | Mũsyĩ | |
| Usambaratikaji | 8 | Kĩmũtũ | Hakuna |
| | | Manzĩ | |
| | | Isamũ | |
| | | Mwenyu | |
| Uimarikaji | 2 | | Kwatwa |
| Tasfida | 6 | Isamũ | Kwatwa |
| | | Maangi | |
| Utowekaji wa maana | 6 | Ĩlawa | Hakuna |
| | | Ĩmisi | |
| | | Mathatwa | |
| Kuhamisha maana | 2 | Ĩthweo | Hakuna |

Jedwali hili linatupatia taswira ya michakato mbalimbali ya kisemantiki ambayo ilisababisha mabadiliko ya maana ya nomino na vitenzi tulivyoteua kama data ya utafiti wetu. Kati ya nomino thelathini (30) zilizochunguzwa, nomino ishirini (20) pekee ndizo zilizoathiriwa na michakato ya kisemantiki; nomino zote kumi na tano (15) za B1 na nomino tano (5) za B2. Nomino kumi na tatu (13) kati ya hizo ishirini (20) ziliathiriwa na mchakato mmoja (1) wa mabadiliko, kwa hivyo zimetokea mara moja (1) katika

jedwali. Nomino tano (5) *asa*, *isamũ*, *kĩmũtũ*, *manzĩ* na *ũkũngi* ziliathiriwa na michakato miwili ya mabadiliko, kwa hivyo zote kwa jumla ni kumi (10) katika jedwali. Nomino mbili (2) *mĩsyĩ* na *maangi* ziliathiriwa na michakato mitatu (3) ya kisemantiki, kwa hivyo zimetokea mara sita (6) katika jedwali. Ndiyo maana nomino zote katika jedwali ni ishirini na tisa (29), yaani kumi na tatu (13) jumlisha kumi (10) na sita (6). Nomino nyinginezo kumi (10) za B2 hazikubadilika maana.

Vitenzi ishirini (20) viliteuliwa kama data ya utafiti huu, kumi na vitano (15) kutoka B1 na kumi na vitano (15) kutoka B2. Vitenzi vinne (4) tu vya B1 ndivyo vilibadilika maana. Vitenzi hivyo ni *kwatwa*, *nyala*, *vikĩla* na *vuta*. Kitenzi *kwatwa* kiliathiriwa na michakato mitatu tofauti ya kisemantiki kwa hivyo kilitokea mara tatu katika jedwali. Vitenzi viwili (2) vya B2 ndivyo vilibadilika maana; *milwa* na *semba*. Vinginevyo kumi na vitatu (13) havikubadilika maana. Ingawa jumla ya vitenzi vilivyobadilika maana ni sita (6), kutokana na kujirudia kwa kitenzi *kwatwa* mara mbili zaidi vitenzi hivyo vinaonekana kuwa vinane (8).

Tunaweza kusema kwamba mabadiliko mengi ya maana yamesababishwa na ubanaji wa maana. Mchakato wa ubanaji umeathiri asilimia thelathni na mbili (32%) ya maneno yaliyoteuliwa kama data ya utafiti wetu. Maana za nomino zimebanwa kwa kiwango cha asilimia ishirini (20%) na vitenzi asilimia kumi na mbili (12%). Upanuzi umetokea kwa kiwango cha asilimia nane (8%). Maana zimesogezwa kisitiari kwa asilimia sita (6%) na kisinedoche kwa asilimia nne (4%). Maana zilizosambaratika ni asilimia nane (8%) na zilizoimarika ni asilimia mbili (2%). Ubadilikaji wa maana kutokana na utumiaji wa tasfida umetokea kwa asilimia sita (6%) ya maneno. Maneno ambayo yamekumbwa na utowekaji wa maana ni asilimia sita (6%). Maana zimehamishwa kwa maneno yaliyopo katika jamii kwa asilimia mbili (2%). Ubanaji wa maana umetokea

kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na upanuzi. Hali hii imeathiri msamiati wa lugha ya Kikamba kwa njia hasi kwa kuwa iwapo msamiati utadondosha maana kwa kiasi kikubwa kuliko jinsi unavyopata maana za ziada basi huenda maneno mengi zaidi ya yale tuliyogundua yakatoweka.

## 4.3 Sababu za Mabadiliko ya Maana za Maneno

Maana ya neno inaweza kubadilika katika lugha. Wataalamu mbalimbali kama vile Ullman (1972), Palmer (1996), Blank (1999) na wengine wameeleza sababu mbalimbali za mabadiliko ya maana. Baadhi ya sababu ni za kijamii na nyingine ni za kiisimu. Zifuatazo ni baadhi ya sababu walizojadili wataalamu. Tulijadili tu sababu zilizosababisha mabadiliko ya maana za maneno katika utafiti wetu:

### 4.3.1 Maendeleo ya Jamii

Gichuru (2020) anasema kwamba jamii imeshuhudia maendeleo makubwa hasa upande wa sayansi na teknolojia katika karne hii ya ishirini na moja (21). Dhana na vifaa vipya vimeibuka na vingine vikakosa matumizi kwa kupitwa na wakati. Kutokana na kuibuka kwa dhana mpya, leksia mpya zimebuniwa na nyingine zilizopo katika lugha kutwikwa maana za ziada ili kukidhi mahitaji haya. Kwa mfano neno *ubuye* awali lilitumika kurejelea ‘mchezo wa watoto katika jamii ya Waswahili’. Leo neno hilo hutumika kumaanisha ‘hali ya neno kuwa na umbo ambalo halidokezi maana’ (Massamba, 2004).

Kwa mfano tunaamini kwamba njiti za kiberiti hazikuwa zimesambaa Ukambani katika kipindi cha kuandikwa Biblia ya kwanza ya Kikamba (1956) ambayo ndiyo iliyochapishwa tena mwaka 1974. Baadaye ziliposambaa hadi Ukambani pakawa na uhitaji wa jina la kuzirejelea. Badala ya kuunda msamiati mpya, nomino *mĩsyĩ* ambayo ilirejelea 'mishale' ilitwikwa jukumu la kuwakilisha dhana 'njiti za kiberiti'. Nomino hiyo ikapata upolisemia. Wakati wa kuchapishwa kwa *Mbivilia* (2011), tayari nomino

*mĩsyĩ* ilikuwa imedondosha maana asilia mishale, na dhana hii ikaundiwa jina *maangi*. Aidha, dhana zilizowakilishwa na nomino *mathatwa* na *ĩmisi* zimepitwa na wakati na maana hizo kutoweka.

### 4.3.2 Kupotea kwa motisha ya matumizi

Kupotea kwa motisha ni hali ambapo maana mojawapo ya neno la kipolisemia hutumiwa zaidi kuliko maana nyinginezo (Anusu, 2015). Hali hii hufanya wazungumzaji wa lugha kuzoea maana moja ya neno na kupuuza maana nyinginezo. Maneno yanapoegemezwa kwenye mizizi yao au kwenye fahiwa zake huwa ni mbinu moja ya kudhibiti maana kwa kiwango fulani. Maana moja ya neno ikitumiwa zaidi kuliko maana nyinginezo za neno hilo, maana zisizotumiwa zitakufa (Campbell, 2004).

Katika kipindi fulani, neno *gay* lilikuwa na maana mbili; *joyful* na *homosexual*. Maana hizi mbili zilitumika pamoja hadi pale taratibu wazungumzaji wa lugha ya Kiingereza walianza kuegemea kwenye maana *homosexual* kiasi kwamba maana nyingineyo ilikufa. Nomino 'shoga' katika lugha ya Kiswahili pia ilikuwa na maana mbili; 'rafiki wa kike wa mwanamke' na 'mwanamume anayefanya mapenzi na mwanamume mwingine'. Maana hii ya pili imetumiwa sana katika jamii kiasi kwamba maana ya kwanza inaelekea kupotea.

Katika utafiti huu, nomino *mũtumĩa* ilikuwa na maana tatu. Maana moja ni 'mtu yeyote aliyezeeka, awe mwanamume au mwanamke'. Maana ya pili ni 'mwanamume mzee' na maana ya tatu ni 'mume wa mtu'. Maana moja 'mwanamume mzee' imetumiwa sana katika jamii ya Wakamba kiasi kwamba maana nyinginezo mbili zimepotea katika matumizi. Hakuna anayetaka kurejelea mwanamke mzee kwa nomino *mũtumĩa.* Aidha, siku hizi 'mume' hurejelewa kwa jina lililotoholewa kutoka Kiswahili *mũsee* (mzee) au *mũũme* (mume).

Nomino *asa* awali ilitumiwa kwa maana 'baba'. Baadaye maana hii ilisogezwa kwa Mungu kutokana na sifa za ki-baba za Mungu. Maana za *asa* zikawa mbili kama tulivyoona katika B1 (Mat. 16:17, Lk.15:18). Hatimaye wazungumzaji waliegemea kwenye maana ya pili 'Mungu' zaidi hadi maana asilia ikatoweka katika mazungumzo. Ndiyo maana tuliona maana iliyotoweka haikuwapo katika B2. Sasa hivi katika karne hii ya ishirini na moja (21) nomino *asa* inahusishwa na maana moja 'Mungu' hata katika maandishi. Hali hii inaweza kuchangia kutoweka au kufa kwa maana au msamiati.

### 4.3.3 Upolisemia wa maneno

Polisemia ni neno lenye maana mbili au zaidi zinazokaribiana sana (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2013). Kwa mfano 'kupe' kwa maana ya mdudu na 'kupe' kwa maana ya mtu anayeishi kwa kutegemea wengine. Polisemia ni sifa ya msingi katika mazungumzo ya binadamu ambapo licha ya kuwa na maana zaidi ya moja, maana hizo zina uhusiano (Ullman, 1972).

Maneno kwa kawaida huwa na sifa ya upolisemia kutegemea muktadha (Fromkin n.w, 2014). Neno linaweza kupata maana mpya bila kupoteza maana yake asilia. Kwa mfano nomino ya Kiingereza *mouth* (kinywa) ilikuwa na maana 'sehemu ya mwili iliyo kichwani ambayo hutumiwa kulia chakula na kutamkia sauti'. Nomino hii pia ilipata maana 'sehemu katika bahari au ziwa ambapo mto huingizia maji yake'. Kutokana na sifa hii ya lugha, maneno hubadilika maana kulingana na jinsi yanavyotumiwa. Maneno mengi katika lugha ya Kikamba ni ya kipolisemia. Kwa mfano maana asilia ya kitenzi cha Kikamba *ya* ni 'tia kitu kinywani na kukimeza'. Hata hivyo kimepata maana nyingine tofauti. Kwa mfano mtu anaposema, 'Nina<u>ya</u> milioni!' (nimekula milioni) ni vigumu kubaini maana ya kauli hii. Anaweza kumaanisha ametumia shilingi milioni

zikaisha au ameshinda katika mchezo fulani akapewa shilingi milioni. Maana asilia ya kitenzi *ya* imehawilishwa hadi kwenye vitendo vingine visivyohusiana na kutia kitu kinywani na kumeza.

Utafiti wetu uligundua maneno ishirini na tisa (29) ambayo yalikuwa na upolisemia (katika B1 na B2). Idadi hii ni asilimia hamsini na nane (58%) ya jumla ya maneno yaliyochunguzwa. Maneno hayo yamekuwa yakipokea maana za ziada kadiri wakati unapopita ili kukidhi uhitaji wa maana unaozuka katika jamii. Kwa mfano, nomino *ĩtu* ambayo ilikuwa na maana 'mahali juu anapoishi Mungu', ilitwikwa jukumu la kuwakilisha dhana 'wingu'. Maana ya nomino hii ilipanuka. Maana hizi mbili zinahusiana kwa kuwa 'wingu' huonekana huko juu mbinguni.

Maana za kipolisemia husababisha utata wa maana iwapo muktadha wa mazungumzo hautakuwa bayana. Ili kuondoa utata huo wa maana, kunatokea mtawanyiko wa maana huku kila dhana ikichukua neno lenye umbo tofauti. Hatua hii ya kuondoa utata wa maana husababisha kudodoshwa kwa baadhi ya maana za neno. Kwa mfano nomino *asa* ambayo awali ilirejelea 'baba' na 'Mungu' ilidondosha maana 'baba' na utata ukaondoka. Sasa hivi nomino *asa* ikitajwa inaeleweka kwamba anayerejelewa ni Mungu.

### 4.3.4 Ukuruba wa maana

Ukuruba ni ukaribiano wa dhana mbili kimaana. (Blank, 1999). Ujirani au mfanano wa dhana mbili kimaana unaweza kusababisha mabadiliko ya maana. Iwapo dhana moja kati ya zile zinazofanana ni duni, basi dhana nyingineyo itapata mwelekeo hasi miongoni mwa watumiaji lugha. Mfanano uliowekwa na Wakamba baina ya dhana mbili 'maji' na 'shahawa' ulisababisha kusambaratika kwa nomino *manzĩ*. Nomino *kĩw'ũ* ikaundwa ili kuwakilisha dhana 'maji'. Nomino *kĩw'ũ* pia iliathirika ikapata maana

ya ziada kutokana na mfanano wa maji na kiowevu kinachotoka mwilini kwa mfano kutoka kwenye jipu (usaha) au katika baadhi ya miti.

Mfanano wa kisifa baina ya 'baba mzazi' na 'Mungu' ulisababisha upanuzi wa maana ya nomino *asa*, ikawa inarejelea baba mtu na Mungu. *Ũkũngi* (upepo mwanana) hubeba makapi na makapi huwa ndani ya upepo. Mfanano huu ndio uliofanya watoto wawili (2) kusema kuwa maana ya *ũkũngi* ni uchafu utokao kwenye nafaka. Maana hii ikidumishwa na kurithishwa, basi nomino hii itakuwa imepata upanuzi wa maana. Aidha, njiti za kiberiti zina mfanano na mishale. Mfanano huu ulisababisha upanuzi wa maana ya nomino *mĩsyĩ* ili kurejelea njiti za kiberiti. Vilevile, mfanano unaweza kuhusu kitu kuwa sehemu ya kingine. Kijiji ni sehemu ya mji. Uhusiano huu ndio uliosababisha maana ya nomino *ndũa* kusogezwa kutoka mji hadi kijiji. Vile vile nomino *ĩthweo* na *ĩtu* zina mfanano. Nomino *ĩthweo* ilitumiwa kurejelea wingu nayo nomino *ĩtu* ilirejelea 'mbingu'. Wingu hupatikana mbinguni. Hata wsakati mwingine inasemekana Mungu huishi mawinguni. Hakuna mpaka bayana wa tofauti ya maana za nomino hizi mbili. Ndiyo sababu maana ilihamishwa kutoka kwa *ĩthweo* hadi kwa nomino *ĩtu*.

### 4.3.5 Maneno Mwiko katika Jamii

Mwiko ni makatazo ya kijamii dhidi ya maneno, vitu, matendo ama watu ambao hawapendezi kwa kundi la watu, utamaduni au jamii (Ullman, 1972). Maneno mwiko ni maneno ambayo yanahusishwa na matendo au vitu mwiko. Kwa mfano maneno ya kuapa, maneno yanayohusu ngono na kazi zinazotekelezwa na sehemu za mwili kama vile 'kunya'.

Uwepo wa maneno mwiko katika jamii husababisha mabadiliko ya maana za maneno (Palmer, 1996). Katika jamii ya Wakamba, baadhi ya maneno ni mwiko. Kwa mfano kutaja jina la mkwe au la mkaza mwana, kutaja jina la aliyekufa na kutaja sehemu za

uzazi. Ili kuficha aibu na kuepuka maana hasi inayotokana na kuyataja maneno hayo, jamii huchukua maneno yaliyo katika lugha yakapata maana za ziada. Neno ambalo ni mwiko hukoma kutumiwa katika jamii na mara nyingi hufa. Mfano ni nomino *isamũ* ambayo maana yake ilikuwa 'utajiri alio nao mtu' au 'vitu vya aina yoyote'. Nomino hii ilitwikwa jukumu la kuwakilisha dhana 'sehemu za siri'. Pia, nomino ambayo hutwikwa jukumu la kuwakilisha dhana mwiko hupata maana hasi baada ya kutumiwa kwa muda. Kwa sasa nomino *isamũ* imesambaratika maana na wanajamii hasa watoto wa karne hii ya ishirini na moja (21) hawapendi kuitaja. Vile vile nomino *manzĩ,* baada ya kupata maana moja mwiko, 'shahawa', ilisambaratika na sasa watu hawaitumii katika mazungumzo ya kawaida. Kwa hivyo kuwepo kwa maneno mwiko katika jamii kulisababisha mabadiliko kama vile ubanaji, upanuzi, usambaratikaji wa maana na kutoweka kwa umbo lililowasilisha maana.

## 4.3.6 Uzalishaji wa maana potovu

Ullman (1972) anasema kwamba daima lugha hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Watoto hujifunza lugha katika jamii. Wanapokua wanaweza kuelewa maana zilizo tofauti. Wakikosa kurekebishwa patatokea mabadiliko ya kisemantiki katika kizazi kipya. Wao pia wanaweza kuwapokeza wana wao maana zenye makosa. Hatimaye maana potovu zitazalishwa katika jamii. Katika mahojiano na watoto kumi, ilibainika kuwa maneno *ĩlawa*, *ĩmisi*, *meta*, *thilĩka* na *ya ĩvu* yalipewa maana potovu, iliyo mbali sana na maana asilia au mzizi. Kitenzi *nyala* pia kilizua utata wa maana. Kitenzi mbadala ni *ĩw'a nzaa*. Maana yake katika Kiswahili ni 'ona njaa'. Wazee wote (100%) walikubaliana kuwa maana ya kitenzi hiki ilikuwa 'tokwa na jasho'. Hakuna hata mmoja aliyetupatia maana 'ona njaa'.

### 4.3.7 Unasibu wa alama za Kiisimu

Alawadi (2020) akimnukuu Ferdinand de Saussure katika anasema kwamba unasibu ni hali ya kutokuwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya alama ya kiisimu na kinachorejelewa. Kwa mfano maneno 'dada', mama, kaka, kata na mita hayana uhusiano wa moja kwa moja na vitu vinavyorejelewa. Alama hizi za maandishi ni nasibu kwa kuwa kuzuka kwake ni kutokana na mazoea ya watumiaji kuendelea kutumia alama hizo katika mawasiliano.

Uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa waweza kubadilika wakati wowote. Kiashiria chochote chaweza kutumika kuashiria kitu chochote katika ulimwengu halisi. Kwa mfano alama ya msalaba (+) inaweza kutumiwa kanisani au katika reli kuleta maana tofauti. Kwa kuwa alama za kiisimu ni nasibu, zinaweza kutumiwa katika miktadha mbalimbali kwa maana tofauti.

Utafiti wetu uligundua maneno matatu (3) ambayo yalibadilika maana kutokana na unasibu kati ya kiashiria na kiashiriwa. Kwa mfano kitenzi *nyala* chenye maana ya 'kutokwa na jasho' kilitumiwa kuashiria 'kuhisi njaa'. Utafiti wetu umebainisha kwamba dhana inayorejelewa katika karne hii ya ishirini na moja (21) ni 'kutokwa na jasho'. Nomino *mwenyu* ilitumiwa kabla ya karne ya ishirini na moja (21) kurejelea 'mama'. Katika karne hii ya ishirini na moja (21), uhusiano baina ya nomino *mwenyu* na dhana 'mama' umebadilika. Nomino hiyo haitumiwi tena kurejelea 'mama'. Aidha, uhusiano kati ya kiashiria *ĩkanga* na kiashiriwa 'askari' umebadilika. Nomino *ĩkanga* sasa inarejelea 'mtu anayefanya kazi ya kupakia abiria garini'. Alama hizi za kiisimu *nyala*, *mwenyu* na *ĩkanga* zilibainisha unasibu wa alama za kiisimu, unasibu ambao ulisababisha mabadiliko ya maana za maneno.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imechanganua mabadiliko ya maana ya baadhi ya nomino na vitenzi katika lugha ya Kikamba. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa maana za maneno katika lugha ya Kikamba zimebadilika. Michakato ya mabadiliko ya maana imebainishwa. Michakato hiyo ni pamoja na upanuzi, ubanaji, usogezi, usambaratikaji, uimarikaji, uhamishaji maana na utowekaji. Mchakato ulioathiri maneno haya kwa kiasi kikubwa ni ubanaji wa maana. Maana zilizodondoshwa na maneno ya B1 zilihawilishwa hadi kwenye maneno mengine katika lugha. Kwa mfano nomino *ĩthweo* ilidondosha maana yake ya pekee 'wingu' ikahamishwa kwa nomino nyingine *ĩtu* ambayo awali ilikuwa na maana moja.

Mwisho sababu za mabadiliko hayo zilizoangaziwa ni za kiisimu pamoja na za kijamii. Sababu hizo ni mahitaji ya maana mpya, upolisemia wa maneno, kuwepo kwa maneno mwiko, lugha kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, kupotea kwa motisha, mfanano wa dhana mbili tofauti na unasibu wa alama za kiisimu. Hata hivyo ilikuwa vigumu kubaini sababu ya mabadiliko ya baadhi ya maneno kwa kuwa yalibadilika kutokana na sababu kadhaa.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti kutoka sura ya kwanza hadi ya nne. Matokeo ya utafiti huu pia yameangaziwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Aidha, tumeshughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti uliofanywa kuhusu mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba. Mapendekezo yametolewa kwa ajili ya watafiti wengine na wataalamu wa isimu hasa katika nyanja za semantiki.

Utafiti huu umechunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba. Tumechunguza maana za maneno kwa mujibu wa maelezo ya wazee na kuwahoji watoto ili kuchunguza iwapo walifahamu maana na iwapo maana za maneno zilibadilika. Tumejadili michakato ya kisemantiki ambayo imechochea mabadiliko. Aidha, sababu za mabadiliko hayo zimejadiliwa. Matokeo ya utafiti yamechanganuliwa na kuelezwa kwa kuzingatia nadharia ya dhana na ile ya nyanja za kisemantiki.

## 5.1 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti wetu yamedhihirisha kuwa maneno yaliyoteuliwa yalipitia mabadiliko ya kisemantiki. Maneno hayo yalikuwa nomino na vitenzi vya Kikamba. Malengo miwili ya kwanza yalihusu kutambua nomino na vitenzi vilivyobadilika maana na kubainisha mabadiliko hayo. Utafiti ulitambua maneno hamsini (50) ambayo yamebadilika maana, nomino thelathini (30) na vitenzi ishirini (20). Nomino zilizoteuliwa kutoka B1 zilikuwa kumi na tano (15); *asa, ĩkanga, ĩlawa, ĩmisi, ĩsamũ, ĩthweo, kĩmũtũ, manzĩ, mata, mathatwa, mĩsyĩ, mwenyu, mwĩai, ũkũngi* na *ndũa*. Nomino kutoka B2 zilikuwa kumi na tano (15) pia; *ĩthe, mũsikalĩ, mbota, mbisũ, syĩndũ,*

*ĩtu, mũkate, kĩw'u, ũta, ikuu, maangi, inyia, mũtumĩa, kĩseve* na *mũsyĩ.* Vitenzi kutoka B1 vilikuwa kumi; navyo ni *kũka, kwatwa, meta, mumunya, nyala, tambũka, thilĩka, vikĩla, vuta* na *ya ĩvu*. Navyo vitenzi vilivyoteuliwa kutoka B2 ni kumi pia*; semba, milwa, ĩthĩwa na kyeva, kumbatĩlya, ĩw'a nzaa, tembea, thata, atĩĩa, vena*, na *itava*. Mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti, wazee na watoto yamethibitisha kuwa maneno yaliyoteuliwa yalibadilika maana. Majibu ya wazee yamedhihirisha kwamba walizitambua nomino zote na vitenzi vyote vya Kikamba cha kale na maana zake. Watoto walitatizika kutambua maana za nomino na vitenzi vya B1.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kutathmini michakato ya kisemantiki iliyosababisha mabadiliko ya maana ya maneno katika lugha ya Kikamba. Tumegundua kuwa michakato tisa (9) ilihusika katika mabadiliko ya maneno teule katika utafiti huu. Michakato hiyo ni upanuzi, ubanaji, sitiari, sinedoche, tasfida, usambaratikaji, uimarikaji, kuhamisha maana na kutoweka maana. Mchakato mkuu uliohusika katika utafiti huu ni ubanaji. Ilibainika kwamba maneno kumi na sita (16) yamebadilika kutokana na ubanaji wa maana, nomino kumi (20%) na vitenzi sita (12%). Idadi hii ni asilimia thelathini na mbili (32%). Nomino zilizobanwa maana ni *asa*, *ĩkanga, maangi, manzĩ, mata, mĩsyĩ, mũsikalĩ, ũta, mũtumĩa* na *mwĩai*. Vitenzi vilivyobanwa maana ni *kwatwa, milwa, nyala, semba, vikĩla na vuta*.

Ni asilimia nane (8%) ya maneno ilipitia upanuzi wa maana. Maneno hayo ni *ũkũngi, kĩmũtũ, mĩsyĩ na maangi*. Kutokana na majibu ya watoto, maneno haya yamepata maana pana. Aidha, usambaratikaji ulitokea kwa asilimia nane (8%) ya maneno. Maneno hayo ni *isamũ, kĩmũtũ, manzĩ* na *mwenyu*. Maneno yaliyosambaratika maana yalipata maana hasi na wazungumzaji wa lugha kuepuka kuyatumia. Maana ziliimarika kwa kitenzi *kwatwa* na idadi hii ni asilimia mbili (2%) ya maneno. Mchakato wa sinedoche uliathiri

asilimia nne (4%) ya maneno. Maneno katika kategoria hii ni *ndũa* na *mũsyĩ*. Mchakato mwingine ni usogezi wa kisitiari ambao ulibainika kwa asilimia sita (6%) katika nomino *asa, ũkungi* na *mĩsyĩ*.

Maneno matatu (3) yalibadilika kutokana na sababu ya kitasfida. Maneno hayo ni nomino *isamũ, maangi* na kitenzi *kwatwa.* Kwa mfano utafiti umebaini kuwa nomino *isamũ* pia imekuwa mwiko kwa kuwa ni asilimia kumi pekee (10%) ya watoto ambayo iliandika maana. Wengine (90%) hawakuandika kutokana na kutojua maana au kuchelea kuandika maana hiyo. Uhamishaji wa maana ulidhihirika kwa nomino moja (1); *ĩthweo*. Hii ni asilimia mbili (2%). Aidha, utowekaji wa maana ulitokea kwa maneno matatu (3) ambayo yaliwakilisha dhana zilizopitwa na wakati na zikakoma kutumika katika jamii. Maneno hayo ni *ĩlawa*, *ĩmisi* na *mathatwa*. Idadi hii ni asilimia sita (6%).

Kwa mujibu wa uchanganuzi wa majibu ya watoto, ilibainika kuwa watoto walikuwa na ufahamu mdogo sana wa maana asilia za maneno yaliyoteuliwa kutoka B1. Watoto hawakuweza kutambua maana asilia za nomino nane (8) kati ya zile kumi na tano (15) zilizoteuliwa kutoka B1 na hiyo ni asilimia hamsini na tatu (53%). Nomino hizo ni *ĩthweo, ĩmisi, kĩmũtũ, manzĩ, mathatwa, mwenyu, ũkũngi na ĩlawa.* Aidha, walikuwa na utata kutambua maana za vitenzi saba (7) kati ya kumi (10) vya B. Idadi hii ni asilimia sabini (70%). Vitenzi hivyo ni *mumunya, meta, tambũka, thilĩka, vikĩla, vuta* na *ya ĩvu*.

Kabla ya kufanya utafiti huu, ilitarajiwa kwamba kutokana na mabadiliko ya jamii na maendeleo ya kiteknolojia, maneno mengi yangepata maana za ziada na mengine kupata maana tofauti na maana asilia. Hivyo sivyo ilivyobainika. Mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na watoto yalibainisha kwamba maana za maneno

zilibanwa na nyingine kuhawilishwa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na jinsi upanuzi ulivyotokea. Viwango vya kutokea kwa michakato hiyo vimeelezwa hapo juu.

Lengo la nne la utafiti lilikuwa kuchunguza sababu za mabadiliko hayo. Miongoni mwa sababu hizo ni maendeleo ya jamii, kupotea kwa motisha ya matumizi, upolisemia wa maneno, ukuruba wa maana, maneno mwiko katika jamii, uzalishaji wa maana potovu na unasibu wa alama za kiisimu.

## 5.2 Hitimisho

Katika utafiti huu mtafiti alilenga kuchunguza mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba. Maneno yaliyochunguzwa ni nomino thelathini (30) na vitenzi ishirini (20). Utafiti umebaini kuwa maneno yote yaliyochunguzwa yalibadilika maana. Mabadiliko hayo yalisababishwa na michakato mbalimbali kama vile upanuzi wa maana, ubanaji, usambaratikaji, uimarikaji, usogezi na tasfida. Sababu za mabadiliko ya kisemantiki kwa mujibu wa utafiti zilikuwa za kiisimu na za kijamii.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya dhana inayodai kwamba maana za neno ni dhana inayoibuliwa na neno hilo akilini mwa mwanalugha wakati neno hilo linapotumika. Nadharia hii ilimwezesha mtafiti kupata maana za nomino na vitenzi vilivyotafitiwa kama zilivyokuwa awali na zilivyo sasa. Dhana zilizoibuka akilini mwa wazee zilitoa maana asilia za maneno na maana za ziada. Maneno yalipoandikwa ubaoni kwa ajili ya watoto yaliibua taswira akilini mwao na kutokana na taswira hizi maana ya sasa ya maneno hayo ilipatikana.

Pia kwa kuongozwa na nadharia hii, mtafiti aliweza kutambua iwapo watoto walitoa maana potovu au la. Uwezo wa kutambua ulitokana na umilisi wa lugha alio nao mtafiti kwa kuwa ni mzawa wa jamii-lugha iliyotafitiwa.

Nadharia ya pili iliyoongoza utafiti huu ni ile ya nyanja za kisemantiki. Utafiti uliiunga mkono nadharia hii kwa kubaini kwamba maneno yote yaliyotafitiwa hayakujisimamia kimaana bali yalihusiana na mengine katika nyanja za maana. Maneno mbadala yote katika B2 yalibeba maana moja ya maneno ya B1 isipokuwa nomino *ĩmisi* na kitenzi *nyala*.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umefanyika wakati ambapo serikali ya Kenya imebadilisha mfumo wa elimu ikakumbatia mfumo wa Elimu inayojikita katika Umilisi *CBC* (Competence-based Education). Mfumo huu unasisitiza ufunzaji wa lugha asili katika viwango vyote. Hata hivyo mfumo uliopita wa nane-nne-nne (8-4-4) umechangia pakubwa kudunisha lugha za asili kwa kutozipa nafasi ya kunawiri katika viwango vyote vya elimu. Nafasi finyu ya ukuaji wa lugha ya Kikamba na lugha nyinginezo za Kiafrika ilipewa darasa la kwanza hadi la tatu katika shule za mashambani.

Kutoendelezwa kwa ufunzaji wa lugha asilia katika viwango vya juu vya elimu kumeipokonya jamii ya Wakamba umilisi wa lugha yao asilia. Aidha, kumeidunisha lugha ya Kikamba hasa miongoni mwa wazawa wa karne hii ya ishirini na moja (21), ikawa ikichukuliwa kama lugha isiyofaa kuzungumzwa hadharani. Kwa hivyo mtafiti anapendekeza mambo yafuatayo:

Utafiti huu hauwezi kushughulikia kila jambo katika semantiki ya Kikamba. Kwa hivyo inapendekezwa tafiti zaidi zifanywe kuhusu mabadiliko ya kisemantiki ya aina nyingine za maneno kama vile vivumishi, vielezi, viunganishi, viwakilishi na vihisishi vya Kikamba ili kuchunguza iwapo vimebadilika maana.

Mtafiti alitumia *Biblia Takatifu* kama matini ya utafiti kwa hivyo anapendekeza matini nyinginezo zilizoandikwa kwa lugha ya Kikamba zikiwemo zile za fasihi zitumiwe

kupata data ya utafiti kuchunguza zaidi mabadiliko ya kisemantiki ya maneno katika lugha ya Kikamba.

Utafiti huu ulilenga lugha ya Kikamba. Ni vizuri lugha nyinginezo za kiasili nchini kote pia zichunguzwe.

Mtafiti anapendekeza kuandikwe kamusi za Kikamba kuendeleza msamiati wa lugha ya Kikamba na kufaidi kizazi cha karne hii ya 21 na vizazi vijavyo. Maana asilia na maana za ziada zioanishwe ili kupunguza utata uliopo wa kimawasiliano. Pia kamusi ya visawe katika Kikamba iandaliwe.

Itakuwa vyema iwapo waandishi wa vitabu wataandika vitabu vitakavyosomwa na wanafunzi wanaopitia mfumo wa sasa wa Elimu inayojikita katika Umilisi (CBE) na pia kuwafaa wanajamii kwa jumla.

Aidha, madhehebu ya Kikristo yanayotumia Biblia yatoe ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyokumbwa na mabadiliko ili kurahisisha Injili.

## MAREJELEO


Abuga, B. (2013). “Mabadiliko ya Lugha: Hali Maalum ya Lugha ya Ekegusii katika Eneo la Goseta kaunti ya Trans- Nzoia”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret (Haijachapishwa)

Alawadi, G. F. T. (2020). Translation based on Ogden and Richard’s semantic change triangle theory. JELITA: Journal of English Language Teaching and Literature. 1(1), 1-10.

Allan, K. n.w (2012). *Current Methods in Historical Semantics.* Berlin: De Gruyter Mouton

Antchison, J. (1991). *Language Change; progress or decay?* (2nd edition). Cambridge: Cambridge University Press.

Anttila, R. (1989). *Historical and Comparative Linguistics (2nd ed.).* Amsterdam: Benjamin.

Anusu, J. (2015). “Usawazishaji wa Leksimu katika Kiswahili: Utafiti kifani wa Vihiga”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Ashworth, E. J. (2020). *Locke on Language. Canadian Journal of Philosophy*, 14(1), 45-73.

Retrieved from https://doi.org/10.1080/00455091.1984.10716368

Babusa, H. (2019). “Ukopaji wa Lugha, Etimolojia na Mabadiliko ya Maana na Utamkaji wa Msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili”. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Berwick et.al (2016). *Why Only Us: Language and Evolution.* England: The MIT Press.

Bible Society of Kenya. (2011). *Mbivilia Uvoo Museo: Kikamba Interconfessional translation.*

Retrieved from https://www.bible.com/languages/kam

Blank, A. (1999). *Why do new meanings occur? A cognitive typology of the motivation for lexical semantic change*. Berlin, New York: Mouton de Gruyter.

Campbell, L. (2004). *Historical Linguistics.* Cambridge, MA: MIT Press.

Chapman, S. & Routledge, P. (eds) (2005). *Key Thinkers in Linguistics and the Philosophy of Language*. Edinburgh, U.K: Edinburg University Press.

Charles, W. G. (2000). Meaning and Context. *Three different Perspectives*, *Volume 3* (2), 13-17

Crowley, T., & Bowern, C. (2010). *An Introduction to Historical Linguistics* (4th ed.). Oxford University Press.

Retrieved from https://books.google.com/books/about/An-Introduction-to-Historical-Linguistic.html?id=RfpQEAAAQBAJ

Crystal, D. (2003). *Language Death.* Cambridge: Cambridge University Press.

David, J. (2009). "Uchanganuzi Semantiki wa Maneno Mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Denscombo, M. (2005). *The Good Research Guide for Small Scale Social Research Project.* New York: Open University Press.

Dube, W. & Wafula, R. S. (2017). *Postcoloniality, Translation and the Bible in Africa.* Oregon: Pickwick.

Enon, J. C. (1988). *Education Research Statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University Press.

Fordor, J. (1982). *Semantics: Thories of Meaning in Generative Grammar.* Brighton: The Harvester Press.

Fromkin, V., Rodman, R, & Hyams, N. (2014). *An Introduction to Linguistics.* New York: Holt, Reinehart &Winston Inc.

Geeraerts, D. (1997). *Diachronic Prototype Semantics: A Contribution to Historical Lexicology*. Oxford: Clarendon.

Geeraerts, D. (2010). *Theories of Lexical Semantics.* New York: Oxford University Press.

Gichuru, T. (2020). "Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo Linganishi wa Kikale na Kisasa". Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Habwe, J. na Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hale, M. (2007). *Historical Linguistics: Theory and Method.* Oxford: Blackwell.

Heinne, B. (2000). *African Languages: An Introduction.* Cambridge: Cambridge University Press.

Katz, J. (1972). *Semantic Theory*. New York: Harbor and Row.

Kibiki, J. M. (2012). "Mabadiliko ya Maana katika Vitenzi vya Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa)

Kihore, Y.M, Massamba, D. P. B. & Msanjila Y.P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu* (SAMAKISA): *Sekondari na vyuo*. Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam: TUKI

Kioko, D. (2012). *The Akamba People and Music*. Nairobi: Mvule Publishers.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: Wisha Prakashan.

Kresse, K. (2007). Ahmed Sheikh Nabhany Swahili Poetry and the concervation of cultural knowledge. In *Philosophising in Mombasa: Knowledge, Islam and intellectual practice on the Swahili Coast* (pp. 103-125). Edinburg University Press.

Leech, G. (1981). *Semantics.* Harmondsworth: Penguin.

Lyons, J. (1981). *Language; Meaning and Context.* California: Fontana Paperbags.

Lyons, J. (1999). *Language and Linguistics: An Introduction.* Cambridge: Cambridge University Press.

*Maandĩko Matheu ma Ngai Metawa Mbivilia Nĩmo Utianĩo Mũkũũ̃na Utianĩo Mweũ.* (2011). Nairobi: UBS Bible.

Martines, J. & Montserrat, S. (2015). "Semantic Change". *Catalan Journal of Linguistics, Volume 14,* uk.7-10.

Massamba, D. P. B. (1988). "Sababu za kubadilika kwa maana za maneno: Mifano katika Kiswahili". *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Juzuu ya 55,* uk.8-13.

Massamba, D. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha; Isimu na Nadharia.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mbiti, J. S. (1967). *African Religion and Philosophy.* Nairobi: East African Education Publishers.

McWhorter, J. (2020). *The Processes of Semantic Changes in Language*. Columbia University: Columbia.

Mey, J. (2001). *Pragmatics: An Introduction.* Oxford: Blackwell.

Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mojola, A. (2020). *God Speaks my Language.* U.K: Hippobook.

Mugambi, J. N. K. (1995). *From liberation to reconstruction: African Christian theology after the Cold War.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (2013). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts.

Musyimi, M. D. (2011). "Maana za Majina ya watu katika jamii ya Wakamba." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Musyoka, E. N. & Ireri, H. K. (2019). Types of Non- Equivalence in the Kikamba Bible Translation. *Open Access Library Journal, Vol.6,* (9), 1-21.

Muthoka, G. (2017). “Kikamba Language Shift and Endangerment in an Urban Upmarket Setting: A sociolinguistic Analysis”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Mwendamseke, F. (2016). “Uelekeo wa Maana za Kipolisemia katika Msamiati wa Kiswahili*:* Mifano kutoka Kamusi Sanifu ya Kiswahili”. *Kioo cha Lugha, juzuu 14* (1), uk 1-5.

Newmark, P. (2001). *Approaches to Translation.* Shanghai: Shanghai Foreighn Language Education Press.

Ngina, F. K. (2015). “A Semantic Analysis of Kikamba Spacial Expressions using the Cognitive Semantic Theory”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Nordquist, R. (2019, July 3). *Reflected meaning (Semantics).* ThoughtCo. https://www.thoughtco.com/reflected-meaning-semantics-1691904

Nzioki, S. (1982). *People of Kenya: The Akamba.* Nairobi: Evans Brothers.

Palmer, F. (1996). *Semantics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Prakasam, V. & Abbi, A. (2018). Semantics, stylistics & pedagogics. New Delhi, India: Allied Publishers.

Rajab, W. T. (2017). “Tathmini ya Mabadiliko ya Maana ya Msamiati wa Kiswahili katika Muktadha wa Kisiasa”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa)

Resani, M. (2014). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Riemer, N. (2010). *Introducing Semantics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Stehling, D. (2014). *Semantic change in the Early Modern English Period: Latin Influences on the English Language*. Hamburg, Germany: Anchor Academic Publishing.

Taylor, J.R. (1999). “Cognitive Semantics and Structural Semantics”. *Historical Semantics and Cognition.* pp. 17-47.

Trier, J. (1934). *Lexical Analysis: Norms and Exploitations*. Cambridge: MIT Press.

Traugott, E. & Richard, B. (2002). *Regularity in Semantic Change.* Cambridge: Cambridge University Press.

Tsunoda, T. (2006). *Language endangerment and Language revitalisation: An Introduction* (vol. 148). Berlin, Germany: Mouton de Gruyter.

Ullman, S. (1972). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Blackwell.

TUKI. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990). Dar es Salaam: TUKI.

Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic.,* New York: Routledge.

Wardhaugh, R. (2006). *An Introduction to Sociolinguistics (4th ed.)*. United States: Wiley- Blackwell.

Waruta, D. (1975). “Scripture Translation in Kenya”. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Willem, B. (2009). “Semantic change”. *English Language*: *Description, variation and context*, P.525-527.

Wittgenstein, L. (2009). *Philosophical Investigations* (P. M. S. Hacker& J. Schulte, Eds. & Trans., Rev. 4th ed.). Chichester, UK: Wiley-Blackwell.

Yule, G. (2000). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

# KIAMBATISHO I

# MASWALI YA KUONGOZA MAHOJIANO

Maneno yafuatayo yamekumbwa na mabadiliko ya kisemantiki tangu karne ya ishirini (20) hadi karne ya ishirini na moja (21).

1. Tafadhali nitajie kisawe cha kila neno kitumiwacho hivi sasa (karne ya 21) na maana.

2.Yatambue maneno ambayo hayatumiki tena katika mawasiliano ya kawaida katika karne hii ya 21.

3. Ni mambo gani unafikiri yamesababisha mabadiliko ya maneno hayo?

| Nomino | Kisawe | Maana |
|---|---|---|
| Asa | | |
| Ĩkanga | | |
| Ĩlawa | | |
| Ĩmisi | | |
| Isamũ | | |
| Ĩthweo | | |
| Kĩmũtũ | | |
| Manzĩ | | |
| Mata | | |
| Mathatwa | | |
| Mĩsyĩ | | |
| Mwenyu | | |
| Mwĩai | | |
| Ndũa | | |
| Ũkũngi | | |
| Wewa | | |

| Kitenzi | Kisawe | Maana |
|---|---|---|
| Kũka | | |
| Kwatwa | | |
| Meta | | |
| Mumunya | | |
| Nyala | | |
| Tambũka | | |
| Thilĩka | | |
| Vikĩla | | |
| Vuta | | |
| Ya ĩvu | | |

# KIAMBATISHO II

# MANENO YALIYOBADILIKA MAANA

Nomino

1.Asa

2.Ĩkanga

3.Ikuu

4.Ĩlawa

5.Ĩmisi

6.Inyia

7.Isamũ

8.Ĩthe

9.Ĩthweo

10.Ĩtu

11.Kĩmũtũ

12.Kĩseve

13.Kĩw'ũ

14.Maangi

15.Manzĩ

16.Mata

17.Mathatwa

18.Mbisũ

19.Mbota

20.Mĩsyĩ

21.Mũkate

22.Mũsikalĩ

23.Mũtumĩa

24.Mwenyu

25.Mwĩai

26.Mũsyi

27.Ndũa

28.Syĩndũ

29.Ũkũngi

30.Ũta

Vitenzi

1.Amũmumunya

2.Amũkumbatĩlya

3.Atĩĩa

4.Itava

5.Ĩthĩwa na kyeva

6.Ĩw’a nzaa

7.Kũka

8.Kwatwa

9.Meta

10.Milwa

12.Nyala

13.Semba

14.Tambũka

15.Tembea

16.Thata

17.Thilĩka

18.Umya

19.Vikĩla

20.Vuta

# KIAMBATISHO III

# MANENO YALIYOTEULIWA KUTOKA B1 NA B2

| **Nomino B1** | **B2** | **Kitabu ktk. Biblia** |
|---|---|---|
| Asa | Ĩthe | Mat.16:17; Lk.15:18 |
| Ĩkanga | Mũsikalĩ | Mat. 5: 25 |
| Ĩlawa | Mbota | Mat.16:6 |
| Ĩmisi | Mbisũ | Mat.5:15 |
| Isamũ | Syĩndũ | Lk. 12: 18 |
| Ĩthweo | Ĩtu | Mat.17:5 |
| Kĩmũtũ | Mũkate | Mat.4:4 |
| Manzĩ | Kĩw'ũ | Zab. 1:3 |
| Mata | Ũta | Zab. 37:14, Mat.27:30 |
| Mathatwa | Ikuu | Lk.5:37 |
| Mĩsyĩ | Maangi | Zab. 18:14 |
| Mwenyu | Inyia | Lk. 8:20 |
| Mwĩai | Mũtumĩa | Mw. 18:12,31 |
| Ndũa | Mũsyĩ | Lk. 22:10 |
| Ũkũngi | Kĩseve | Zab.1:4 |

| **Vitenzi B1** | **B2** | **Kitabu ktk. Biblia** |
|---|---|---|
| Kũka | Semba | Mw.14:10 |
| Kwatwa | Milwa | Mw.9:21 |
| Meta | Ĩthĩwa na kyeva | Mat.9:15 |
| Mumunya | Kumbatĩlya | Lk.15:20 |
| Nyala | Ĩw'a nzaa | Mw.25:30 |
| Tambũka | Tembea | Mw.3:8 |
| Thilĩka | Thata | Mw.31:36 |
| Vikĩla | Atĩĩa | Lk.9:23 |
| Vuta | Umya | Lk.10:30 |
| Ya ĩvu | Itava | Mw.16:4 |

# KIAMBATISHO IV

**MACHAKOS UNIVERSITY**
**OFFICE OF THE DEAN GRADUATE SCHOOL**

Telephone:254-(0)735247939, (0)723805929
Email: graduateschool@mksu.ac.ke
Website: www.machakosuniversity.ac.ke

P.O Box 136-90100
Machakos
**KENYA**

REF. MksU/GS/N/036/VOL.1

3rd November, 2022

The Director,
National Commission for Science, Technology and Innovation
P.O Box 30623,
**NAIROBI**

Dear Sir

**RE: ANGELA NTHENYA MUSYOKA (C50/12733/2017)**

The above named is a Masters student in the second year of study and has cleared course work. The University has cleared her to conduct a research entitled: **"Mabadiliko Ya Kisemantiki Ya Maneno Katika Lugha Ya Kikamba: Mtazamo Wa Kidayakronia."**

Kindly assist her with a Research Permit in order to undertake the research.

Thank you.

DEAN OF GRADUATE SCHOOL
P.O. Box 136-90100, MACHAKOS
04 NOV 2022
MACHAKOS UNIVERSITY

**PROF. KIMITI RICHARD PETER, PhD**
**DEAN GRADUATE SCHOOL**

KRP/em

# KIAMBATISHO V

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **646825**

Date of Issue: **23/December/2022**

**RESEARCH LICENSE**

**This is to Certify that Ms.. Angela Nthenya Musyoka of Machakos University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Machakos on the topic: MABADILIKO YA KISEMANTIKI YA MANENO KATIKA LUGHA YA KIKAMBA: MTAZAMO WA KIDAYAKRONIA for the period ending : 23/December/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/22881**

**646825**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**